

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Ishirini na Sita – Tarehe 10 Mei, 2021

(Bunge Lillanza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tukae.

Katibu.

NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,
WAZEE NA WATOTO:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Katibu.

NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

NAIBU SPIKA: Maswali, tutaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle, Mbunge wa Lupembe, sasa aulize swali lake.

Na. 215

Kuvutia Wawekezaji wa Parachichi - Njombe

MHE. EDWIN E. SWALLE aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuvutia Wawekezaji katika kilimo cha Parachichi mkoani Njombe.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (UWEKEZAJI)
aliibusi:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle, Mbunge wa Lupembe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia mwaka 2020, thamani ya zao la parachichi katika Soko la Dunia inakadiriwa kuwa Dola za Kimarekani milioni 4,800. Kwa Ukanda wa Kusini mwa Jangwa la Sahara, soko la parachichi linakadiriwa kuwa na thamani ya Dola za Kimarekani milioni 254. Aidha, nchi yetu imeendelea kufanya vizuri katika uzalishaji na uuzaaji wa zao la parachichi katika masoko ya ndani na ya Kimataifa kama vile Umoja wa Ulaya, China, India na Kenya. Hivyo, mwaka 2020 kiasi cha Dola za Kimarekani milioni nane kilipatikana kutohana na wastani wa kiasi cha tani 4,000 zilizosafirishwa katika Soko la Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Awamu ya Sita imedhamiria kuboresha mazingira ya uwekezaji nchini na ufanyaji wa biashara kwa kushughulikia kero zitokanazo na ukadiriaji na ukasanyaji wa kodi usio rafiki; upatikanaji mgumu

wa ardhi unaochukua muda mrefu kwa ajili ya uwekezaji; changamoto za upatikanaji wa vibali nya kazi na ukaazi; na kuondoa tozo mbalimbali ambazo ni kero katika Serikali za Mitaa. Hadi sasa, jumla ya tozo 273 ambazo zilikuwa kero kwa wawekezaji zimefutwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza Sera ya Uwekezaji, Serikali imeendelea kuweka mazingira rafiki ya uwekezaji ikiwa ni pamoja na kutoa vivutio kama vile misamaha ya kodi kwenye makasha/majokofu (*cold rooms*) yanayotumika kuhifadhi mazao ya bustani ikiwemo zao la parachichi. Aidha, Serikali ina mpango wa kujenga chumba baridi katika uwanja wa ndege wa Songwe, ambapo ndege za Kimataifa zinazobeba mizigo zitaanza kusafirisha parachichi na mazao mengine ya matunda na mboga mboga moja kwa moja kwenda kwenye masoko ya Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, Serikali imepanga kujenga jengo lijulikanalo kama ukanda wa kijani katika bandari ya Dar es Salaam kwa ajili ya kuhifadhi bidhaa na mazao yanayoharibika mapema likiwemo zao la parachichi. Jithada nydingine ni pamoja na kutafuta masoko ya nje, kuhakikisha upatikanaji wa mbegu bora, kuimarisha miundombini ya umwagiliaji, uhifadhi, uchukuzi na usafirishaji. Serikali itaendelea kushirikiana na wadau wote ikiwemo sekta binafsi katika kukuza uwekezaji wa zao la parachichi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle, swali la nyongeza.

MHE. EDWIN E. SWALLE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nashukuru pia kwa majibu mazuri ya Serikali kuhusu swali hili. Ninalo swali moja tu la nyongeza.

Kwa kuwa zao hili la parachichi limeanza kupata msukumo mkubwa na wananchi wengi wanaendelea kulima zao hili katika mikoa mbalimbali hapa nchini ikiwemo mikoa ya nyanda za juu kusini hasa katika Mikoa ya Mbeya, Njombe, Songwe na Rukwa ; na wananchi wengi wanalima zao hili

kwa njia za asili bila kufuata taratibu za kilimo bora: Je, Serikali haioni haja sasa kulisimamia zao hili kwa ukaribu ili wakulima walime kwa tija kwa kuzingatia kilimo bora cha parachichi. (*Makof*).

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwekezaji, Mheshimiwa William Tate Olenasha majibu kwa swali hilo muhimu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (UWEKEZAJI): Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kama nilivyosema kwamba zao hili la parachichi ni katika mazao ambayo kwa sasa kwa kweli yameleta matumaini makubwa kwa ajili ya kuwanufaisha wananchi wetu. Ndiyo maana kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi, Serikali imeanza kuweka mikakati ya kuhakikisha kwamba wananchi wanaweza wakazalisha zao hili kwa wingi zaidi na katika mazingira bora zaidi ili kuweza kukidhi ushindani uliopo Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kwamba sehemu ya mkakati huo ni pamoja na Wizara ya Kilimo kuanza kujikita kutayarisha mkakati wa kulima mazao ya mboga mboga. Mkakati unaoanzia mwaka 2021 mpaka mwaka 2030 ambao pamoja na mambo mengine utahakikisha kwamba kunakuwa na mbegu bora, kunakuwa na kilimo ambacho kina tija; pia Serikali imeanza kuangalia zaidi katika masoko hayo ya Kimataifa ambayo tumesema kwa kweli ni mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukijaribu kuangalia uzalishaji wetu bado ni tani 4,000 wakati dunia nzima zinahitajika zaidi ya tani 2,000,000. Kwa hiyo, fursa bado zipo na ndiyo maana tumeweka mikakati mbalimbali ya kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanaweza wakazalisha kwa ubora zaidi.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa, tunaenda Ofisi ya Rais TAMISEMI. Mheshimiwa Jonas William Mbunda, Mbunge wa Mbinga Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 216

Kujenga kwa Kiwango cha Lami Barabara za Mbinga Mji

MHE. JONAS W. MBUNDA aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami katika Mji wa Mbinga?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Jonas William Mbunda, Mbunge wa Jimbo la Mbinga Mjini, kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Mbinga Mji, ina barabara zenyeye urefu wa kilomita 7.45 zilizojengwa kwa kiwango cha lami zikiwemo kilomita 0.2 zilizojengwa katika mwaka wa fedha 2020/2021 kwa gharama ya shilingi milioni 170. Aidha, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali imetenga shilingi milioni 500 kwa ajili ya kumalizia ujenzi wa barabara ya Mbuyula Hospitali hadi Ikulu ndogo yenye urefu wa kilomita moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kujenga na kukarabati miundombinu ya barabara nchini kote ikiwemo Halmashauri ya Mji wa Mbinga kwa kadri ya upatikanaji wa fedha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Jonas William Mbunda, swalii la nyongeza.

MHE. JONAS W. MBUNDA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza niishukuru Serikali kwa majibu mazuri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, Mji wa Mbinga unakua kwa kasi na kipindi cha mvua barabara nyingi ambazo zimejengwa kwa

kiwango cha changarawe huwa zinaharibika. Je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa kuongeza kiasi kilichotengwa katika msimu wa 2020/2021 na 2021/2022 ili kuhakikisha kwamba angalau kipande kirefu kijengwe ili kukidhi matakwa ya wananchi wa Jimbo la Mbinga Mjini?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Serikali imefanya vizuri sana katika *program* ya *ULGSP* na *TSCP* na kuna uwezekano mradi wa *TACTIC*, je, Halmashauri ya Mbinga Mjini itakuwepo katika *programu* hii ya *TACTIC*?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nipate majibu ya Serikali. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Swali la kwanza la Mheshimiwa Mbunge alikuwa anaomba tu kwamba katika bajeti ya mwaka 2021/2022 Serikali iweze kuongeza fedha katika Mji wa Mbinga Mjini ili angalau Serikali iendelee kujenga barabara nyingi za kutosha. Kwa sababu bajeti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI ilishapitishwa na kiwango tulichokitenga kwa ajili ya fedha kipo kulingana na ukomo, lakini katika majibu yetu ya msingi tumeainisha hapo kwamba kwa kadri fedha zitakavyoendelea kupatikana, udharura na kadhalika, tutaendelea kupeleka fedha katika Halmashauri ya Mji Mbinga ili wananchi wake waweze kupata barabara nzuri na zinazopitika wakati wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ameuliza kama Mji wa Mbinga upo katika ule mradi wa *TACTIC*. Nimwambie tu kabisa kwamba katika ule mradi, Halmashauri ya Mji Mbinga ipo. Ni sehemu ya ile miji 45 ambayo imeainishwa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Aida Khenani, swali la nyongeza.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Kutokana na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, anasema wataendelea kujenga barabara kadri wanavyopata fedha, lakini kuna maeneo ambayo yana changamoto kubwa. Napenda kujua, kuna maeneo ambayo hayapitiki kabisa ikiwemo kule kwangu Nkasi, Barabara ya Kasu – Itindi ambayo mpaka sasa wanawake wanajifungulia njani kutokana na uharibifu wa barabara :-

Je, ni lini Serikali itakuwa na kipaumbele kwa maeneo ambayo yana changamoto kubwa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mheshimiwa Silinde, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Mheshimiwa Mbunge amejaribu hapa kuainisha kwamba tutaendelea kujenga kwa kadri ya upatikanaji wa fedha. Katika yale maeneo ambayo kuna shida kubwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI (*TARURA*) tuna fungu la dharura kwa ajili ya kurekebisha maeneo korofi kama hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, endapo patakuwa na shida basi tumekuwa tukipeleka timu ya wataalam kufanya tathmini na baada ya hapo tumekuwa tukitoa fedha kama ambavyo tunaendelea katika maeneo mbalimbali nchini hivi sasa. Kwa hiyo, katika hilo eneo ambalo ameliainisha, naiagiza Ofisi ya Raisi, TAMISEMI (*TARURA*) kwamba waende wakafanye tathmini halafu baada ya tathmini wailete kwetu tuone namna gani tunaweza tukasaidia wananchi wa Jimbo lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Hhayuma.

MHE. SAMWELI X. HHAYUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona. Changamoto ya barabara iliyopo Mbanga ni sawa sawa na changamoto iliyopo kwenye Jimbo

langu la Hanang hasa Mji wa Katesh. Ule ni Mji ambao una umri zaidi ya miaka 30 na kitu ukiwa ni Makao Makuu ya Wilaya lakini hakuna kilometra hata moja ya lami :-

Je, Wilaya ina mpango gani angalau kuweka kilometra 10 za lami ambayo pia ni ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Sita?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge amejaribu kuainisha hapa barabara ambazo ni ahadi za viongozi na sasa hivi nikuhakikishie tu kwamba Serikali ipo katika Mpango wa Kukusanya ahadi zote na kuziweka pamoja, kuzifanya tathmini pamoja na kuzitengea bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hicho ambacho amekieleza katika Mji wa Katesh ambapo mahitaji yao yapo, nimhakikishie kuwa ahadi zote za viongozi tutazainisha, tutazitenga katika bajeti kwa ajili ya utekelezaji ikiwemo katika mji wake wa Katesh.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa, tuendelee na swali la Mheshimiwa Felista Deogratius Njau, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 217

**Kukamilisha Ujenzi wa Barabara ya Kairuki -
Mikocheni - Shoppers – Kawe**

MHE. FELISTA D. NJAU aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kukamilisha ujenzi wa barabara ya Kairuki hadi Mikocheni *Shoppers* ambayo hadi sasa imejengwa kipande kidogo.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Felista Deogratias Njau, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Kairuki hadi Mikocheni *Shoppers* inayojulikana kwa jina la Barabara ya Warioba - Chakwu yenye urefu wa kilomita 1.73 ilijengwa kwa kiwango cha lami kipande cha kilometa 1.13 kwa gharama ya shilingi bilioni 1.017 katika mwaka wa fedha 2014/2015. Hivyo, kipande chenye urefu wa kilomita 0.6 hakikujengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii yote inahitaji matengenezo makubwa kikiwemo kipande cha kilometa 0.6 ambacho hakina lami. Katika mwaka wa fedha 2021/2022 *TARURA* Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni imepanga kufanya tathmini ya barabara hii na Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya kujenga na kuifanyia matengenezo barabara hii kwa mujibu wa matokeo ya tathmini.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Felista Deogratias Njau, swali la nyongeza.

MHE. FELISTA D. NJAU: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niseme kwamba katika Jimbo la Kawe kuna barabara kama hizo ambazo ni sugu kama Barabara ya Ununio – Malindi, Mbweni – Teta mpaka Mpiji. Barabara hii inajengwa lakini inasuasua kwa muda mrefu: Ni lini sasa Serikali itamalizia barabara hii ili wananchi hawa waweze kupata nafuu?

Swali la pili, ni mkakati gani endelevu wa Serikali ambao sasa baada ya barabara hizi kujengwa wataweka mitaro ambayo haitaathiri barabara hizi kwa sababu

imeonekana barabara nyingi zinaharibika kwa sababu ya mitaro? Ahsante. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Silinde, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Mheshimiwa Mbunge amejaribu kuainisha baraba nyingine katika Jimbo la Kawe ambazo ni mbovu ikiwemo barabara ya Ununio – Malindi, Mbweni – Teta mpaka Mpiji na akaiomba Serikali izitengeneze. Najua Mheshimiwa Mbunge anafanya kazi nzuri na mimi nimwahidi kabisa kwamba kama tulivyozungumza katika swalii letu la msingi, tutaendelea kufanya tathmini na kadri tutakavyopata fedha hizo barabara zitatengenezwa. Hiyo ndiyo nia ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na mama yetu Mheshimiwa Samia Hassan Suluhu.

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili amejaribu kuainisha kwamba ni mkakati gani ambao unaweza kusaidia zile barabara zetu zisiharibike ikiwemo kujenga mitaro itakayopitisha maji nyakati za mvua? Hata hiyo, Mheshimiwa Mbunge anatambua kabisa kwamba kuna mpango mkubwa wa *DMDP* wa ujenzi wa barabara kwa maana ya miundombinu yote katika Jiji la Dar es Salaam. Sehemu ya fedha ambazo zipo ni pamoja na kujenga mitaro ili kuhakikisha barabara zetu zote zinakuwa na ubora katika muda wote. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge nikuhakikishie mkakati wa Serikali ni pamoja na kuendelea kujenga mitaro, madaraja na kuziboresha barabara zetu kwa kipindi chote. Ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Christine Mnzava, swalii la nyongeza.

MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi kuuliza swalii la nyongeza. Kwa kuwa changamoto ya Barabara ya Kairuki ni sawa kabisa na changamoto iliyopo katika barabara ya kutoka

Ndala kwenda Mwawaza kwenye Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Shinyanga. Je, ni lini Serikali itatoa fedha kukamilisha barabara hiyo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu kwa swali hilo.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Christina Mnzava, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge ameainisha Barabara ya Ndala – Mwawaza kuelekea Hospitali ya Shinyanga. Ameuliza ni lini Serikali itaikamilisha. Niseme tu kwamba, tutaikamilisha kwa kadri ya upatikanaji wa fedha na tathmini ambazo zinaendelea kufanyika. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge awe na subira, hiyo barabara itajengwa kwa kadri tutakavyopata fedha. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Issa Mtemvu, swali la nyongeza.

MHE. ISSA J. MTEMVU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniona. Kwa kuwa, ndani ya Jimbo la Kibamba ipo barabara ya Temboni – Msingwa kwenda Kinyerezi ina changamoto kubwa sana kwa muda mrefu. Je, mchakato unaoendelea kupata mkandarasi ni lini utakamilika na barabara hiyo kuanza kujengwa chini ya TARURA?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Silinde, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Issa Mtemvu, Mbunge wa Kibamba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge ameainisha kwamba, barabara ya Temboni – Msimbwa kwenda Kinyerezi imeharibika na anataka kujua lini barabara hii itanza kujengwa. Nimwambie tu kwamba, mchakato unaendelea na mchakato utakapokamiliika kama ambavyo ye ye ameainisha, tutakapomaliza huu mchakato hii barabara itanza kujengwa mara moja kwa sababu, tumeshaitenga katika bajeti. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Tunaendelea na Wizara ya Viwanda na Biashara. Mheshimiwa Hamis Mohamed Mwinjuma, Mbunge wa Muheza, sasa aulize swali lake.

Na. 218

Hitaji la Kiwanda cha Kuchakata Viungo – Muheza

MHE. HAMIS M. MWINJUMA aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango mkakati gani wa kuhakikisha kuwa kunajengwa Kiwanda cha Kuchakata Viungo Wilayani Muheza?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Exhaud Kigahe, majibu.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hamis Mohamed Mwinjuma, Mbunge wa Jimbo la Muheza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua umuhimu wa viwanda katika kuchangia ukuaji wa uchumi nchini, Serikali imeendelea kuweka mazingira rafiki na wezeshi kwa Sekta Binafsi ili iweze kuanzisha na kuendeleza shughuli za viwanda hapa nchini. Aidha, Wizara kuititia Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (*SIDO*) inaendelea kutoa huduma mbalimbali zinazohusiana na uanzishwaji wa

viwanda vidogo na vya kati ikiwa ni pamoja na mafunzo juu ya usindikaji wa mazao ya kilimo, uendelezaji teknolojia rahisi za uongezaji thamani mazao ya kilimo, utafutaji wa masoko ya bidhaa zinazozalishwa na wajasiriamali na kutoa mikopo kwa masharti nafuu kupitia Mfuko wa Taifa wa Kuendeleza Wajasiriamali Wananchi (*NEDF*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Muheza ina viwanda vidogo vitatu kwa ajili ya kuchakata viungo. Viwanda vinavyofanya kazi ni viwili ambavyo ni *Trianon Investment Limited* kilichopo eneo la Lusanga, Muheza Mjini, ambacho mwaka 2020 kimeuza nje jumla ya tani 120 za viungo ambavyo vimechakatwa katika kiwanda hicho. Kiwanda cha pili ni *G.F.P Organic Limited* kilichopo barabara ya kuelekea Pangani ambacho mwaka 2020 kiliuza nje jumla ya tani 80 za viungo.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda hivyo vinahudumiwa na Shirika letu la *SIDO* na vimetoa ajira za kudumu zipatazo 30 na vibarua zaidi ya 50. Viungo vinavyochakatwa ni pamoja na iliki, mdalasini, pilipili manga, karafuu, mchaichai, binzari, maganda ya machungwa na limao. Aidha, kiwanda cha *Raza Agriculture Limited* kilichopo katika Kijiji cha Muungano, Muheza, kinatarajia kuanza uzalishaji hivi karibuni.

Pamoja na viwanda hivyo wilayani Muheza kuna wajasiriamali wadogo wengi ambao husindika viungo katika ngazi za kaya (*household level*). Serikali kupitia Shirika la Viwanda Vidogo (*SIDO*), Shirika la Viwango Tanzania (*TBS*) na Mamlaka ya Biashara Tanzania (*TANTRADE*) inawasaida wajasiriamali hao kuwapatia mafunzo na ushauri ili waweze kuzalisha kwa ubora unaotakiwa na kuuza bidhaa zao katika masoko ya ndani, kikanda na kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wote kushirikiana na Serikali katika kuhamasisha Sekta Binafsi kuwekeza zaidi katika ujenzi wa viwanda vya kuchakata viungo nchini ikiwemo katika Jimbo la Mheshimiwa Hamis, Jimbo la Muheza.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Hamis Mohamed Mwinjuma, swali la nyongeza.

MHE. HAMIS M. MWINJUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri kwa niaba ya Serikali na ambayo yananipeleka kwenye maswali mawili ya nyongeza. Mionganoni mwa matatizo makubwa ya kilimo na biashara ya viungo Wilayani Muheza ni kukosekana kwa ardhi kubwa ya kulimia mazao hayo kule ambako yanastawi. Pia na viwanda vya kuyachakata kulekule kwenye Tarafa ya Amani, ili kuyaongezea thamani kwa vile kule hakuna kiwanda hata kimoja. Sasa kuna ekari 35,063 ambazo ziko chini ya Kampuni ya *East Usambara Tea Company* ambazo zilikuwa na viwanda viwili ambavyo kwa sasa ni magofu na zinazotumika ni ekari 4,909 tu kwa miaka mingi na viwanda hivi vimegeuka magofu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, je, Serikali haionti hivi sasa ni wakati wa kuvirudisha viwanda hivi kwenye umiliki wake, ili kuwasaidia wananchi ikiwa ni kwa kuwekeza yenyeve ama kwa kushirikiana na wawekezaji wapya *serious* ili wananchi wa Amani wapate kupata viwanda vya kuongeza thamani mazao yao ya viungo kule? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; tatizo la aina hii, Waheshimiwa Wabunge wanaweza kuwa mashahidi, limekuwa likitokea sehemu nyingi ambapo wawekezaji wamekuwa wakiomba kumilikishwa viwanda hivi kwa ahadi ya kuvifufua na kuzalisha ajira pamoja na kuliongezea pato Taifa, lakini badala yake wamekuwa wanaviuwa na kuvigeuza kuwa magofu. Je, Serikali haionti sasa ni wakati wa kuwa aidha na sheria kali zaidi ama kutunga sheria mpya ili tusiendelee kuchezewa na viwanda vyetu vifanye makusudio yaliyokuwepo wakati vinaanzishwa? Nakushukuru. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Kigahe, majibu.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya

nyongeza ya Mheshimiwa Hamis Mohamed Mwinjuma, Mbunge wa Jimbo la Muheza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Hamis Mwinjuma kwa kufuutilia sana maendeleo, hasa sekta ya viwanda katika jimbo lake. Amenifuata mara nyingi kuhusiana na viwanda hivi, hasa vyatya hivi vyatya *East Usambara Tea Company Limited*, ambavyo viko pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kuhusu suala la ardhi. *East Usambara Tea Company Limited* ina ekari 35,000 kama alivyosema na katika ekari hizo ni ekari 2,027 tu ndio zimepandwa chai na ekari 600 zimepandwa miti, kwa maana ya miti ile inayotumika kama nishati, kuni kwa ajili ya kutumika katika viwanda hivyo. Pia eneo lingine maeneo yaliyobakia ambayo yanamilikiwa na kampuni hii yanatumika kwanza katika sehemu nyingine ni vyanzo vyatya maji, lakini maeneo mengine ni *natural reserve* kulingana na utaratibu wa UNESCO kwamba, huwezi kutumia mazingira yote kulima, kwa hiyo, maeneo mengine makubwa yako katika mazingira ya *reserve*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kutokana na uhitaji wa wakulima katika Jimbo la Muheza, tutaona namna gani kushirikiana na wenye kampuni, ili tuone kama wanaweza kutoa sehemu kidogo ambayo inaweza kutumika na wakulima wadogowadogo kwa ajili ya kuzalisha viungo ambavyo vitatumika katika viwanda vyatya kuchakata viungo kama alivyoomba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uwekezaji katika viwanda hivyo. Nimjulishe tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, pamoja na ufuutiliaji huo wote, lakini viwanda hivi sasa vinafanya kazi vizuri. Uwezo uliosimikwa kwa viwanda vile viwili ambavyo vinafanya kazi vyatya Bukwa na Kwamkoro vina uwezo wa kuchakata kilo 120 kwa siku, lakini sasa hivi vinaweza kupata *raw material* kwa maana ya malighafi zaidi ya kilo 90,000. Kwa hiyo, maana yake viwanda hivi vinafanya kazi vizuri, lakini kuna viwanda vile viwili ambavyo kutokana na

mahitaji haya wenye viwanda, Kampuni ya *East Usambara Tea Company Limited*, walivigeuza kama ma-godown, ambavyo vilikuwa Viwanda vya Munga na Nderema, lakini pia baadaye, nimjulishe tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, kampuni hii ina mpango sasa wa kuanza ku-pack kwa maana ya *blending* ya ile chai wanayozalisha pale badala ya kwenda kuuza kwenye minada ya Mombasa na kwingine, wataanza kufanya *blending* pale. Kwa hiyo, tuna mpango wa kuwasaidia ili wafufue viwanda hivi viwili viweze sasa kufanya *blending* badala ya kuwa *store* au magofu kama yalivyo sasa.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Madini; Mheshimiwa Boniphace Nyangindu Butondo, Mbunge wa Kishapu, sasa aulize swali lake.

Na. 219

**Mgodi wa Mwadui *Williamson Diamond Limited*
Kuanza Uzalishaji**

MHE. BONIPHACE N. BUTONDO aliuliza:-

Je, ni kwa nini Mgodi wa Mwadui *Williamson Diamond Limited* umesimamisha shughuli za uzalishaji wa almasi kwa muda mrefu na ni lini mgodi huo utaanza uzalishaji tena?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini. Mheshimiwa Profesa Shukrani Manya, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Boniphace Nyangindu Butondo, Mbunge wa Jimbo la Kishapu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mgodi wa Mwadui unaomilikiwa na Kampuni ya *Williamson Diamond Limited*

ulisimamisha shughuli za uzalishaji mwezi Aprili, 2020 na hii ni kutokana na kushindwa kumudu gharama za uzalishaji kufuatia anguko la bei ya madini ya almasi katika masoko ya dunia. Anguko la bei ya almasi katika soko la dunia liliababishwa na athari za ugonjwa wa *COVID-19* mwishoni mwa mwaka 2019. Athari ya kuanguka kwa bei hii ya almasi kulisababisha bei ya wastani ya almasi katika mauzo ya mgodi huo kwa mwezi Machi, 2020 kuanguka hadi kufikia Dola za Kimarekani 131.13 kwa karati, bei ambayo kimsingi haikidhi gharama za uzalishaji wa mgodi huo. Kwa mujibu wa makadirio ya mgodi huo wastani wa bei unapaswa kuwa angalau Dola za Kimarekani 208 kwa karati ili mgodi uweze kukidhi gharama za uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mgodi huo utanza tena uzalishaji baada ya maombi yao ya *overdraft funds* kukubalika na benki za hapa nchini. Hii ni kwa ajili ya kugharamia shughuli zao za uzalishaji angalau kwa kipindi cha miezi mitatu hadi kufikia awamu nyingine ya mauzo ya almasi. Hali ya bei ya almasi kwenye soko la dunia kwa sasa inatarajiwa kuwa bora zaidi ikilinganishwa na kipindi cha mwaka 2020.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Boniphace Butondo, swalil ya nyongeza.

MHE. BONIPHACE N. BUTONDO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nishukuru sana kwa majibu ya Serikali yaliyotolewa na Naibu Waziri. Kwanza nipongeze kwa jitihada hizi ambazo zinaendelea, lakini bado lipo tatizo kubwa la hizi benki ambazo Mgodi wa Mwadui umekwenda kwa ajili ya kuomba mkopo huu ilimradi uanze uzalishaji kwa mara nyingine. Jambo kubwa linalohitajika hapa ni hii *corporate guarantee* ambayo inatakiwa itolewe na Petra ambaye ndiye kimsingi mwekezaji wa Mgodi huo wa Mwadui, lakini jambo ambalo nadhani ni zuri zaidi kwa Serikali ni kuhakikisha inazungumza ama inakaa kwa karibu na Petra, ilimradi suala hili la *corporate guarantee* liweze kutolewa na Petra na badaye utaratibu wa kutolewa fedha na ili mgodi uweze kuzalisha ufanyike haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia...

NAIBU SPIKA: Uliza swali Mheshimiwa.

MHE. BONIPHACE N. BUTONDO: Mheshimiwa Naibu Spika, swali, liko tatizo kubwa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu Serikali yenyewe, lakini pia na suala zima la *Service Levy* pamoja na *CSR* ambayo imekuwa ni msaada mkubwa kwa shughuli za maendeleo kwa wananchi wa Kishapu. Ni lini sasa Serikali itakwenda kusimamia na kushirikiana na hawa ma-banker ilimradi benki hizi ziweze kutoa fedha na kuweza kuzalisha? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa swali la pili nenda moja kwa moja kwenye swali.

MHE. BONIPHACE N. BUTONDO: Mheshimiwa Naibu Spika, wako watumishi zaidi ya 1,200 pale katika Mgodi wa Mwadui na changamoto kubwa ya hawa watumishi ni mishahara yao kusimama kwa muda mrefu. Sasa ipo sababu ya Serikali kuona umuhimu wa mgodi huu kuhakikisha unaanza uzalishaji, ili adha na matatizo makubwa ya watumishi hawa waliopo katika Mgodi wa Mwadui waondokane na adha hii kubwa. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, Profesa Shukrani Manya, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze Mbunge pia kwa kutambua kwamba, Wizara inafanya kila linalowezekana kuona kwamba, mgodi huu unarejea katika hali ya uzalishaji. Kwa swali lake la kwanza, lakini pia ni kweli kwamba, natambua Wizara itafanya kila linalowezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumza uzalishaji wa almasi Tanzania tunaongea habari ya Mgodi wa *WDL* ndio kiini kikubwa cha uzalishaji wetu wa almasi. Pia,

tunatambua adha ambayo watumishi wanapata kwa kushindwa kulipwa mishahara, lakini pia tunatambua kwamba, kama uzalishaji hautafanyika kwa muda mrefu maana yake ni kwamba, hata shimo lile tunapochimba litaanza ku-*cave in* na kwa hiyo, gharama ya kuja kuanzisha mgodi mara nydingine itakuwa ni kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nipende kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, Wizara ya Madini itafanya kila linalowezekana, iwe ni kuongea na watoa huduma, iwe ni kuendelea kufanya ushawishi wake kwa ajili ya benki za hapa nchini na hata kuongea na Petra, ili ikiwezekana basi turejee katika uzalishaji. Mara tutakapoanza uzalishaji maana yake ni kwamba, matatizo yote aliyoaa inisha Mbunge ya adha ya watumishi kutolipwa pamoja na *service levy* yote vitakuwa vinapatiwa suluhisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Wizara itafanya kila njia inayowezekana; yaweza kuwa ni ushawishi kwa benki zetu, hilo moja, au kukaa na watoa huduma ili kwamba, wakubali kufanya hata kwa kukopwa ili baadaye tuzalishe halafu tuuze. Njia zozote ambazo zinaweza zikarejesha uzalishaji katika Mgodi wa *WDL* tutazi-pursue ili kwamba, tuweze kurejesha hali ya uzalishaji katika Mgodi wetu wa Almasi Tanzania. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Kilimo. Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mbunge wa Bunda, sasa aulize swali lake.

Na. 220

Upungufu wa Mafuta ya Kula Nchini

MHE. BONIPHACE M. GETERE aliuliza:-

(a) Je, ni nini kinasababisha Tanzania kutojitosheleza kwa mafuta ya kula?

(b) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha mikoa yenye ardhi ya kutosha ya kuzalisha zao la alizeti hususan Mkoa wa Mara inatambuliwa rasmi na kupewa mahitaji yote ya mbegu?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Boniface Mwita Getere, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mahitaji ya mafuta ya kula nchini yanakadiriwa kuwa wastani wa tani 570,000 kwa mwaka. Hata hivyo, uzalishaji wa mafuta ya kula nchini unakadiriwa kufika wastani wa tani 205,000 na kufanya upungufu wa wastani wa tani 365,000 kwa mwaka, ambapo husababisha nchi kutumia wastani wa Shilingi bilioni 474 kuagiza mafuta ya kula kutoka nje kwa mwaka.

Aidha, uhaba wa mafuta ya kula nchini umetokana na uzalishaji mdogo wa mazao ya mbegu za mafuta yakiwemo alizeti, michikichi, pamba unachangiwa na matumizi hafifu ya teknolojia ikiwemo mbegu bora na usindikaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kuhamasisha kilimo cha mazao ya mafuta ikiwemo alizeti, michikichi na pamba katika mikoa yote yenye ardhi na hali ya hewa inayofaa kwa kilimo cha mazao hayo. Aidha, Serikali imeweka msukumo wa kuimarisha huduma za ugani nchini ambapo katika bajeti ya 2021/2022, Wizara imepanga kuwezesha Maafisa Ugani 680 wa Mikoa ya Singida, Dodoma na Simiyu pikipiki kwa ajili ya ufuutiliaji, kupatiwa mafunzo rejea na kuwezesha wagani hao kuanzisha mashamba ya mfano ya alizeti na pamba pamoja na kuanzisha mashamba ya (*Block Farm*) ambayo tunafanya pamoja na Wizara ya

Ofisi ya Waziri Mkuu. Lengo la uwezeshaji huo ni kuleta ufanisi katika kutoa huduma za ugani ili kuongeza tija na uzalishaji wa mazao ya mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2021/2022, Serikali itawekeza jumla ya bilioni 10 kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa mbegu bora za mazao yakiwemo ya mbegu za mafuta kwa kuimarisha miundombinu ya umwagiliaji na kupanua mashamba ya mbegu ya Wakala wa Serikali (ASA), mbegu hizo zitasambaza kwa wakulima kwa Mikoa yote itakayozalisha mazao hayo ikiwemo Mkoa wa Mara kuitia ASA na wasambazaji binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha Serikali inaendelea kuhamasisha sekta binafsi kuingia kwenye uzalishaji wa mbegu na ipo tayari kufanya majadiliano na makampuni au watu wenye nia ya kuwekeza kwenye uzalishaji wa mbegu ili kuweka utaratibu wa kupunguza gharama za uzalishaji wa mbegu kwa tija.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, swali la nyongeza.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza swali la kwanza nilitaka kujua tu kwa kuwa Mkoa wa Mara ardhi yake ina hali ya hewa nzuri ya zao la Alizeti, na hasa katika tarafa ya Chamriyo Wilaya ya Bunda yenye vijiji 30 na kata saba.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni lini sasa Serikali kwakuwa inataka kupunguza uhaba wa mafuta ya kula hapa Tanzania ni lini itapiga kambi pale kwenye Tarafa ya Chamriyo yenye vijiji 30 na kata saba yenye hali ya hewa nzuri ya kulima Alizeti ili kuwapa mbegu bora za kulima Alizeti na kupunguza uhaba wa mafuta hapa Tanzania?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili kwa kuwa katika swali lako la msingi umezungumza kwamba Maafisa ugani watapewa pikipiki na vitendea kazi vingine Je, kwa Mkoa

wa Mara ambao upo tayari kulima Alizeti ni lini vitendea kazi hivi navyo vitafika kwa maafisa ugani wa maeneo hayo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Bashe majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza maeneo yote ambayo yana-*potential* ya kuzalisha Alizeti au mazao yote ambayo yatatusaidia kupunguza tatizo la mafuta tutayapa kipaumbele kama Serikali, na nimuhidi Mheshimiwa Mbunge kwamba baada ya Bunge tunaweza kukaa mimi na yeye na tukajadiliana namna gani tunaweza kuanzisha mfumo wa *Block farm* katika Wilaya ya Bunda, na kwasababu wenyewe wanazalisha pamba, na pamba ni moja ya zao ambalo tunalipa kipaumbele. Kuhusu vitendea kazi ni kwamba kwanza bahati nzuri Mheshimiwa Mbunge anatoka kwenye ukanda wa Pamba. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia bodi ya pamba sasa hivi tumeanza *program* ya kuwapatia Maafisa Ugani Elimu na vitendea kazi kwenye ukanda wote unaozalisha pamba na Bunda ni moja wa Wilaya na hivi sasa tunavyoongea bodi ya pamba imeanza kukutana na Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wa Wilaya zinazozalisha pamba ili maafisa Ugani waingizwe kwenye *program* ya kupatiwa vitendea kazi lakini vile vile kupatiwa vifaa *soil analysis kit* ambazo watatumia kuwa wanapima afya ya udongo katika maeneo hayo. Kwa hiyo, Wilaya ya Bunda na Mkao wa Mara ni moja ya Mkao ambayo kwetu ni *potential* na tutaipa kipaumbele.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwantumu Zodo.

MHE. MWANTUMU M. ZODO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuwa kati ya vikwazo vyta zao la alizeti ni upatikanaji mdogo kwenye Mbegu ya alizeti wa mafuta. Je, Serikali haioni haja sasa ya kuja na utafiti wa kina wa kuhakikisha tunapata mbegu bora zinazotoa mafuta kwa wingi ili kuchochaea wasindikaji na wakulima wa zao hili la alizeti? (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza utafiti ni jambo *ongoing* tunaendelea kufanya utafiti lakini tumeshafanya utafiti wa kutambua aina gani za mbegu, tunazo mbegu aina mbili tuna *high hybrid* na tuna mbegu za *OPV* ambazo zinatumika kwenye uzalishaji wa alizeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachokifanya sasa hivi kama mlivyosikia kwenye jibu letu la msingi kwamba mwaka ujao wa fedha tutawekeza kiasi cha shilingi bilioni 10 kwa ajili ya kuzalisha mbegu za kutosha na malengo yetu ni kuzalisha *metric tons* 5,000 za Mbegu ambazo zitakwenda shambani ambazo zitatupatia *metric tons* 625,000 za mbegu za kwenda kukamuliwa ambazo zitatupatia *metric tons* 170,000 za mafuta kupunguza *gape* yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo suala la uzalishaji wa mbegu tayari tunashirikiana na sekta binafsi tutazalisha mbegu za kutosha katika mwaka ujao wa fedha na hii itatufanya kwamba tutakuwa tumepunguza 50% ya *gape* yetu, na mwaka unaofuatia nadhani kwamba tutakuwa tumemaliza. Kwasababu mahitaji yetu ni kupata mbegu za kwenda kiwandani kukamuliwa *metric tons* 1,226,000 ambazo zitatupatia wastani wa tani 400,000 za mafuta ili tuweze kupunguza kabisa tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, na sisi tunaamini kwamba kutoka upande wa Serikali ni kwamba ndani ya miaka miwili au miaka miwili ya fedha tutakuwa tumelipunguza tatizo hili la mafuta kwa kiwango kikubwa na *priority* ni zao la Alizeti yakifuatiwa na mazao mengine, kwa hiyo, utafiti umeshafanyika na mwakani tunaanza uzalishaji. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Halima James Mdee, swalil la nyongeza.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto wanazokabiliana Maafisa Ugani mbali na

kwamba hawana vifaa, mbali na kwamba wapo wachache lakini wengi hawana ujuzi wa kukabiliana na mazingira ya kisasa. Na tafiti mbalimbali za Serikali zimeonesha kwamba asilimia zaidi ya 90 ya Maafisa Ugani wanatumia zile skills ambazo walikuwa wamepewa shulenii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nilitaka Mheshimiwa Naibu Waziri aniambie ni lini basi Serikali itakuwa na mkakati madhubuti wa mafunzo ya maafisa Ugani wetu ili waendane na mazingira ya sasa ya ushindani wa Kilimo? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kwa muda mrefu maafisa ugani wetu kuna *gapekati* ya *technology advancement* na elimu wallyonayo. Kwa hiyo, kama Wizara hatua ya kwanza tuliyochukua na mtaiona katika Mpango wetu wa bajeti mwaka huu ni pamoja na kuwapatia vitendea kazi, tutawapatia *soil kit* kila Afisa ugani ambaye anafanya kazi katika eneo lake, tutampatia pikipiki lakini *training* ambayo tutaifanya, tutafanya *training* ya darasani kwa ajili ya kuwa-equip na *technology* na *knowledge* za sasa hivi kutokana na mazao na *ecology* ya eneo ambalo anafanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile kila afisa ugani atakuwa na shamba darasa yeye mweyewe ambalo yeye Afisa Ugani atalisimamia lile Ushamba katika eneo lake kutokana na zao linalozalishwa pale ili liwe ni sehemu ya kufundisha wakulima na gharama za uwekezaji zitatolewa na Serikali katika eneo hilo kwa kumwezesha mbegu, kumwezesha madawa na kumwezesha... ili kuwe kuna-*practical experience* ambayo wakulima wanaiona na yeye mwenyewe anai-practice kwa hiyo, *training* ni sehemu ya muhimu na tumeanza *repair* ya chuo chetu cha Bihawana hapa sasa hivi ambacho kitatumika kwa ajili ya kuwfundisha Maafisa Ugani *continues* kutokana na mahitaji ya soko na dunia.

NAIBU SPIKA: Nataka kuamini Mheshimiwa Almas Maige, Mheshimiwa Almas Maige tafadhali utusaidie wataalam wa kiswahili waje wafanye mafunzo kwa Waheshimiwa Wabunge hapa. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi. Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi Mbunge wa viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 221

Ujenzi wa Barabara ya Lumecha - Londo

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI aliuliza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya Lumecha – Londo – Kilosa kwa Mpepo, inayounganisha mkoa wa Ruvuma na Morogoro kwa kiwango cha lami?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Eng. Godfrey Kasekenya Msongwe majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Lumecha, Londo, Kilosa kwa Mpepo ni sehemu ya barabara Kuu ya Mikumi, Kidatu, Ifakara, Lupiro, Malinyi Kilosa kwa Mpepo, Londo hadi Lumecha yenye jumla ya kilometra 512 ambayo inaunganisha Mikoa ya Ruvuma na Morogoro. Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hii ulikamilika mwaka 2018 ikiwa ni lengo la Serikali kujenga barabara yote kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi sasa ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Mikumi hadi Kidatu kilometra 35.2 na ujenzi wa Daraja la Magufuli lenye urefu wa mita 384 pamoja na barabara unganishi yenye urefu wa kilometra 9.142 umekamilika. Aidha, ujenzi wa sehemu ya Kidatu – Ifakara ambayo ina urefu wa kilometra 66.9 unaendelea na umefikia asilimia 22.6.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa barabara hii kuanzia Lupilo, Malinyi Kilosa kwa Mpepo, Londo hadi Lumecha, Serikali inaendelea kutafuta fedha za kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami ikiwemo sehemu ya Lumecha, Londo hadi Kilosa kwa Mpepo. Aidha, wakati juhudzi za kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami zikiendelea, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania yaani *TANROADS* Mkoa wa Ruvuma na Morogoro itaendelea kuifanya matengenezo mbalimbali barabara hii kutoka Ifakara, Lupiro, Malinyi, Kilosa kwa Mpepo, Londo hadi Lumecha kila mwaka ili iweze kupitika majira yote ya mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha huu wa 2020/2021, barabara hii imetengewa jumla ya shilingi milioni 3,610.54 kwa ajili ya matengenezo mbalimbali. Kati ya fedha hizo shilingi milioni 985.585 ni kwa ajili ya sehemu ya barabara ya Lumecha, Londo ambayo iko Mkoa wa Ruvuma, ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi swalii la nyongeza.

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swalii la nyongeza. Kwa kuwa Serikali iliona umuhimu wa kujenga barabara hii na barabara hii ni ya kimkakati dhidi ya masuala ya kiuchumi ambayo inakwenda kujengwa kwa ajili ya kuinua uchumi wa Kikanda, Kimkoo na Kitaifa, na barabara hii ilishafanyiwa upembuzi wa kina na upembuzi huo ulishakamilika toka mwaka 2018. Je, ni lini Serikali itatoa fedha kupeleka huko kwa ajili ya kuana ujenzi huo haraka iwezekanavyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili ucheleweshaji wa ujenzi wa barabara hii ya kimkakati ambao unachukua muda mrefu sana kuanza kujengwa je, Serikali haionti kwamba kutokuanza kujenga barabara hii kwa haraka inaendelea kusababisha udumavu wa ukuaji wa uchumi katika Mkao wa Ruvuma?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mheshimiwa Eng. Msongwe majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ina urefu wa kilometra 521 kwa hiyo ni uwekezaji mkubwa na tayari tulishaanza jitihada za kujenga hii barabara kwa kiwango cha lami kwa hatua za awali ikiwa ni pamoja na hizo hatua ambazo tayari zimeshafanyika usanifu wa kina lakini nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Msongozi kwamba tayari tumeshaanza ujenzi wa kiwango cha lami katika vipande kadhaa ambavyo nimevitaja ikiwa ni pamoja na ujenzi wa kiwango cha lami kilometra 66.9 kuanzia Kidatu kwenda Ifakara, na bado tumehakikisha kwamba barabara hii itakwenda kutengenezwa kadri fedha zitakapokamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba nia ya Serikali ni kuikamilisha barabara hii ili kuifungua Ruvuma na kanda yote ya kusini ambayo inatumia barabara hii. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kadri fedha zitakapoendelea kupatikana barabara hii tutahakikisha tunaiunganisha kwa Mikoa ya Ruvuma na Morogoro kuititia kwenye hiyo barabara ambayo amesema ambayo inapita kwenye mbuga za Selous na ni miinuko mikali kwa hiyo, uwekezaji ni mkubwa lakini Serikali inatafuta fedha na tunahakikisha tutajengwa, ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Michael Mwita Kembaki, swali la nyongeza.

MHE. MICHAEL M. KEMBAKI: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii kuiliza swali, swali langu ni

kwamba mwezi mmoja uliopita daraja lilikatika katika mji wetu wa Tarime na likasababisha vifo vya watu watatu na wengine watatu mpaka sasa hivi hawapatikani na inadhaniwa kwamba walikwenda na maji, na hata sasa hivi ninavyozungumza kuna daraja limekatika kipande kimoja daraja ambalo linatoka mjini kuelekeza Kibaga ambako wanachimba madini na kuna magari makubwa yanabeба makinikia yanapita pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu ni kwamba je, ni lini watarekebisha hili daraja ili lisije likaleta maafa mengine kama ilivyosababishwa na kuvunjika kwa daraja, ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mheshimiwa Eng. Msongwe majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wengine kwamba Serikali inatambua kwamba mwaka huu kumekuwa na uharibifu mkubwa sana wa barabara nyingi na hasa hizi za changarawe na udongo. Na sisi kama Wizara tulishalitambua hilo tuna maandalizi ambayo tulishayafanya ikiwa ni pamoja na kununua madaraja ya dharula lakini imekuwa ni vigumu sasa hivi kutengeneza hizo barabara kwasababu nyingi sio tu zinahitaji kuweka madaraja lakini pia zinahitaji kuweka matuta ambayo yanainuliwa sasa inakuwa ni ngumu kufanya kazi hiyo katika kipindi hiki ambacho mvua inaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wengine kwamba barabara zote inaanishwa zile ambazo zimepata changamoto hasa kutokana na mvua na mara hali ya hewa itakapokuwa vizuri wakandarasi wapo tayari watazirejesha barabara hizi zote katika hali yake ya kawaida ili ziendelee kutumika ikiwa ni pamoja na barabara ya Mheshimiwa Michael Kembaki Mbunge wa Tarime.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Hawa Mchafu, swali la nyongeza.

MHE. HAWA M. CHAKOMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kuniona hali ya barabara ya Lumecha kilosa inafanana kabisa na ile ya Bungwi Nyamisati je, ni lini sasa Serikali itajenga barabara hii kwa kiwango cha lami ikizingatiwa ni muhimu kwa wananchi wa Mafia, Mkuranga na Kibiti yenyewe? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mheshimiwa Eng. Msongwe majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri barabara ya Bungwi Nyamisati nimefika na tukiwa tumeongozana na Mheshimiwa Mbunge Mpembwenwe naomba nimhakikishe Mheshimiwa Mbunge kwamba hii ni barabara ambayo ni ahadi ya viongozi wa Kitaifa lakini pia ipo kwenye llani ambayo inaunganisha wananchi wa Mafia na wanaokuja bara, kwa hiyo ipo kwenye mpango, fedha itakapopatikana barabara hii itajengwa ili kuifanya wananchi waweze kupata huduma bora ya barabara, ahsante. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Qwaray swali la nyongeza. Mheshimiwa Qwaray nyuma ya Mheshimiwa Mwijage ama jina lako ni tofauti na hilo.

MHE. DANIEL A. TLEMAI: Mheshimiwa Naibu Spika, Naitwa Daniel Awack.

NAIBU SPIKA: Haya Mheshimiwa Awack.

MHE. DANIEL A. TLEMAI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Serikali iliahidi babarara ya Njiapanda Mang'ola, Mataala Mwausi Lalago, kwa kiwango cha lami kwenye llani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi sasa ni lini bararara hiyo itajengwa kwa kiwango cha Lami? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Naibu Spika, tunategemea kuitisha ama kuleta bajeti yetu ili iweze kujadiliwa naomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira ili kipindi cha bajeti tutaitolea maelezo sahihi kuhusu hiyo barabara ambayo ameisema na nimhakikishie tu kama nilivyosema kwenye majibu mengine ya msingi na wananchi wa Jimbo lake kwamba barabara ambazo zote zimeahidiwa na kuwa kwenye llani zipo kwenye mpango wa Kipindi cha Miaka Mitano na tutazijenga kadri ya fedha zitakapoendelea kupatikana. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Cecilia Paresso, swali la nyongeza.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa barabara ya Loliondo – Wasu - Mto wa Mbu ni ahadi ya muda mrefu kwamba barabara hiyo itajengwa kwa kiwango cha lami. Natambua kuna kipande cha Wasu - Sale kilometra 49 sasa hivi kinaendelea kujengwa kwa kiwango cha lami ila kuna eneo korofsi sana la Sale – Ngaraesero, je, ni lini barabara hiyo itajengwa kwa kiwango cha lami?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu kwa swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Cecilia Paresso, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuitia Bunge lako nimuagize Meneja wa *TANROADS* Mkoa aweze kwenda

kwenye barabara hii ya Sale - Ngaraesero ili aweze kufanya tathmini na aone kama tunaweza tukajenga kipande; imekuwa ni kawaida sehemu ambayo tunaona ni korofii yenyе vilima ama yenyе miteremko mikali ama yenyе utelezi aende akafanye tathmini na kuleta bajeti ili tuone namna ambavyo tunaweza tukafanya ili tusikwamishe wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa awe na amani na ikiwezekana baada ya kikao hiki tuweze kukutana ili aweze kunipa taarifa kamili ya eneo hilo ili tuweze kulifanyia kazi. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, Mbunge wa Mikumi sasa aulize swali lake.

Na. 222

**Usalama wa Wananchi Wanaoishi kwenye Vijiji
Vinavyopakana na Hifadhi**

MHE. DENNIS L. LONDO aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha wananchi wanaoishi kwenye vijiji vinavyopakana na hifadhi pamoja na mali zao wanakuwa salama kwani wanyamapori wamekuwa wakiingia na kufanya uharibifu kwenye vijiji?

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mary Masanja, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, Mbunge wa Mikumi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba kutoa pole kwa Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa

Mikumi kwa kadhia hiyo ya kupambana na changamoto ya wanyamapori wakali na waharibifu katika maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji vinavyozunguka hifadhi za wanyamapori nchini vinakabiliwa na changamoto ya wanyamapori wakali na waharibifu kama vile tembo, simba, fisi, nyati, viboko na mamba. Pamoja na mambo mengine, hali hii hii inasababishwa na kuvamiwa kwa maeneo ya kinga (*buffer zone*) na mapito ya wanyamapori.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kupambana na wanyamapori wakali na waharibifu, Serikali imeunda kikosi maalum ambacho kimekuwa kikishirikiana na wadau mbalimbali kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu katika maeneo yanayozunguka hifadhi kwa kadri taarifa za matukio zinavyopatikana.

Aidha, Serikali imeandaa mpango mkakati wa kitaifa wa kushughulikia wanyamapori wakali na waharibifu unaotoa mwongozo wa namna nzuri ya kuwawezesha wananchi kutumia maeneo yao bila kuathiriwa na uwepo wa wanyamapori.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikakati hiyo ni pamoja na kutoa mafunzo kwa wananchi wanaoishi maeneo ya pembezoni mwa hifadhi kuhusu mbinu bora za kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu. Mafunzo haya ni endelevu na yatafanyika katika maeneo yote yenye changamoto hapa nchini. Pili, kuimarisha vikosi vya doria za kudhibiti wanyamapori vikiwemo vitendea kazi ili viweze kufanya doria ipasavyo. Tatu, kushirikiana na Halmashauri za wilaya na vijiji, ili kuwawezesha uandaaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe rai kwa wananchi wa Mikumi na maeneo mengine yanayozunguka hifadhi waendelee kutoa ushirikiano na kuendelea kufuata maelekezo ya wataalam wa wanyamapori kwa kutekeleza mbinu mbalimbali za kukabiliana na wanyamapori hao ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, swali la nyongeza.

MHE. DENNIS L. LONDO: Mheshimiwa Naibu Spika, dhumuni la eneo kinga (*buffer zone*) siyo kuzuia wanyama kuingia vijiji. Ni kwa jinsi gani Serikali imejipanga kuangalia usalama wa wananchi kwa sababu tembo hawa wanaingia katikati ya vijiji kule Kilangali, Tindiga, Malolo hata Yogo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ikumbukwe tarehe 15 Januari 2019 Mheshimiwa Rais alitoa maelekezo kwa Wizara saba kukaa chini na kuititia upya mipaka na kuangalia usalama wa watu katika vijiji vinavyopakana na hifadhi. Hata hivyo, mpaka sasa hatujasikia ni vijiji gani vimeshughulikiwa zaidi ya kuona wananchi wakinyanyasika na pia hakuna alama za kudumu ambazo zimebekwa kwenye eneo la kinga (*buffer zone*) katika vijiji vinavyopakana na mpaka.

Ni lini Serikali inaenda kuweka alama lakini pia inaenda kuanzisha *game ranger post* pamoja na kuanzisha vikundi vyta kuzuia wanyama waharibifu katika vijiji vyetu? Nashukuru.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mary Masanja, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dennis Londo, Mbunge wa Mikumi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpe pongezi Mheshimiwa Mbunge Dennis Londo kwa kuendelea kutoa rai kwa Serikali jinsi ambavyo wanyamapori hasa waharibifu na wakali wanavyoendelea kuathiri wananchi. Hata hivyo, kama nilivyojibu kwenye swali la msingi ni kwamba sasa Serikali imejipanga kuandaa mkakati ambaa utawawezesha hawa wananchi kutambua ni namna gani ya kukabiliana na wanyamapori hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri tumeshaanza kutoa mafunzo katika Mikoa ya Simiyu, tumeshafanya katika Wilaya ya Busega, Wilaya ya Bariadi na maeneo mengine ambayo yanazunguka mkoa huo, lakini pia awamu inayofuata tutaenda katika Mkoa wa Ruvuma, Morogoro na maeneo mengine hapa nchini. Lengo kuu ni kuhakikisha hawa wanyamapori ambao wamekuwa changamoto kwa Tanzania na kwa nchi kwa ujumla wanadhibitiwa kwa kushirikiana na wananchi ambao wanazunguka maeneo ya hifadhi.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, swali la nyongeza.

MHE. ANNE K. MALECELÀ: Mheshimiwa Naibu Spika, huu uharibifu unaoletwa na wanyamapori ni mkubwa sana kwa nchi nzima na vifo vinatokea karibu kila siku tunaongea humu ndani. Hivi Serikali haionti inastahili kufanya zaidi ya inavyofanya sasa ili kuokoa maisha ya wananchi wetu? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

NAIBU WIZARA WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Serikali inatambua changamoto hii na wananchi kweli wamekuwa wakiathirika vikiwemo vifo ambavyo vinatokea. Hata hivyo, naendelea kusema kwamba changamoto ya wanyamapori wakali imekuwa kubwa na sababu kuu ni kwamba tumevamia maeneo ambayo ni mapito ya wanyama wakali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Serikali kuona haya yote, kwa sasa hivi tumejipanga kuandaa hivi vikosi kazi vya maaskari na tutagawa orodha ya watumishi wote ambao wanazunguka maeneo ya hifadhi kuhakikisha kwamba inapotokea athari yoyote au kuonekana kwa

mnyama mkali yoyote basi taarifa itolewe kwa haraka ili tuweze kudhibiti hawa wanyama wakali. Kingine ni kuhakikisha kwamba tutakapokuwa tumewafundisha hawa wananchi kujua namna ya kujikinga na hawa wanyama wakali, basi tutakuwa tumeshirikiana kwa pamoja kuhakikisha kwamba maeneo yenye hifadhi yanahifadhiwa vizuri lakini na wananchi wanaendelea kujikinga na hawa wanyama wakali.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwape pole sana wananchi wote ambao wamekuwa wakikutana na hii kadha na hata Serikali siyo kwamba inapenda kuona wananchi wake wanaendelea kupata shida ya namna hii. Tunajipanga ili kuhakikisha kwamba kadha inapungua ama kutoweka kabisa kwa sababu hata sisi imekuwa ni changamoto kubwa lakini tunajipanga kwa ajili ya kuhakikisha wananchi wanaishi kwa amani.

NAIBU SPIKA: Tumalizie na swali la Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 223

Mipaka Sahihi ya Bonde la Kilombero

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA aliuliza:-

Je, ni upi mpaka sahihi wa Bonde la Kilombero kati ya mpaka uliowekwa mwaka 2012 na ule uliowekwa mwaka 2017?

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mary Masanja, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Pori Tengefu la Kilombero (*Kilombero Game Controlled Area*) lilianzishwa kuitia Tangazo la Serikali (GN) Na. 107 chini ya Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori na Mimea (*Fauna and Flora Ordinance*) ya Mwaka 1951 iliyoanza kutumika mwaka 1952. Baada ya kurejea mwaka 1974, Pori Tengefu la Kilombero lilitambulika kwa GN. Na. 269 ya mwaka 1974 iliyonihwa kwa GN. Na. 459 ya Mwaka 1997 chini ya Sheria ya Wanyamapori Na. 12 ya mwaka 1974 lilikuwa na ukubwa wa kilomita za mraba 6,500. Pori hilo ni sehemu ya ardhiyevu ya Bonde la Kilombero lenye ukubwa wa kilometra za mraba 7,950. Aidha, bonde hilo linachangia takriban asilimia 62.5 ya maji yote ya Mradi wa Bwawa la Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere.

Mheshimiwa Naibu Spika, Pori Tengefu Kilombero halijawahi kubadilishwa mipaka yake. Hata hivyo, mwaka 2012 na 2017 iliwekwa alama kwa ajili ya kuokoa klini cha Mto Kilombero. Aidha, Serikali iliunda Kamati ya Mawaziri Nane (8) kwa ajili ya kushughulikia migogoro ya ardhi ya maeneo yaliyohifadhiwa na watumiaji wengine wa ardhi likiwemo Bonde hilo la Mto Kilombero. Kamati hii ilitoa mapendekezo ambayo yalijadiliwa kwenye Baraza la Mawaziri na maamuzi yake yamekwishafanyika na utekelezaji wake utatolewa hivi karibuni.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, swali la nyongeza.

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Licha ya majibu mazuri ya Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi hawa wanaelewa lakini suala hili limechukua muda mrefu, walikuwa wanatumia maeneo haya kulima na wanajua faida ya Bwawa la Mwalimu Nyerere lakini wanachohitaji ni kupata uelewa na kufahamishwa. Kwa kuwa Mawaziri wameshapitisha na suluhisho limeishafikiwa, je, ni lini Mheshimiwa Waziri atakwenda kuongea na wananchi hawa kusudi waweze kupata suluhisho? (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, tatizo hili lipo pia katika Kitongoji cha Dutumi, Kata ya Bwakila Chini, Wilaya ya Morogoro Vijiji ambapo kuna tatizo la Hifadhi ya Selous pamoja na wananchi wa Dutumi hasa wakiwemo wakulima na wafugaji kiasi kwamba kuna kijana mmoja alitobolewa macho, mwingine amejeruhiwa mkono, ni lini Mheshimiwa Waziri atakwenda kuwasikiliza kwa sababu vikao vimekaa lakini hakuna suluhisho? Ahsante

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, maswali yote anauliza ni lini utaenda huko kuwasikiliza.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuahidi tu Mheshimiwa Mbunge kwamba kabla ya bajeti hii kuisha Juni tutaongozana naye kwenda Kilombero lakini pia Morogoro Vijiji ili kutatua mgogoro huu wa wakulima na wafugaji.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Hussein Amar, swali la nyongeza.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hawa wanyamapor i wamekuwa wakivamia vijiji na kushambulia wananchi hususan Wilaya ya Nyang'wale zaidi ya wananchi 10 wameliwa na fisi. Je, Serikali ina mpango gani wa kwenda kuwatemebelea na kuwapa pole lakini pia kuwalipa kifuta machozi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, lini mtaenda kulipa kifuta machozi?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hussein Amar, Mbunge wa Nyang'wale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kumpa pole sana Mbunge wa Nyang'wale na Wabunge wengine wote ambao wamekumbana na athari hii. Nimhakikishie kwamba hawa fisi ambao wako kwenye maeneo ya Nyang'wale na maeneo mengine yote yanayoathiriwa na wanyama hawa tutaenda kuwahamisha na tutawarudisha hifadhini, kwa sababu Nyang'wale ni eneo ambalo kidogo hifadhi ziko mbali na makazi ya wananchi lakini fisi wanaendelea kwenda kwenye maeneo hayo. Pia tutaongozana naye kwenda kuwaona wananchi hao na tutashirikiana kadri itakavyowezekana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Jerry Slaa, swali la nyongeza.

MHE. JERRY W. SILAA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa masuala haya ya mipaka baina ya makazi ya watu na maliasili yamekuwa ni ya kudumu lakini nchi hii inaongozwa na sheria, Sheria Sura 324 inampa Mkurugenzi wa Upimaji na Ramani mamlaka ya kuhakiki mipaka pale panapotokea mgogoro. Kule kwenye Jimbo la Ukonga upo mgogoro mkubwa baina ya Msitu wa Kazimzumbwi na wananchi wa Kata za Buyuni, Chanika na Zingiziwa. Tayari uhakiki ulifanyika tarehe 24 Februari, 2012 na magazeti yote yalitoa tangazo na lipo linafahamika.

Je, ni lini Waziri atakuwa tayari tuambatane na wataalam wa Wizara ya Ardhi kwenda kuhakiki mpaka huu na kuwaondolea kero ya kupigwa, kubakwa na kuchukuliwa hatua kinyume na sheria wananchi Jimbo la Ukonga?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, ni lini utaenda huko?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jerry Silaa, Mbunge wa Ukonga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mbunge Jerry Silaa kwa kuendelea kuwaonyesha wananchi wake kwamba wamemtuma kwa kazi maalum hapa Bungeni. Nimuhidi tu Mheshimiwa Mbunge kwamba baada ya bajeti hii tutaongozana naye kwenda kutatua mgogoro huu. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Olelekaita, swali la nyongeza.

MHE. EDWARD O. KISAU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vijiji vyangu vya Ndaleta, Ngabolo, Olkoponi, Pori kwa Pori, Mbeli, Amei, Namelok wanasumbuliwa sana na tembo na hivi tunavyozungumza tembo wako mashambani. Nini kauli ya Serikali kwa wananchi hawa?

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii Mheshimiwa Mary Masanja, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Olelekaita, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kutoa pole kwa wananchi wanaozunguka maeneo hayo, lakini Serikali kama ambavyo nilisema mwanzo kwamba tumeanza kutoa mafunzo baada ya kuona athari hii inaendelea kuongezeka. Mafunzo haya yatatolewa nchi nzima namna ya kukabiliana na hawa wanyama wakali. Pia tutatoa vifaa maalum kwa ajili ya kudhibiti hawa wanyama wakali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuombe tu Mheshimiwa Mbunge tuendelee kushirikiana pale ambapo inatoka

watupe taarifa na vikosi kazi ambavyo tumevisambaza nchi nzima vitaendelea kufanya kazi kudhibiti hawa wanyama wakali.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umekwenda sana lakini niseme wazi hii changamoto ya mipaka ni kubwa sana na kuna wakati Serikali iliunda jopo kubwa kabisa la Mawaziri kwenda kuzunguka huko kwenye mipaka kutatua hizi changamoto lakini inavyoonekana tatizo bado lipo, ni muhimu sana kulifanyia kazi.

Wiki iliyopita alisimama Mbunge hapa wa Mbarali kule nako kuna kitu kinaitwa GN. Na. 28 yaani hiyo namba mpaka mtoto mdogo anazaliwa anajua GN. Na. 28 kwa athari wanazozipata wananchi kule na zimeendelea pamoja na hiyo timu ya Mawaziri kama nane hivi kwenda kule.

Sasa sijui shida ni ipi, kama Serikali ilituma Mawaziri nane kwa pamoja na bado shida iko pale pale nadhani kuna haja ya kilitathmini jambo hili kwa mapana yake maana kila mtu akisimama hapa anaongelea mipaka. Ni vizuri lifanyiwe kazi kwa ujumla wake ili kuwe na mahusiano mazuri kati ya wananchi na hifadhi zetu hizi ambazo tunazihitaji sana ili kutunza mazingira lakini pia kwa ajili ya kuliletea Taifa letu mapato ya kigeni.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa maswali na majibu. Ninayo matangazo hapa ya wageni mbalimbali walioko hapa Bungeni.

Kwanza ni wageni wawili wa Mheshimiwa Jumaa Aweso ambaye ni Waziri wa Maji; hao ni mke wake Ndugu Kauthur Francis na mdogo wake Ndugu Shaban Kassim. Karibuni sana. (*Makofii*)

Mke wa Mheshimiwa Aweso ni yupi hapo? Karibu sana. Ni shemeji yetu huyo jamani na wifi yetu.

MBUNGE FULANI: Sijamwona vizuri.

NAIBU SPIKA: Ah, tumeshamwona. Wewe uliyesema ujamwona vizuri! (*Kicheko/Makofi*)

Pia hawa wameambatana na Kamati ya Siasa ya CCM Wilaya ya Pangani na Waheshimiwa Madiwani Wilaya ya Pangani, wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM Wilaya, Ndugu Rajab Abdulraman Abdallah; na Katibu wa CCM, Ndugu Mohamed Moyo; na Mwenyekiti wa Halmashauri, Akida Buhorera. Karibuni sana wageni wetu kutoka Pangani, kijana wenu anafanya kazi nzuri. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

Vilevile Mheshimiwa Aweso anaye mgeni mwininge ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya *RUWASA* na huyu ni Professa Idrissa Mshoro. Karibu Sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Aweso doh! Ana wageni wengi leo; anao wageni wengine ambaao ni Maafisa Tarafa wanne kutoka Pangani wakiongozwa na Ndugu Zuhura Rashid. Karibuni Sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wangeni wa Mheshimiwa Maryprisca Mahundi; na hawa ni wageni watatu ambaao ni dada zake, Ndugu Doreen Bahati, Ndugu Ruhama Ezekia na Ndugu Mariam Kikasi kutoka Jijini Mbeya. Karibuni Sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji pia anao wageni wengine 14 ambaao ni Viongozi wa CCM kutoka Mkoa wa Mbeya, wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM Mkao, Ndugu Jacob Mwakasole. Karibuni sana sana. Katika hao wallosimama, wapo pia viongozi wa Umoja wa Wanawake kutoka Wilaya zote za Mkao wa Mbeya wakiongozwa na Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake wa Mkao wa Mbeya, Mwalimu Oliva Kibona. Karibuni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge; kwanza ni Wageni nane wa Mheshimiwa Nusrat Hanje, ambaao ni Viongozi wa Chuo Kikuu cha Tumaini kutoka Mkoani Iringa wakiongozwa

na Makamu Mkuu wa Chuo Ndugu Nderelio Urio. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia Wageni watatu wa Mheshimiwa Flatei Massay ambaao ni wapiga kura wake kutoka Mbulu Vijiji Mkoa wa Manyara; na hawa ni Mwenyekiti wa CCM Kata ya Endahagichan, Ndugu Boay Tluway, Ndugu Barnabas Kisyo na Ndugu, Marselia Ami. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao Wageni watano wa Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula kutoka *Jema Africa Limited* Nyamagana Jiji Mwanza wakiongozwa na Meneja Uzalishaji, Ndugu Elphas Odingo. Karibuni sana. (*Makofi*)

Vile vile wapo wageni watano wa Mheshimiwa Mwanakhamis Said ambaao ni watoto wake kutoka Mkao wa Mjini Zanzibar wakiongozwa na Ndugu Ayan Abdallah. Karibu sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, hao ndio wageni tulionao hapa Bungeni kwa asubuhi hii. Kabla hatujaendelea na ratiba yetu, tutazame kanuni ya 49 (2) inazungumza kuhusu namna ya kuuliza swali. Kanuni ya 49(2) inazungumza kuhusu namna ya kuuliza swali. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tuzingatie masharti ya Kanuni hii. Kwa sababu mnayo, sina haja ya kuwasomea, naamini mmeshaandika kwamba mtaisoma. Pia Kanuni 45(9) inazungumza kuhusu idadi ya maswali. Sasa hapa wako ambaao wameshazidisha maswali manne ya nyongeza. Kanuni hii inasema, maswali ya mdomo kwa mukutano mmoja kwa Mbunge mmoja ni manne. Kwa hiyo, yule mwenye maswali manne, akiwa ana kosa kosa nafasi asisikitike, kwa sababu kanuni yetu imeweka ukomo huo. Kwa hiyo, wale waliouliza uliza huku mwanzoni, wengine wameshamaliza kabisa nafasi zao za maswali ya nyongeza. Kwa hiyo, wale ambaao bado nafasi zao zipo, Kanuni yetu inatuongoza vizuri.

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Mheshimiwa Naibu Spika, wengine hatupati nafasi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Anatropia, inabidi nikutaje kipekee. Unasema hupati nafasi ya kuuliza maswali. Ninayo hapa nakala ya Waheshimiwa Wabunge. Inabidi tuwe tunaweka kumbukumbu vizuri, maana wakati mwingine midomo yetu huwa inatuponza.

Mheshimiwa Anatropia Theonest, ninayo maswali hapa; naye anayo maswali mawili ya nyongeza na anasema huwa hatupati. Sasa sijui hapati yeye na nani? Hapa anayo maswali mawili na kuna watu ambao hawana kabisa. Kwa hiyo, ndiyo mpate picha ya Wabunge, wakati mwingine malalamiko yanayotolewa hayana huhalsia.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, tunaendelea na ratiba iliyombele yetu.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo wa Spika.

MBUNGE FULANI: Jambo la Dharura.

MWONGOZO WA SPIKA

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo wa Spika.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Lukuvi.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama kutoa ufanuzi kidogo wa jambo ambalo limekua linajirudiarudia. Wiki mbili zilizopita jambo hili la Kamati la Mawaziri wa wanane, limesemwa, wiki hii tena limesemwa. Bahati nzuri baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliokuwa wameniuliza nikapata nafasi ya kukaa nao nje pamoja na Waziri wa Maliasili na Utalii kufafanua.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ufanuzi ni hivi, pamoja na hilo ambalo umelimalizia wewe la Mbarali, ni kweli kwamba Mheshimiwa Rais aliunda timu ya Mawaziri wanane

tukapita, na tukatoa taarifa kwenye Baraza la Mawaziri, lakini hivi vijiji 975 hatukutunga sisi, ilikuwa shirikishi. Mikoa yote tulikaa nao na wilaya pamoja na mimi mwenyewe kutoa orodha ya maombi ya Waheshimiwa Wabunge, mkaandika wenyewe majedwali ya vijiji vyenye migogoro mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kutokana na jedwali lile na taarifa zilizotoka mkoani ndipo tukapata orodha kwamba kumbe vijiji vyenye miingiliano na matatizo ni vijiji 975. Kwa hiyo, tukapita baadhi ya maeneo tukapata suluhisho. Suluhisho lile na mapendekezo tulishayawasilisha kwenye Baraza la Mawaziri; na Mheshimiwa Waziri Mkuu, huyu hapa alitangaza maamuzi ya Baraza la Mawaziri siku ile ile ya kikao. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, maamuzi yalikuwa, kati ya vijiji 975, vijiji 925 visiondolewe kwa wakati ule, illamuliwa hivyo. Pamoja na kwamba ndani ya vijiji 925 kuna kazi ndogo ndogo za kufanya, lakini kwa wakati ule uwamuzi ulikuwa visiondolewe. Kazi iliyobaki mbele yetu, tuliambiwa tufanyie kazi vijiji 55 vikiwemo na hivyo vya Mbarali. Tukishamaliza kazi ya vijiji hivyo 55, tutarudisha tena kwenye Baraza la Mawaziri na uamuzi wa Serikali utatolewa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kama kuna mambo yoyote yanaendelea Mbarali na nilikwambia juzi, Mheshimiwa Naibu Spika. Hakuna kazi yoyote imeamuliwa kufanywa Mbarali kwa sasa kwa sababu uamuzi wake haujapitishwa.

Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge mtuvumilie, bajeti hii ya mwaka huu ndiyo imeweka mapendekezo ya fedha ya kufanya kazi ya utekelezaji wa maagizo ya Baraza la Mawaziri. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bila shaka kupitia Kamati yetu ya Maliasili na Ardhi tutatoa taarifa baada ya kuitisha hizi bajeti mbili, kazi gani ambayo imeamuliwa kufanywa katika vijiji 925 na maamuzi gani yametolewa na Serikali katika vijiji ambavyo vilikuwa vimebakizwa 55?

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka tu kutoa ufanuzi huo. (*Makofii*)

MBUNGE FULANI: Jambo la dharura.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, amesimama, nimpe nafasi azungumze. (*Makofii*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama kufuatia kero iliyojitokeza siku ya tarehe 8 mwezi huu wa tano, liliowakera sana wanamichezo hasa wapenda mpira mguu nchini baada ya kuahirishwa kwa mchezo wa watani wa jadi, Simba na Yanga uliotakiwa kuchezwa siku hiyo na kusababisha manunguniko, mijadala kwenye mitandao ya Jamii na pla kutojua hatima ya wallolipa viingilio kwenye mchezo ule. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili limevuta hisia za Watanzania hata pia nje ya nchi kwa sababu timu hizi ndizo ambazo zimebeba *image* ya michezo hasa mpira wa miguu Tanzania. Kufuatia kero hii, tayari tumeagiza Wizara ya Habari Michezo, Utamaduni na Sanaa, kuhakikisha kwamba wanatoa taarifa haraka sana kwa Watanzania kwamba mchezo wenyewe utachezwa lini? Pia vile viingilio vya Watanzania waliokuwa wamenunua kuingia wenyewe mchezo ule, hatima yake ni nini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba nitumie nafasi hii kuwasihii Watanzania na hasa wapenzi wa michezo kwenye eneo la mpira wa miguu ambao pia walijandaa kuona, kusikia lakini pia kutolea viingilio kwamba tuipe muda Wizara ije itoe taarifa ikishirikiana na taasisi inayoshughulikia mpira wa miguu ambayo ni *TFF* ili Watanzania wapate kujua hatima ya haya yote niliyoyaeleza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na ratiba iliyopo mbele yetu. Katibu.

NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

**MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA MAJI
KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

(Majadiliano yanaendelea)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano. Ninayo majina mbalimbali hapa ya Waheshimiwa Wabunge ambao wameomba kuchangia. Tutaanza na Mheshimiwa Momamed Monni, atafuatiwa na Mheshimiwa George Mwenisongole na Mheshimiwa Joseph Mhagama, ajiandae.

MHE. MOHAMED L. MONNI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami nichangie kwenye Wizara hii muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu ambazo zimetolewa na Wizara ya Maji zinaonyesha asilimia 72 ya watu waishio vijijini sasa wanapata maji, lakini kwenye wilaya yangu sidhani kama asilimia 42 inafika. Nilikuwa nategemea sana mradi mkubwa wa Bwawa la Farkwa na kwenye mradi huo tayari Serikali iltoa zaidi ya shilingi bilioni 7.8 kuwahamisha watu, lakini cha ajabu zaidi, haukutengewa hata shilingi moja kwenye bajeti hii. Wasiwasi wangu mkubwa ni kwamba sasa wale watu wanaenda kurudi pale na hakuna namna tena ya kuja kuwaondoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mambo mengi, kulikuwa na migogoro mingi sana kwa ajili ya kuhakikisha watu wale wanahama pale. Sasa hili jambo limenishtua sana. Nilitamani wakati Waziri anakuja ku-*wind-up* aniambie kwanini hawakutenga fedha angalau kidogo kwa ajili ya bwawa lile? Ninaamini, ili tuweze kutatua changamoto ya

maji kwenye Makao Makuu ya nchi, ilikuwa ni lazima tuanze haraka sana utekelezaji wa mradi ule kwa sababu mradi ule ni katika miradi ya maji ya kimakakati tulionayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Wizara, Wilaya yangu ya Chemba ni katika Wilaya ambazo ni kame kweli kweli na ndiyo maana tumejaribu kufanya miradi mingi ya maji na miradi mingine inashindikana hasa ile ya kuchimba visima. Nasi tunaamini, namna peke yake ya kutatua changamoto za maji kwenye wilaya ile ni kujenga bwawa hili kwa haraka sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kusema pia, kuna changamoto nyingine ambazo zinashangaza sana. Tuna visima ambavyo vilichimbwa mwaka 2014. Katika visima vile, wakati huo Halmsahauri siyo *RUWASA*; walitangaza tenda kwa ajili ya usambazaji. Mkandarasi akapatikana, lakini mpaka leo hii hawajasaini mkataba wa yale maji wasambaze. Mpaka leo, kuanzia mwaka 2014! Vile vile maji yale yamechimbwa kilometra sita kutoka vijiji vilipo. Kwa hiyo, haina faida yoyote kwa sababu lazima watu waweke punda kwenda kuchota maji kilometra sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami naiomba Wizara ya Maji ikashughulikie visima vile vitatu ambavyo ni Chandama, Mapango na Machiga. Watu wengi ambaao hawajasoma kule kijijini wanashindwa sana kuelewa, inawezekanaje mkachimbe maji, mtangaze tenda, mkandarasi apatikane, halafu msisaini afanye kazi? Wanashindwa kuelewa, nini kinaendelea pale? Naomba Waziri wa Maji atakapokuja ku-*wind-up* hotuba yake ya mwisho, aseme chochote ili watu wa kule watuelewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, nimeona mmenipa visima kadhaa vyaa maji; mmeonyesha kwenye jedwali kwamba tutapata visima 13 kwenye bajeti hii, lakini mmetenga shilingi milioni 180. Ni ukweli usiopingika kwamba kwa namna ambavyo Wilaya ya Chemba ilivyo *dry* milioni 180 haziwezi kuchimba visima 13. Sana sana zitachimba visima vinne. Sasa takwimu hizi ni za kwenda kumgombanisha

Mbunge na watu wake, kwamba tumetajiwa viji ambavyo vinaenda kupata maji, lakini kiuhalisia ni kwamba maji kwa bajeti hii haiwezekani. Namwomba Mheshimiwa Waziri, anapotenga fedha angalie na Wilaya zenyewe na namna gani unaweza kupata maji kwenye mazingira haya? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna changamoto nyingine hii inaitwa ya manunuvi. Tulipata mradi pale Chemba Mjini na tuliambiwa mradi ule una shilingi milioni 250, lakini mpaka leo umeshindwa kutekelezwa. Ukimwuliza Meneja wa RUWASA, tangu mwezi wa 11 anasema watu wa manunuvi hawajaleta vifaa mpaka leo, miezi sita. Nami nikisimama jukwaani nawaambia ndugu zangu tumepeata fedha milioni 250 tunaweka sawa mambo ya maji hapa. Jambo dogo kama hilo, tunatumia miezi sita kununua vifaa vya maji, sijui mabomba, mnatuweka kwenye wakati mgumu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru sana, juzi baada ya Waziri wa TAMISEMI kuja pale, mmetupa shilingi milioni 150. Siku mbili tu kaja, ametoa shilingi milioni 150 kwa ajili ya kuhakikisha maji yanapatikana pale hospitali. Nawashukuru sana, lakini nawaomba msisubiri mpaka Mheshimiwa Waziri aje, tukiwaambia sisi, ndio tumewaambia mahitaji ya watu waliopo kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo pia nilitaka niseme, tuachane na utaratibu kwamba manunuvi lazima yafanyike HQ, kila mtu ukimuuiliza yanafanyika HQ, sisi tuko Dodoma HQ Dar es Salaam tunahitaji vifaa vya milioni 20 tunasubiri mpaka watu wa Dar es Salaam waje wanunue, hii haiwezi kuwa sawa hata kidogo. Nimwombe Waziri abadili utaratibu au aweke utaratibu ambao ni rafiki ili tunapopitisha bajeti vifaa vile vipatikane kwa haraka zaidi.

Mheshimwa Naibu Spika, nataka pia niongelee juu ya uchakavu wa miundombinu ya maji iliyopo katika wilaya yangu. Tuna miradi mizuri kabisa ambayo imekuwepo kwa muda mrefu, changamoto kubwa tuliyonayo sasa maji hayapatikani. Shida ni ndogo tu, wakati mwingine unaona

mradi unahitaji milioni 30 tu, lakini kata nzima inashindwa kupata maji kwa sababu tu eti fedha za kukarabati miundombinu milioni thelathini mpaka uende kuomba Wizarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana nilikuwa nimefanya ziara kwenye Kata moja ya Nahoda, tenki limepasuka, tenki lenyewe kulinunua ni milioni moja, watu zaidi ya vijiji sita zaidi ya miezi mitatu hawapi maji. Nimwombe sana Waziri lazima tuwe na utaratibu rafiki ambao unawezesha pale matatizo yanapotokea, pale changamoto za maji zinapotokea waweze kuzitatuwa kwa urahisi na kwa haraka zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa George Mwenisongole, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Mhagama na Mheshimiwa Issa Mtemvu ajiandae. Waheshimiwa Wabunge mnachangia dakika saba saba.

MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Nianze kwa kuungana na Wabunge wenzangu kuipongeza sana Wizara ya Maji kwa juhudhi kubwa walizozifanya kusambaza maji vijijini. Vilevile napenda niwapongeze RUWASA Mkoa wa Songwe hasa Meneja Injinia Charles Pambe kwa kazi kubwa anayoifanya, ingawa nasikitika kusema kwamba RUWASA, Mkoa wa Songwe hatuna gari, wamekuwa wakifanya kazi kwa kuazimaazima gari. Vilevile nimpongeze meneja wa RUWASA, Wilaya ya Mbozi Bw. Gratius Haule kwa kazi kubwa anayoifanya ndani ya Wilaya ya Mbozi. (*Makofii*)

Mheshiniwa Naibu Spika, pamoja na juhudhi hizi kubwa za Wizara ya Maji kusambaza maji huko vijijini juhudhi hizi zinaweza zikawa bure kama Serikali haitaingilia gharama za kuunganisha maji vijijini. Katika ilani yetu ya Chama Cha Mapinduzi inasema kwamba kufika mwaka 2025 asilimia 85 ya wakazi wetu vijijini lazima wapate maji, lakini kwa gharama hizi ya shilingi laki nne laki tano kuungainishiwa maji, hivi

mwananchi maskini wa kijijini hizi laki nne laki tano anapata wapi? (*Makofi*).

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wakulima mwananchi ataamua ni bora anunue mifuko ya mbolea kuliko kuunganishiwa maji, lakini kama gharama hizi zikishushwa zikawa sawa kama umeme wa REA ambao kuungaishiwa ni Shilingi elfu 27 tunaweza tukafikia sio tena asilimia 85 itakuwa ni asilimia 100. Ushauri wangu Mheshimiwa Waziri ni huu, wananchi waunganishiwe bure halafu wakate gharama za kuunganisha bure wanapokuja kulipia gharama za maji kila mwezi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kufanya hivyo kama wananchi wote wataunganishwa bure maji, halafu wakaja kuwakata mwisho wa mwezi wanapolipa bili yao ya maji, tunaweza kufika sio tena asilimia 100 hata asilimia 150, lakini bila kufanya hivyo hizi juhudhi zote zitakuwa bure kama hatutaweza kushusha gharama za maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine Mheshimiwa Waziri kwa masikitiko makubwa wananchi vijijini wanalazimishwa kununua vifaa vya kuunganisha maji kwenye mamlaka za maji. Sasa nataka niulize hizi mamlaka za maji zina maduka ya kununulia vifaa vya kuunganisha maji? Kama sio udalali! Kwa sababu maduka hayo hayo wananchi ambao wangeenda kununua ndio hayo hayo ambayo hao Maafisa wa Maji ndio wanakwenda kununua hivyo vifaa. Sasa kuna sababu gani ya msingi kulazimisha wananchi kununua vifaa vya kuunganisha maji kwenye mamlaka za maji, kwa nini wasiende kununua kivyao wao wa-deal/tu na gharama za kuunganisha maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ushauri wangu ni huu, kama kweli tuna nia yakutaka kusambaza maji na kuhakikisha maji yanafika kwa kila mwananchi ndani ya nchi yetu ya Tanzania, ni lazima gharama za kuunganisha maji ziwe ndogo. Kwa kufanya hivyo tutaweza kabisa kumaliza tatizo la maji ndani ya nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nikushukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Mhagama atafuatiwa na Mheshimiwa Issa Mtemvu na Mheshimiwa Ester Bulaya ajiandae.

MHE. JOSEPH K. MHAGAMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia. Awali ya yote nampongeza sana Waziri Mheshimiwa Aweso kwa kazi nzuri anayoifanya kwenye Wizara hii. Mheshimiwa Aweso ni mmoja katika Mawaziri ambao wanawafahamu wananchi wa Madaba na anafahamika na wananchi wa Madaba. Ametutembelea na kuangalia changamoto zetu katika Kijiji cha Mtyangimbole, lakini pia amekuja Mdaba Mjini Lituta, ameenda pia Kijiji cha Mtepa, Wino na pia amechangia fedha zake kuwezesha miradi ya maji ya wananchi. Ni mmoja katika Mawaziri wa kupigwa mfano. Kwa niaba ya wananchi wa Madaba namshukuru sana sana Waziri Aweso kwa ushirikiano mzuri anaowapa wananchi wa Madaba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Serikali kwa kupitia Wizara ya Maji kwa kufanikisha miradi ya Madaba Mjini, tumefaulu kwa kiwango kizuri lakini bado hatujamaliza ule mradi kwa asilimia mia moja. Nimwombe Mheshimiwa Aweso kwamba eneo la Mtepa, Lituta na Kipingo maeneo ambayo tayari amekwishatembelea yamepata maji kwa kiwango, lakini kwa sehemu kubwa bado hatujamaliza usambazaji. Tunaomba Waziri aendelee kutupa *support* kwa kupitia timu yake ya mkoa na wilaya ambao kwa sasa wamefanya kazi nzuri sana, tunaomba aendelee kuwatia nguvu wafanikiwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Halmashauri yetu ya Madaba tunao mradi mmoja mkubwa sana wa vijiji nane na Mheshimiwa Waziri anavifahamu. Vijiji hivyo nane, ni Rutukira, Ndelenyuma, Bangamawe, Ngadinda, Ngumbiro, Mtyangimbole, Ruhimba na Likarangiro. Vijiji hivi havikuwa na maji kabisa, tulianza mchakato na Mheshimiwa Waziri kutafuta fedha bilioni sita kwa ajili ya ujenzi wa mradi mkubwa

utakaotoa maji Mgombezi kupeleka kwenye vijiji hivi nane. Hata hivyo ilionekana hizi fedha ni nydingi na haziwezi kupatikana kwa mara moja. Ushauri wa Wizara na wataalam ulikuwa twende kwa vipande vipande.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru Serikali imeshatenga fedha milioni 350 kwa ajili ya Mradi wa Maji Rutukila na Ndelenyuma, lakini tayari imetenga fedha milioni 300 kwa Kijiji cha Mbangamawe kwa ajili ya kuanza kutekeleza mradi, lakini pia Kijiji cha Mahanje milioni 250. Jumla ya fedha iliyotengwa ni bilioni moja na milioni mia moja na tisa (Sh.1,109,000,000) kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa vijiji vinne; kati hivyo vijiji vitatu vinatoka katika vile vijiji nane nilivyokwishavitaja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapompongeza Waziri kwa kukubali kutenga fedha hii na Serikali kufanya hivyo, ninao ushauri wa kuhakikisha namna gani tunatekeleza miradi hii kikamilifu. Uzoeuf unaonyesha mifumo ya utekelezaji ndio iliyoiqwamisha Wizara hii kuwafikishia maji watanzania. Moja kati ya mambo ambayo napendekeza, eneo la kwanza utamaduni umekuwa kuunda kamati za utekelezaji wa miradi hii baada ya miradi kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kamati ziundwe kabla ya mradi haujaanza, kamati zishiriki kwenye utekelezaji wa mradi ili wanapokabidhiwa mradi wajue changamoto za mradi. RUWASA watekeleze miradi yote kwa kushirikiana na Kamati za Maii tanqu *day one* hii itasaidia *sustainability*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa na ushauri wa maeneo mengine matatu, lakini nimesikia kengele imepiga, nataka niongeze umuhimu wa kuhakikisha kwamba mifumo ya kuingiza maji kwenye nyumba, pale Madaba tuna shida, tunawataka wanaotaka kuingiza maji kwenye nyumba waje wanunue mabomba *RUWASA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, inatosha kutoa viwango vya ubora vya mabomba yanayotakiwa, mteja akanunue mwenyewe vifaa vyote, *RUWASA* wakaque wamsaidie mteja.

Mfumo tulioweka sasa Mheshimiwa Waziri wananchi wanaamini kwamba ni mfumo unaowezesha watu kupiga fedha, hatutaki kuwapa wananchi fursa ya kutafsiri vibaya nia njema ya Serikali ya kuwawezesha, tuwaachie wananchi wakanunue vifaa. *RUWASA* wakague vifaa hivi vimefikia viwango viwekwe, sio wananchi wanunue kupitia *RUWASA*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa *RUWASA* kununua vifaa vya miradi kwa kutumia mfumo ambaa ni *centralized* unachelewesha sana utekelezaji wa miradi maeneo ya miradi, waandae utaratibu mpya utakaowawezesha wilaya, halmashauri au *RUWASA* katika ngazi ya wilaya na mkoa kununua vifaa wenyewe moja kwa moja kwa sababu hiyo *centralized system* ni nzuri lakini inachukua miezi sita mpaka saba kupata vifaa tunavyotaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania wanapata maji, Mheshimiwa Aweso amekuwa makini na Naibu wake Waziri, hawajatukatisha tamaa, nasi tunawatia moyo wanaweza, tuhakikishe kwamba Watanzania wanapata maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Issa Mtemvu atafuatiwa na Mheshimiwa Ester Bulaya na Mheshimiwa Anton Peter Mavunde ajiandae.

MHE. ISSA J. MTEMVU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie...

NAIBU SPIKA: Samahani Mheshimiwa Issa Mtemvu kabla hujaanza kuchangia, Wajumbe wa Kamati ya Uongozi, saa tano na nusu Mheshimiwa Spika anawaita kwa ajili ya kikao hapa *lounge*.

Mheshimiwa Issa Mtemvu, endelea.

MHE. ISSA J. MTEMVU: Mheshimiwa Naibu Spika nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie katika Wizara ya Maji, Wizara ambayo ni muhimu sana kwa wananchi wa Jimbo la Kibamba. Nitumie nafasi sana kuwapongeza viongozi wenye dhamana ya Wizara hii ndugu yangu Mheshimiwa Jumaa Aweso, Waziri, lakini pia dada yangu Maryprisca kwa kufanya kazi vizuri pamoja na Katibu Mkuu Dkt. Sanga. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuwa nikisema mara nydingi hapa Dar es Salaam ina mafanikio makubwa sana kwenye suala la maji na taarifa zetu zote Mheshimiwa Waziri Mkuu amewahi kutuambia hapa, Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam kwa mara nydingi sana amekuwa akisema takwimu zaidi ya asilimia 92 Dar es Salaam ina maji. Nawapongeza sana, lakini nimekuwa nikisema hizo asilimia zillizobakia Dar es Salaam ni za Jimbo Kibamba. Kibamba kuna shida kubwa ya maji. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi imeenda mingi sana ipo pale Kibamba imeenda kwa kaka yangu Mheshimiwa Jafo kule, mradi mzuri kabisa zaidi ya asilimia 97 umetoka Luguruni Kibamba. Umeenda kwa kaka yangu Profesa Kitila Alexander Mkumbo, akinamama wametuliwa ndoo kichwani kule Ubungo, lakini wananchi wa Jimbo la Kibamba wanaendelea kuteseka.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi iliyopo pale ambayo inaendelea nishukuru sana upo mradi mkubwa sana unatoka changanyikeni unaenda Bagamoyo lakini lipo tanki kubwa la litu milioni 5.6, liko pale Tegeta A, hili likitengenezwa vizuri, linaenda vizuri, lilikamiliika na usambazaji wa mabomba Kata nzima ya Goba wanaenda kupata maji salama na yenye kutosheleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi tunaoulilia sasa, ambao Hayati alipita mchakato ulikuwa tayari unaendelea, lakini akasema mfanye kwa dharura ni tanki kubwa pale Mshikamano, Kata ya Mbezi, mpaka sasa halijaanza, Mheshimiwa Waziri akija naomba nifahamu vizuri ni lini tanki

hili pale Mshikamano lisaidie wananchi wote wa Makabe, wananchi wa Msakuzi, wananchi wa Mpiji Magoe, wote waweze kupata maji safi, salama na yenye kutosheleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye taarifa ya Mheshimiwa Waziri niliisikiliza, mmoja wa mradi uliotamkwa ni pale Kata ya Kwembe Kinyazi A, unazungumza milioni 33, mradi ule umekamilika mwezi Februari, ni ukweli hakuna kitu kama hicho. Bahati nimemwomba Mheshimiwa Waziri kwenda baada ya bajeti yake kupitishwa na amekubali na barua ipo mezani kwake, tutaenda tutafika pale ataona watu wanaendelea kunywa maji ya chumvi, lakini maji ya njano, maji mabaya kabisa ndani ya Kata ya Kwembe au eneo la Kinyazi A.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme juu ya changamoto kubwa katika Kata ya Kibamba maji yapo changamoto ni usambaji wa mabomba. Ipo miradi midogo midogo zaidi ya kumi na mbili toka mwaka 2020 mwezi Machi, bajeti iliopita tena ya juzi yake ya mwaka 2019/2020 mpaka leo katika mabomba haya maji hayatoki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri aliwahi kufika Wilaya ya Ubungo, upande wa Jimbo la Ubungo, kwa bahati tulikuwa wote. Nafurahi sana kaka yangu Rwejema pale anafanya kazi vema, lakini katika hili wanisaidie kutoa mabomba, yasambazwe kwa wananchi hawa nilliotamka katika kata nydingi ili waweze kupata maji salama na yenye kutosheleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo kama Kibwegere, Kwembe, Msingwa, Malamba Mawili, Ukombozi na Msumi na kule Kibesa mbele ya Mpiji Magoe kwenda Mabwepande, kule kunataka tusambaze mabomba tu il mtu aweze kupata.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua bado dakika moja au na nusu, nimwombe sasa Mheshimiwa Waziri, katutengea bilioni 25, usambaji wa maji katika maeneo ambayo hakuna maji Jijini Dar es Salaam. Naomba hizi hela alizozitenga Waziri, hajasema zinakuja Kibamba ameweka kwa ujumla wake,

asilimia 92 tayari Dar es Salaam, hakuna maji Kibamba, tupeleke Kibamba ili wananchi wapate maji salama na nyenye kutosheleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nikushukuru kwa kunipa nafasi, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri na Wizara ya Maji kwa asilimia zinazotosha kwa sababu wananchi wanaenda kupata maji salama na ya kutosheleza. Ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Ester Buyala, atafuatiwa na Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde atafuatiwa na Mheshimiwa Zuberi kuchauka ajiandae.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia ya Wizara hili muhimu ambayo inatesa sana wanawake kwa kutembea umbali mrefu kutafuta maji na Mheshimiwa Rais amesema hilo jambo la maji ni kitu chake cha moyoni kwa sababu anajua wanawake wa nchi hii wanateseka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kuzungumzia tatizo la upotevu wa maji. Tatizo hili limekuwa sugu tangu nimeingia katika Bunge hili mwaka 2010 tunazungumzia changamoto ya upotevu wa maji kwenye mamlaka zetu. Nitoe mfano kwenye mamlaka 23, mamlaka 21bado zina changamoto ya upotevu wa maji kupita kiasi. Kwa miaka miwili tu kwa mfano mwaka wa fedha wa 2019/2020 kutohana na upotevu wa maji Serikali imepata hasara ya billioni 177. Mwaka 2081/2019 kutohana na tatizo hili la upotevu wa maji Serikali ilipata hasara ya bilioni 155. Sasa kwenye miaka miwili tumepoteza bilioni 332 ambazo Waheshimiwa Wabunge tutafakari, ingetengeneza miradi mingapi katika majimbo yetu, au tungechimba visima vingapi katika majimbo yetu na kumtua mwanamke ndoo kichwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine tunapoyasema haya, tunataka tatizo hili liishe na tunajuaje kuna upotevu wa maji? Ni baada ya kukokotoa maji

yanayozalishwa na yanayomfikia mteja. Tatizo hili sugu kwa nini tunakubali kupoteza pesa za walipa kodi, kwa uzembe, kwa kutokuwa na ufanisi wa kuhakikisha miundombinu ya maji inakuwa salama na kuziba mianya ya watu kujunganishia maji kiholela.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati haya yanaendelea, kwa mujibu wa Kanuni ya 6 ya mwaka 2013 ya Usambazaji Maji, Serikali inapaswa kupeleka ruzuku kwenye mamlaka ambazo zimefuzu, ziko Daraja A, B na C. Kwa mwaka 2019, Serikali imeshindwa kupeleka bilioni 856 katika mamlaka 10. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hizi mamlaka zitawezaje kuijendesha? Zinatakiwa zijiendeshe, zinatakiwa ziendelee na ukarabati wa miundombinu ya maji, na hizi halmashauri, lkiwepo na kwako Mbeya. Sasa haya mambo hatuwezi kuyavumilia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi kweli huku tunashindwa kuminya, huku tunashindwa kuhakikisha tunatengeneza miundombinu mizuri ya maji, huku hatupeleki pesa kwenye mamlaka ziweze kuijendesha na kukarabati hii miundombinu ya maji halafu tunataka kumtua ndoo mwanamke kichwani. Kwa miujiza? Kwa mambo haya?

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na tatizo la kutokukusanya madeni kwenye mamlaka ya maji; bilioni 148 ziko nje! Lakini mbaya zaidi, Serikali inadaiwa bilioni 64 katika mamlaka zake. Lipeni madeni ili hii Wizara iweze kuweka mipango yake mbalimbali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, madeni mengine, bilioni 83 ni kwenye viwanda na wateja wa kawaida. Tuna changamoto nyngi za miundombinu, tuna changamoto za kuhakikisha tunamaliza miradi kwa wakati, lakini bado Wizara hii imekuwa na changamoto kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo linguine Serikali kutolipa wakandarasi kwa wakati na kufanya riba ziongezeke;

kwa mfano kuna ujenzi wa jengo la Wizara ambalo linagharimu billioni 44. Lakini wameacha kulipa kwa wakati, riba imetoka kuanzia milioni 99 mpaka billioni 4.9; *shame!* Hizi pesa mngekuwa mnalipa kwa wakati zingeenda kutengeneza miradi mingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa mtambo wa kusambaza maji Mradi wa Ruvu Chini, ambaao Serikali inadaiwa billioni 17 na Mchima, wameshindwa kulipa riba ni bilioni 3.9. Hivi kama mingelipa kwa wakati hizi pesa zingine zingeenda kukamilisha miradi mingine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano kuna miradi sita Dar es Salaam, Moshi na Arusha imeshindwa kuendelea kwa miaka mitatu mfululizo kwasababu tu Serikali imeshindwa kupeleka bilioni mbili. Na huo mradi mpaka sasa hivi wamelipa billioni 16, mradi una gharama ya billioni 18. Mnalipa riba huku kwa uzembe wa kutokeleka pesa kwa wakati, mnaacha miradi mingine ambayo inatakiwa ikamilike kwa wakati inashindwa kukamilika. Haya mambo ndiyo yanafanya Wizara hii ishindwe kutimiza wajibu wake na kuhakikisha mwanamke anatuliwa ndoo kichwani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge, hebu tuijilize hizi tathmini ambazo tunapewa kwamba upatikanaji maji vijijini *maybe* ni asilimia sabini na. nilikuwa nimepitia ripoti; *EWURA* inasema Mkuranga, Kisarawe, Chalinze, upatikanaji wa maji ni asilimia 96, Iakini *CAG* amekwenda kuchunguza, upatikanaji wa maji ni asilimia 53.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, takwimu tunazopewa na Wizara na changamoto ya kutokeleka miradi na upotevu wa maji, inawezekana kabisa upatikanaji wa maji katika nchi yetu haufiki hata asilimia 50. Kwa hiyo, haya ni mambo ya msingi sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa moja ya miradi iliyokaa muda mrefu ni pamoja na Mradi wa Maji wa Bunda unaotoka Ziwa Victoria. Biashara ya chujio tumeisikia sana, biashara ya usambazaji wa mabomba kwenye kata saba tumezisikia

sana. Sasa tunataka kata 14 za Mji wa Bunda zipate maji; hilo ndilo nimetaka kulisitsitiza. Zibenii mianya ya upotevu maji, pesa zinapotea.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wewe unasema wakikuzingua utawazingua, na sisi Wabunge humu ukitizingua maji hayatoki katika maeneo yetu na sisi tutakuzingua kabla Rais hajakuzingua. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde, atafuatiwa na Mheshimiwa Livingstone Lusinde, Mheshimiwa Daniel Awack ajiandae.

MHE. ANTHONY P. MAVUNDE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naanza kwa pongezi nydingi sana kwa Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri kwa kazi nzuri na kubwa ambayo wanaifanya. Lakini pia nampongeza sana Katibu Mkuu, *Engineer Anthony Sanga*, pamoja na Naibu Katibu Mkuu, mama Nadhifa Sadiki Kemikimba ambao kwa pamoja wanafanya kazi hii vizuri sana ndani ya Wizara ya Maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Jiji la Dodoma ni kati ya majiji ambayo yanaongoza kwa ukuaji wa kasi sana hivi sasa. Hali ambayo inasababisha kuwaleta watu wengi sana Dodoma wakiwemo wawekezaji wakubwa. Kwa hivi sasa lita za ujazo wa maji ambazo zinahitajika kwa Jiji la Dodoma kwa siku ni lita milioni 103, lakini uwezo uliopo hivi sasa ni lita milioni 66 kwa siku. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na mikakati ya Serikali kwenye kutatua changamoto hii. Mikakati hii miwili, wa muda mfupi na muda mrefu, nakubaliana nayo. Isipokuwa, naiomba Serikali katika mkakati huu wa muda mfupi, tuendelee kuongeza nguvu zaidi ili wananchi wengi wapate maji mengi na kwa wakati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa tunayo changamoto hapa ambapo maeneo mengi yanapata maji kwa mgao, na hivyo kuwasababisha wananchi wengi kupata adha. Niwaombe Wizara kuongeza kasi. Najua mmetenga kiasi cha shilingi bilioni 2.4 cha kuyatoa maji kutoka pale lhumwa mpaka Njedengwa ambayo itawagusa wananchi wa Kisasa, Nzuguni na maeneo mengine. Lakini vilevile ninafahamu pia kwamba kuititia mtandao huohuo tutagusa maeneo mengi ya katikati ya Jiji la Dodoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuombe Waziri, na bahati nzuri umetoa ushirikiano mkubwa sana, tumetembea mimi na wewe kwa pamoja tumeangalia maeneo yote hayo. Niombe tuongeze kasi ya uchimbaji wa visima vyta pembeni ili maji mengi zaidi yaongezeke. Najua kule Mzakwe mnafanya, lakini tuongeze kasi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kumshukuru sana Waziri, ameniletea mtaalam pale *DUWASA*, Eng. Aaron; umeniletea mtu sahihi sana, anajitahidi sana, anafanya kazi nzuri sana. Ni mtu ambaye hakai ofisini, ukimwambia tatizo anakwenda *site* moja kwa moja. Mheshimiwa Waziri nikuombe katika hili utusaidie kutatua changamoto hii ya maji katika Jiji la Dodoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye mkakati wa muda mrefu umezungumza kuhusu Ziwa Victoria, nakubaliana nayo, lakini mmetenga kiasi cha fedha cha takribani shilingi bilioni moja. Lakini Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 19 wa hotuba yako umezungumza Farkwa kwa udogo sana, tunaomba ukija ku-*wind up* hapo utuambie mradi wa Farkwa inakuaje kwasababu sisi tunaamini mradi wa Farkwa na wenyewe utasaidia sana kuongeza vyanzo vyta maji na kuondoa changamoto hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, nikushukuru sana kwenye bajeti hii mmetutengea fedha za kutosha za miradi mikubwa ya maji ambayo pia itagusa maeneo mengi ya pembezoni kuazia Mzakwe yenyewe, Mbalawala, Veyula, Mpunguzi mnagusa mpaka Chololo,

maeneo ya Kikombo yote mmeyagusa, tunashukuru sana kwa kuliona hilo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niishukuru Serikali kwa mkopo huu wa euro milioni 71 kutoka Korea kwa ajili ya mfumo wa maji taka kwenye Jiji la Dodoma. Hii ni changamoto kubwa hivi sasa lakini naamini kwa fedha hizi za mkopo kutoka Korea, maana yake tuta-*address* changamoto ya maji taka katika maeneo ya Swawa, Chamwino, *Area C* na Ipagala ambayo hivi sasa yana changamoto kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, naiomba Wizara iangalie upya matumizi ya *force account*. Iko miradi mingi ambayo hivi sasa imekwama kwasababu Wizara inaitegemea *DDCA*. Mheshimiwa Waziri, ni ukweli ulio wazi kwamba *DDCA* haina *capacity* ya kuweza kuisimamia hii miradi yote kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, naomba ukija ku-*wind up* hapa utuambie kwa nini Serikali sasa msione haja ya kuruhusu *contractors* wengine wafanye kazi hizi za maji. Kwasababu *DDCA* tunamsubiri sana. Wananchi wanasubiri maji kwa muda mrefu lakini *DDCA capacity* yake ni ndogo, tunawakwamisha Watanzania kwasababu ya *force account*. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, kuna miradi takribani 2,610 katika bajeti iliyopita ambayo ilipaswa kutekelezwa lakini *capacityya DDCA* ni ndogo, mashine zake ni *outdated*, chache, ukimpa leo kisima kimoja hapo lhumwa anakaa miezi miwilli; hii miradi 2,000 anaifikia lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, naomba ukija ku-*wind up* utuambie namna ambavyo Serikali imejipanga kwenye hili la *force account* kwasababu wananchi wetu wanapata taabu kusubiri *DDCA*, na *DDCA capacity* yake ni ndogo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naelewa sana dhana ya *force account*, lakini kwa miradi ya maji tuiangalie katika jicho

tufauti Mheshimiwa Waziri. Kwenye miradi ya maji tuiangalie kwa jicho tofauti kwa sababu wananchi wengi wanakwama. Fedha zipo, tuna miradi ya *PbR*, tuna *P4R*; yote imekwama kwasababu ya utekelezaji mdogo wa *DDCA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, kwa hiyo, nikuombe sana ili tuwakwamue wananchi wetu wa Tanzania kwa adha hii ya maji. Na hizi fedha za hii miradi ambayo iko chini ya *DFDA* na *World Bank* zipo. Nikuombe utoe tamko hap oleo kuziruhusu sasa hizi mamlaka ambazo zina miradi hii waweze kutoka nje ya mipaka ya *force account* kwa sababu *DDCA* wanatuchelewesha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maneno ambayo nimeyasema hapa nakuamini sana Mheshimiwa Aweso kwa kasi uliyonayo, Waziri kijana, una uwezo wa kuyasimamia haya. Na sisi tunakuumba heri kwa sababu tunajua una nla njema; endelea kuwazingua sana ili maji yatoke. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana; Mheshimiwa Livingstone Lusinde, atafuatiwa na Mheshimiwa Daniel Awack, Mheshimiwa Dunstan Kitandula ajiandae.

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara ya Maji. Na nimshukuru Mungu sana kwa ajili ya zawadi ya uhai pamoja na afya njema aliyonipatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Aweso, pamoja na Naibu Waziri, Mheshimiwa *Eng. Maryprisca Mahundi* na Katibu Mkuu, *Eng. Sanga*, kwa namna ambavyo Rais amewaaamini kuendelea kuhudumu katika Wizara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitazama namna ambavyo Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan amepanga uongozi kwenye Wizara hii utagundua kwamba ana

matarajio makubwa sana ya safu yake hii kumletea ushindi katika mapambano ya kumtua ndoo mama kichwani. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa ajili ya kuwaamini hawa na kwa ajili ya msukumo anaoufanya ili wananchi waweze kupata maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Maji ni Wizara mtambuka, ni Wizara ambayo ikifanya vizuri inaweza kupunguza bajeti ya Wizara ya Afya kwa kiwango kikubwa sana. Kwasababu Wizara ya Afya wakati mwingine magonjwa mengi yaliyopo ni ya mlipuko yanayosababishwa na watu kukosa maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Wizara ya Maji mkijitahidi mkafikia tu malengo yenu, bajeti ya Wizara ya Afya itashuka chini badala ya kuendelea kupanda. Sio jambo zuri sana kuona kila mwaka Wizara ya Afya bajeti inapanda, maana yake ni kwamba matatizo ni mengi kuliko mafanikio.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi mingi ya Wizara ya Maji ni ya zamani, ni chakavu. Kwa hiyo, tunahitaji nguvu kubwa sana kuweza kuifufua hii miradi na kutengeneza mipya. Mheshimiwa Aweso, wakati mwingine nasema wazi; nchi yetu tusijjenge yote kwa mara moja. Kuna majimbo hayana barabara wala zahanati na maji hakuna, sasa tuwe tunaangalia basi, tufanye sensa ya kutosha tuone hivi maji yako mengi upande gani na upande gani unahitaji, unaweza kuona namna nzuri kabisa ya ku-solve tatizo la maji vijijini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Aweso, sisi Wabunge wa vijijini tuna matatizo makubwa sana ya maji. Visima vyetu vimekuwa visima chakavu, lakini nenda uangalie, hata ongezeko la watu limeongezeka. Chukulia Jimbo la Mvumi; tuna Tarafa tatu za Makang'wa, Mvumi na Mkwayungu. Hizi tarafa zimekuwa miji mikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashauri tu hata kama tutakwenda kila mwaka, mwaka mmoja Tarafa ya Mvumi tujenge tanki kubwa la lita laki mbili, mwaka unafuata Tarafa

ya Makang'wa tujenge tanki kubwa la lita laki mbili, mwaka unaofuata tumalizie Mkwayungu tanki kubwa la lita laki mbili. Tutakuwa tayari tumeondoa matatizo makubwa sana ya namna ya kupata maji. Kwasababu matanki yetu ni ya zamani mno, yana lita 40,000, lita 50,000; hazitoshelezi kutokana na ongezeko kubwa la watu katika maeneo haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambali ninataka kuishauri Wizara; hivi vile visima kumi vifuatilieni; vimefikia wapi? Maana mwanzoni tulikuwa na visima kumi, pesa zikatolewa visima vimechimbwa baadhi ya maeneo maji yakapatikana, vimefukiwa.

Kwa hiyo, wananchi wanaambiwa tu kuna kisima pale lakini maji hakuna. Twende tuwaondolee matatizo kwa sababu kama visima vimechimbwa kusambaza maji kuna gharama gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna baadhi ya maeneo yana maji machungu, yana maji ya chumvi nyngi. Chukua maeneo kama Mlodaa, pale kila tukichimba kisima lazima tukute maji makali sana; Manzase; hivi kama tumeweza kutoa maji Ziwa Victoria tunashindwa nini kuchukua maji Mlowa barabarani kuyapeleka Mlodaa ambapo ni kilometra saba tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, na Mlowa barabarani ina maji mengi, tumechimba Ng'wenda tumekosa maji, tumekwenda hadi mita 150 tumekosa maji, tunashindwa nini kuchukua maji Lowa barabarani au Mlowa bwawani kuyapeleka Ng'wenda, mahali ambapo ni karibu? Tunashindwaje kuchimba maji katika Kata ya Nini kupeleka Ng'wenda; tunashindwaje kutoa maji katika Kata ya Mlowa kuyapeleka Manzase na barabara ni ileile moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, siyo lazima watu wanywe maji ya palepale, maji yatoke sehemu nyngine, yaende yahudumie wananchi sehemu nyngine ili wananchi wetu waweze kupata huduma bora ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuna sababu kama sehemu hiyo tuna-*drill*tunakuta maji ya chumvi, tunaendelea kuchimba tena eneo illelile; ni kupoteza *resources*. Tuangalie kijiji gani kiko Jirani kina maji safi na salama tuchimbe halafu tuyapeleke kwa wale wananchi waweze kupata maji safi na salama. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Aweso, kwa hiyo, nakushukuru sana. Najua mmejipanga vizuri na mnafanya kazi vizuri na Wizara yako itakuwa Wizara ya kelele kwa sababu hakuna mbadala wa maji, maji ni ibada, maji ni afya, maji ni kila kitu. Kwa hiyo tutaendelea kukuhimiza lakini lengo letu ni kukushauri na sisi Wabunge tutakuunga mkono kuhakikisha kwamba unafanya kazi vizuri, wale wezi wa maji tunayo kazi ya kuhakikisha nao vilevile wanapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, upotevu wa maji; tuweke utaratibu mzuri wa kutoa taarifa. Hivi bomba linavuja kutwa nzima na Watanzania wanapita eneo hilo; hii si sawa. Kwa hiyo endeleeni kuzitangaza namba zile za kutoa taarifa za uvujifu a maji, lakini vilevile raia wema watoe taarifa kwa wizi wa maji ili wananchi wote waweze kupata huduma hii ambayo wote tunaitarajia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja; ahsante sana kwa kunisikiliza. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Daniel Awack, atafuatiwa na Mheshimiwa Dunstan Kitandula, Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi ajiandae.

MHE. DANIEL A. TLEMAI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mji wa Karatu upatikanaji wa maji ni kwa asilimia 33 ambayo unaunganishwa na bwawa mbili, moja iko kwenye eneo la Patom na nytingine iko kwenye eneo la Bwawani. Na eneo hili la Bwawani limejaa maji na *borehole* lile haifanyi kazi, na

Mheshimiwa Naibu Waziri alituenzi kutembelea Jimbo la Karatu na ukiangalia Mji wa Karatu ni wa kitalii na upatikanaji wa maji ni asilimia 33. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hili la Bwawani waliomba shilingi milioni 440 kwa mwaka jana na mwaka huu lakini kilichopatikana ni milioni 175 katika eneo hili la Bwawani katika Mji wa Karatu. Kuna eneo lakini Ayalabe, Kata ya Ganako, waliweza kuomba 599,131,000 lakini kilichopatikana ni 168,000,000, hizi zingine bado hazijapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti hii ya mwaka huu kwa Wilaya ya Karatu Wizara imetenga shilingi bilioni mbili na milioni sabini na saba. Sasa hofu yangu ni kwamba kama mwaka jana tuliweza kuomba milioni 599 ikapatikana milioni milioni 168 na wakati huo katika eneo hili la Bwawani waliomba millioni 440 na ikapatikana millioni 175, hofu yangu ni kwamba katika upatikanaji wa pesa, na kama ingeweza kupatikana bilioni mbili ambayo sasa umetenga kwenye bajeti ya mwaka huu wa 2021/2022, kwamba sasa kama inaweza kupatikana hiyo bilioni mbili angalau changamoto katika Mji wa Karatu na maeneo mengine ya vijiji ni ingeweza kupungua kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mji ule wa Karatu wakazi wako 62,300, uhitaji wa maji ni lita milioni tano lakini upatikanaji kwa sasa ni 1,680,000, sasa wangeangalia kidogo katika Mji wa Karatu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo hili la Mji wa Karatu, eneo la Bwawani limejaa maji, na kule wameombaa shilingi milioni 175 ambayo kwa sasa hivi hajaweweza kwenda kufanya kazi kutokana na eneo lile kujaa maji, wanaomba ile milioni 175 ambayo sasa ililetwa kwa ajili ya Mji wa Karatu eneo la Bwawani iende katika eneo lile la Ganako ambako sasa kule kazi inaweza kufanyika kwa sababu kule kuna borehole mbili katika eneo hili la Ganako.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu kwa Waziri ni kwamba hii shilingi milioni 175 ambayo kwa sasa huwezi

kufanya kazi katika Bonde lile la Bwawani iende sasa katika eneo lile la Ganako ili angalau uhitaji wa maji uweze kuongeza. Mradi huu wa Ganako ukikamilika upatikanaji wa maji pale unaweza kwenda kwenye asilimia 61. Ombi langu kwa Wizara ni kwamba ile shilingi milioni 175 ambayo kwa sasa Mji wa Karatu pale Bwawani hauwezi kufanya kazi kutokana na maji yamejaa pale na Mheshimiwa Naibu Waziri alitembelea eneo lile sasa iende katika eneo hili la Ganako ili angalau tutoke kwenye asilimia 33 twende asilimia 61. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo hili la Bwawani maji yanajaa mara kwa mara na watu wanashindwa kupata maji kutokana na eneo lile kujaa maji. Tuliomba Wizarani shilingi milioni 40 kuhamisha pampu pale kwenda kwenye eneo lingine la juu kidogo ili angalau wananchi wasiendelee kuteseka.

Niwaombe watu wa Wizara waweze kutupatia shilingi milioni 40, ni hela ndogo sana, ili tuweze kuhamisha ile borehole. Mheshimiwa Naibu Waziri ni shahidi ametembelea maeneo yale na amejionea kwamba kipindi cha mvua watu hawawezi kupata maji katika Mji wa Karatu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mji wa Karatu maeneo ya vijijini kuna mradi wa *World Bank* wa vijiji 10, huu mradi una zaidi ya miaka 10 kila siku ni ukarabati maji hayapatikani. Nafikiri katika eneo hili tumetengewa shilingi bilioni 2, kama itapatikana mradi huu wa *World Bank* kwa vijiji 10 katika eneo la Karatu Vijijini maji yanaweza kupatikana ili na kule kijijini tuweze kufika asilimia kubwa kidogo kuliko tuliyonayo sasa hivi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo lile la Karatu Vijijini upatikanaji wa maji katika Tarafa ya Bulumbulu ni wa njia ya mtitriko na katika eneo hili wametenga shilingi milioni 520 ikipatikana kwa muda nafikiri tutakuwa tumepeiga hatua kidogo kule kwetu Karatu. Mimi sina mashaka maana Waziri ameanza vizuri na namtakia kila la kheri ili angalau eneo hili la maji tuweze kulipatia ufumbuzi vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Karatu tunaomba sana hii shilingi milioni 40 tuweze kuipata lakini vilevile tunaomba hii shilingi milioni 175 iweze kwenda eneo lile la Ganako ili angalau wananchi wale wa Karatu waweze kutoka kwenye asilimia 33 kwenda asilimia 61.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna miradi mbalimbali katika eneo letu la Karatu. Kuna mradi huu wa Mang'ola Juu ambaao ni wa *World Bank* ambaao kwa sasa wametenga shilingi milioni 100. Vilevile kuna mradi huu ambaao unaenda Laja/Umbangw ambaao umetengewa shilingi milioni 519. Mradi wa Chemchem umetengewa shilingi milioni 200 na mradi wa Gidbaso ambaao umetengewa shilingi milioni 180.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kuna mradi huu wa Makhoromba ambaao umetengewa shilingi milioni 240. Vilevile kuna mradi wa Kwa tom ambaao umetengewa shilingi 65. Pia kuna mradi huu wa Gendaa ambaao umetengewa shilingi milioni 45 na mradi wa Endala ambaao umetengewa shilingi milioni 136.

Pia kuna mradi wa Kilimattembo, Rhotia, Rhotia Kainam, Lositete, Kitete na Marera ambaao umetengewa milioni 520 na mradi wa Chemchem, Kambi ya Simba, Huduma, Bashay, Endesh na Endagem umetengewa shilingi milioni 50.

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya fedha kwa Jimbo langu ni Sh. 2,412,900,135. Fedha hizi zikipatikana kwa Jimbo la Karatu tutapiga hatua zaidi ya kimaendeleo kwa sababu Mji wa Karatu ni Mji wa kimaendeleo na utalii na sisi si wachovu ni wakulima wazuri tu ambaao tunaleta mchango mzuri katika eneo la mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na pia naunga mkono hoja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Dustun Kitandula atafuatiwa na Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, Mheshimiwa Neema Mwandabila ajiandae.

MHE. DUSTUN L. KITANDULA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ili nichangie kwenye mjadala wa hotuba iliyopo mbele yetu. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametupa uhai na kwamba tunaishi kuwatumikia Watanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, moja kwa moja, nianze kuishukuru Serikali, kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na timu ya Wizara ya Maji, kwa hiki ambacho kwa mwaka huu nakiona katika bajeti hii. Nimesema mara nydingi kwamba katika Mkoa wa Tanga kama kuna Wilaya inashida kubwa ya maji ni Mkinga. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepeiga kelele sana kuzungumzia tatizo la maji Mkinga, tulikuwa hatusikikisikiki hivi lakini hizi dalili zinazoziona kwenye bajeti hii namshukuru sana Mheshimiwa Waziri na timu yake. Kwa mara ya kwanza katika bajeti hii Wilaya ya Mkinga tumetengewa shilingi bilioni 5 za maji. Katika historia ya kuwepo kwa Mkinga hizi ndiyo fedha nydingi kwa mara ya kwanza. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tukisikia wenzetu wana shilingi bilioni 15 au 20, sisi tunashukuru kwamba kwa mara ya kwanza tumepeangiwa shilingi bilioni 5. Hatujawaji kuwa na mradi mkubwa wa Kitaifa kwa mara ya kwanza kilio chetu cha kuwekewa maji kutoka kwenye Mto Zigi kimesikika, nawashukuru sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naangalia vitabu pale nimeona mmetutengea shilingi bilioni 3, nawashukuru sana. Sasa vijiji vile 32 vya Tarafa ile ya Mkinga vinaenda kupata maji ya uhakika. Nawashukuru. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, najua fedha hizi hazitoshi lakini ule uthubutu tu wa kusema hapana tuanze kwa kupeleka shilingi bilioni 3 mimi nawashukuru sana. Niwaombe wakati tunapoenda ku-*design* bomba lile tuhakkishe inafanyika kwa *full capacity*. Kwa nini nasema hivi? Ni kwa sababu Mkinga ukanda ule ndiyo wenye *potential* kubwa ya uwekezaji wa viwanda. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi Mheshimiwa Rais wameingia *Memorandum of Understanding* na Rais wa Kenya kwa ajili ya bomba la gesi kutoka upande huu kwenda Kenya. Waziri Mkuu alipokuja alituhakikishia kwamba kituo kikubwa cha kuchakata gesi hiyo kitakuwa Mkinga. Nini maana yake? Maana yake tutavutia ujenzi wa viwanda, kile kilichotokea Mkuranga kinaenda kutokea Mkinga. Sasa tujipange tuhakikishe bomba hili linakuwa na uwezo mkubwa ili tusije kuhangai ka wakati ujao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, Miradi ya Mbuta na Mwakijembe, nilikuambia Mheshimiwa Waziri kwamba miradi hii sijui kwa nini imesahaaulika kuitwa miradi ya kichefuchefu, kwa sababu tumekwenda mimi na wewe unajua, Naibu Waziri amekwenda, miradi hii tangu mwaka 2019 mpaka leo hakuna kinachoelewaka. Kwa mwaka mzima huu wa bajeti hakuna kazi yoyote iliyofanyika kuendeleza miradi hii miwili, hii haiwezi kuwa sawa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeambiwa ule mradi wa Mwakijembe *arbitration* ile imeisha lakini sijui kuna kigugumizi gani. Pale Mbuta tumeposta mkandarasi alikuwa anatakiwa aanze kazi mwezi Januari ameshindwa vigezo, tumemtafuta mkandarasi wa pili, majadiliano yanaendelea hii itatupeleka mpaka kuisha mwezi wa sita, mwaka mzima miradi hii itakuwa hiajafanya chochote, haiwezi kuwa sawa. Naomba tuongeze jicho kuangalia jambo hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nakushukuru kwamba kuna miradi kadhaa imetengewa fedha. Mradi wa Kwantili, Churwa, Muheza, Mihunduro, Bangamwevengero, Mchangani tuna shilingi milioni mia moja na kitu. Kuze, Kibago, Bosha kwa Ntindi, Muze, Kafishe tuna shilingi milioni 173. Bantu, Kwa Ngena, Machimboni tuna shilingi milioni 100. Kidundai, Kwekuyu, Bombo Mbuyuni, Mgumbo, Shashui, Emsambia mpaka Vuga tuna shilingi milioni 300 na Ng'ombeni tuna shilingi milioni mia mbili na kitu. Kuboresha ule mradi wa Daruni tuna shilingi milioni 300. Gombero, Vunde, Manyinyi, Jirihini, Dima tuna shilingi milioni 123. Mowa, Zingibari, Mayomboni shilingi milioni 82. Nashukuru sana kwa miradi hii lakini wakati

nikushukuru kutengwa fedha hapa ni jambo moja, fedha hizi kwenda katika halmashauri ni jambo lingine. Tunaomba fedha hizi zifike ili tuondokane na tatizo la maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi atafuatiwa na Mheshimiwa Neema Mwandabila, Mheshimiwa Josephine Genzabuke ajiandae.

MHE. IDDI K. IDDI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Msalala ili nichangie hotuba ya Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja kwa moja nianze kwa kuipongeza Wizara ya Maji kwa kazi kubwa inayoendelea kuifanya. Pia niishukuru Serikali kwa kuona umuhimu wa sasa wa wananchi wa Jimbo la Msalala kupata maji safi na salama. Pia tutakuwa wachoyo wadhila kuishukuru Serikali kwa fedha nyngi ambazo wametutengea sisi Jimbo la Msalala. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imetutengea kiasi cha Sh.4,600,000,000.00 kwa ajili ya miradi mbalimbali katika Jimbo langu la Msalala. Kwa kweli kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Msalala tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri, tunaishukuru sana Serikali lakini pia tunamshukuru sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama yetu Samia Suluhu Hassan. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeweza kutengea kiasi cha shilingi milioni 558 katika mradi wa maji ambaao utahudumia Vijiji vya Nduku, Ntobo, Busangi. Niombe baada ya fedha hizi kutoka basi ziende haraka iwezekanavyo ili kukamilisha mradi huu ambaao ni changu na utaweza kupunguza tatizo la maji katika Kata hii ya Busangi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri na Serikali hajiaishia hapo tu, wameenda kutupatia kiasi cha shilingi milioni 250

kwa ajili ya *extension* katika mradi mkubwa wa maji. Hata hivyo, kuna mradi mkubwa ambao unaitwa Manguirogi ambao ni *joint venture* katika Serikali na Mgodi, hii ni fedha ya *CSR*. Namwomba Mheshimiwa Waziri baada ya Bunge hili akubali kuambatana nami ili twende kule tukaangalie ili tuweze kufahamu ni kiasi gani Serikali imeweza kuchangia katika mradi huu lakini pia mgodi umechangia kiasi gani? Fedha hizi ni za *CSR* na tunatamani sana tuone ili tujue chenji yetu imebaki kiasi gani ili kusaidia kusambaza maji katika Kata za Runguya, Ipinda, Segese na maeneo mengine. Mradi huu unatoka Mangu unaishia Irogi, niombe Serikali bsi iweze kutenga fedha tena kwa ajili ya kufanya *extension* katika maeneo ya Ikinda Kata za Lunguya, Nyangarata, lakini na maeneo mengine ili kuweza kusaidia na kupunguza tatizo la maji. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Segese inakua kwa kasi sana kwa sasa na matarijo yetu ni kuhakikisha kwamba tunapata maji ya ziwa ili watu waweze kunufaika. Pia tuna Makao Makuu ya Ntobo ambayo kimsingi tunaenda kuyazindua muda si mrefu, niombe mradi huu unaotoka Nduku kuja Ntobo lakini pia mradi huu unaotoka Mangu kuja Irogi *extension* iweze kufanyika pia maji haya yaweze kusogea katika Makao Makuu ili ituwezeshe kuwafikishia wananchi miundombinu hii ya maji na tuweze kuwahimiza sasa waweze kuwekeza kwa kiwango cha juu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna mradi mkubwa ambao umeshakamilika wa Kagongwa – Isaka. Mheshimiwa Waziri kama anakumbuka alikuja kuzindua na Mheshimiwa Rais alikuja pale na alitaja mbele ya Mheshimiwa Hayati Dkt. John Pombe Magufuli kwamba kuna chenji imebaki. Pia mradi huu unapita katika Kata ya Mwakata ambayo haina maji. Naomba Waziri aone ni namna gani chenji iliyobaki katika mradi unaotoka Kagongwa kwenda Isaka mnawenza kuzipeleka katika Kata ya Mwakata ili sasa na wakazi wa Kata ile waweze kunufaika. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niipongeze Serikali na Mheshimiwa Waziri kwa kututengea kiasi cha shilingi

1,500,000,000 katika Kata za Jana na Mwalugulu. Ni matumaini yangu kama fedha hizi zitaenda haraka na kufanya uzinduzi wa mradi huu utasaidia sana wakazi wa Kata hizi ili na wao waweze kunufaika na mradi huu wa maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kusema kwamba kumekuwa na changamoto ya bili za maji, nimwombe Mheshimiwa Waziri wakati anakuja kutembelea mradi huu Mangu - Irogi tupate fursa ya kutembelea wananchi na kusikiliza kilio chao juu ya ongezeko la bili za maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, niishauri Wizara ione namna gani wanaweza wakaja na *solution* ya kuhakikisha kwamba wanatengeneza mfumo mpya ambao utasaidia kupunguza adha ya ongezeko la bili la maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hivyo tu, niiombe Wizara iweze kuwapatia mafunzo maalum wale wasimamizi kule chini. Hii itawasaidia kutumia miradi hii ya maji ambayo inapelekwa kule na inatumia gharama kubwa ili waone namna gani sasa wanaweza kuanza kusambaza katika miji ya watu na ili wakazi wa maeneo yale waweze kunufaika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishie hapo, ahsante sana, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Neema Mwandabila atafuatiwa na Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko ajiandae.

MHE. NEEMA G. MWANDABILA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia. Awali ya yote, napenda kutoa pongozi zangu za dhati kwa moyo mkunjufu kabisa kwa viongozi wa Wizara hii, Mawaziri, Makatibu kwa namna ambavyo wamekuwa wakifanya jitihada kubwa kuhakikisha tunapata maji katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijachangia kile ambacho kinaugusa moyo wangu sana nilitaka nitoe kama taarifa kwa Wizara hii kwamba ile miradi ya maji waliyoilweka kule Tunduma maji hatupati na kisingizio ni kwamba fedha za kununua LUKU hakuna. Naambiwa kwa wiki fedha inayotakiwa ni karibu shilingi 700,000 hadi shilingi 1,000,000. Kitu ambacho siamini kabisa kwamba Wizara mpaka sasa imeshindwa kukaa na watu wale kule chini kuweza kuweka utaratibu mzuri wa kuhakikisha tunapata maji. Hata hivyo, tunawashukuru sana kwa ile miradi ya maji, tunaamini kama mambo haya madogo madogo atayazingatia tutaweza kupata maji kwa uhakika. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba Wizara iweze kukaa na wale watu wahakikishe Mji kama Mpemba unaokua kwa kasi uweze kupata maji. Ni mji unaokuwa kwa kasi lakini mpaka saa hizi maji hakuna na wanategemea mradi wa kutoka lleje kuja Tunduma kitu ambacho najua mradi huo hautakamilika leo. Niikumbushe Wizara kwa kuiomba kwamba ule Mradi wa Maji kutoka lleje kuja Tunduma ambao ni karibu shilingi bilioni 17 tu, mtusaidie tuweze kufanya kazi haraka kulingana na mahitaji ya Mji wa Tunduma. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nilitaka kuiomba Wizara kuhusiana na maji Wilaya ya Ileje. Maji yanayotoka ni machafu, yana takataka kitu ambacho siamini kama Wizara inashhindwa kutoa chujio la kuchuja maji katika Kata ya Itumba ili tuweze kupata maji masafi. Hata sisi tungependa kuonekana tuna nguo safi, nadhifu na hata yale mashuka kwenye hospitali kule ya wilaya yaye basi yana mvuto kwa sababu maji yale yanapelekea hata mashuka kwenye hospitali ile yanakuwa machafu. Alikuja Mheshimiwa Mollel, Naibu Waziri wa Afya aliona hali halisi na namna mashuka yanavyoharibika katika hospitali ile ya wilaya kutokana tu na kwamba maji ni machafu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, napenda sasa kujielekeza kwenye hoja ambayo kwa kweli inaniumiza na inatia uchungu sana ninapokuwa nikiifikiria.

Katika shule zetu nyingi maji hakuna. Tarehe 8 Machi, nilipata nafasi ya kwenda kwenye shule mbili ya Chikanamlilo na Mpakani Sekondari, Chikanamlilo ipo Wilaya ya Mombasa, tulikuta watoto wanaugua matumbo kwa sababu hakuna maji. Nimshukuru Mheshimiwa Condester aliweza kuwapatia zile taulo za kike zenyewe dawa ili wale Watoto zaidi ya mia moja waweez kupona ule ugonjwa uliokuwa unawasumbua wa matumbo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipopewa hii changamoto pale kwamba maji hakuna nilijaribu kufuatilia, uzuri wake tulikuwa na Mheshimiwa *DAS* pale. Maji katika Kata ya Ndalambo yapo shida ikaonekana ni kwamba shule haiwezi kuvuta yale maji kwa sababu gharama za kulipia yale maji ni kubwa na shule kwa kulingana na pesa inayopata haiwezi kugharamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikaona sasa hii ni changamoto ya sisi kama viongozi kuichukua na kuweza kuisemea kwamba Wizara ya Maji na hizi taasisi nyingine mfano hii Wizara ya Elimu waweze kukaa, wajadiliane, waangalie kwanza ni kwa namna gani hizi shule ziwe na uhakika wa maji? Nilitamani kama viongozi tuje na sheria ya kwamba maji kwenye shule iwe kigezo kimojawapo cha kuhakikisha shule inasajiliwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *imagine* tangu asubuhi mtoto anaenda shulenii, hanawi mikono, atatamani ale kitu, atalamba mikono; penseli zenyewe wanalambo, watoto wataacha kuugua? Kwa hiyo, niseme kwamba kwa hili ningependa kabisa Wizara ya Maji ichukue kama changamoto ya msingi na ikiwezekana kwenye miradi yake ya msingi, waongeze mradi ambao utakuwa mahususi kwa ajili ya taasisi ambazo zinahudumia watu wengi ambazo ni shule, vituo vya afya, mahospitali na vitu kama hivyo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa sababu Sheria ya Maji imetaja wazi kabisa kwamba maji ni haki ya kila mwananchi, maji ni huduma ya msingi, usafi wa mazingira ni huduma ya msingi ya wananchi, watuangazie katika eneo

hili. Kwa sababu, kutibu maradhi yatokanayo na uchafu ni gharama kubwa sana, pia kitendo cha kutokuwa na uhakika wa maji kinasababisha watoto washindwe kusoma vizuri. Hii ni kwa sababu sehemu wanazoenda kutafuta maji ili waje wamwagilie tu kwanza maeneo yao pale ni shida; na maji ya kuja kusafishia tu madarasa yao inakuwa ni shida. Kwa hiyo unakuta mtoto anachoka kuchota maji. Badala ya kukaa atulie kusoma, anawaza tu dumu lake la maji atunze viyi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, baada ya kusema hayo, naomba niseme nashukuru. Mchango wangu unaishia hapo kwa leo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Josephine Genzabuke, atafuatiwa na Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko na Mheshimiwa Boniventura Kiswaga ajiandae.

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika Wizara hii. Kwanza kabisa naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa kibali cha kuweza kusimama ndani ya Bunge lako Tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kuunga mkono hoja hii na nimpongeze Mheshimiwa Waziri Aweso na Naibu wake pamoja na wafanyakazi wa Wizara ya Maji kwa kazi nzuri ambayo wamekuwa wakiifanya.

Mheshimiwa Spika, maji ni uhai, maji ni kila kitu. Sisi Tanzania tumejaaliwa kuwa na vyanzo vingi vya maji; bahari, maziwa, mito mikubwa na midogo, lakini kwa kiasi kikubwa maji haya hayajaweza kuwafikia wananchi. Kwa hiyo, naomba kutokana na bahati tuliyopata Watanzania kwa kupata vyanzo hivyo, basi viweze kumaliza tatizo la maji vijijini. Tusitumie kuchimba visima tu, lakini pale ambapo ipo mito mikubwa, maji yatolewe kwenye ile mito mikubwa yapelekwe kwenda kusambazwa vijijini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, kuna Mto Malagarasi una maji mengi sana. Tulikuwa tunaomba kupidia mto huo, vijiji vile ambavyo vimekaribiana na mto huo viweze kunufaika kwa kupitia maji yanayotoka katika Mto Malagarasi. Vile vile zipo Halmashauri ambazo zinayo miradi ilianzishwa kwa muda mrefu, lakini haijaweza kukamilika. Naiomba Serikali iweze kupeleka pesa ili ile miradi ambayo tayari ilishaanzishwa kwa muda mrefu iweze kukamilika na wananchi waweze kupata maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wanawake wengi wanatumia muda mwingi kwenda kutafuta maji na wanashindwa kufanya shughuli za kuzalisha mali. Kwa hiyo, wananchi wakipatiwa maji, wanawake wataweza kutumia muda mwingi kwenda kuzalisha mali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile ukosefu wa maji unasababisha milipuko ya magonjwa mengi ikiwemo kipindupindu na kuhara, kama wenzangu walivyosema, fedha nyingi zinaenda kutumika kwa ajili ya ununuzi wa madawa. Pia naomba shule za msingi na sekondari zipelekewe maji. Zipo shule nyingine hazina maji kabisa. Watoto wanapata shida na hasa watoto wa kike, wanapata shida kutokana na maumbile yao. Mtoto wa kike anatakiwa kupata maji kila wakati. Kwa hiyo, naomba maji yapelekwe shulen; katika shule za msingi na sekondari ili watoto waweze kuondokana na adha hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia karibia kila mwezi Watoto wa kike, wapo ambaao wanapoteza siku tano hawaendi shulen i kabisa kutokana na maumbile yao, wanashindwa kwenda shule. Matokeo yake, zile siku tano ambazo mtoto anakuwa hakwenda shule, anapoteza muda wa kusoma, hawezi kufanya shughuli zake za masomo vizuri. Sasa siku tano hizo za kila mwezi, ukizidisha kwa mwaka mzima, mtoto wa kike amepoteza siku ngapi? Ni siku nyingi kabisa. Matokeo yake baadhi ya watoto wanaathirika na kutokufanya vizuri kwa sababu ya ukosefu wa maji mashulen. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Kasulu una tatizo kubwa la maji, iwe kiangazi iwe masika, mji ule maji yanayotoka ni machafu. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Serikali itusaidie kututengenezea kichujio ili maji yanayotoka katika Mji ule yaweze kuwa masafi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika eneo la Mwandiga nalo bado kuna shida ya maji. Mabomba yametandikwa, miundombinu imesambazwa lakini bado maji hayajafika katika Mji wa Mwandiga; na Mji huo kwa muda mrefu sana, wanapata shida ya maji. Kwa hiyo, naomba kwa sababu miundombinu imeshasambazwa, mabomba yaweze kuletwa kusudi maji yaweze kupatikana katika Mji wa Mwandiga. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, halikadhalika katika Mji wa Kibondo tulipatiwa shillingi milioni 700, lakini bado maji hayajawafikia wananchi. Nilikuwa naomba basi, Serikali iweze kupeleka fedha hizo haraka iwezekanavyo ili kuweza kukamilisha miundombinu hiyo wananchi waweze kupata maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko atafuatiwa na Mheshimiwa Boniventura Kiswaga na Mheshimiwa Francis Mtega, ajiandae.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuweza kunipatia fursa hii kuchangia kwenye Wizara muhimu sana na mtambuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji ni uhai, lakini zaidi maji ni uchumi. Bila maji hatutaweza kuwa na viwanda ambavyo tunaimba “Tanzania ya Viwanda.” Bila maji hatuwezi kuwa na kilimo chenye tija wala ufugaji; bila maji, wamesema wengi hapa kwamba, afya za Watanzania zitatetereka na itaenda kuigharimu Taifa kuweza kugharimia hawa Watanzania ambao watakuwa wameugua, lakini pia

wataacha kufanya kazi za maendeleo kwenye nchi yetu. Bila maji pia tumeshuhudia ndoa nyingi zikiharibika na watu wetu wakiliwa na mamba, watoto wetu wa shule wakipoteza muda mwingi kwenda kutafuta maji. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa ulijiwekea malengo ambayo yalikuwa kwamba kufikia mwaka 2021 kwa maana ya baada ya miaka mitano, maji vijijini yawe yamepatikana kwa asilimia 85 na maji mijini yawe yamepatikana kwa asilimia 90, lakini kwa taarifa ya Waziri ambayo ameitoa hapa ni kwamba maji sasa ni asilimia 72.3 vijijini ambapo pia siyo kiuhalisia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Mpango wameainisha, kwa kipindi chote cha miaka mitano kufikia Desemba, 2020 walikuwa wametekeleza miradi 1,423 ambayo ilikuwa na vituo au visima 131,370. Katika vituo hivyo au visima, ni 86,000 tu vilikuwa vinatoa maji na vituo au visima 44,590 havitoi maji. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hayo yote yanatokea mosi, fedha tunazopeleka hazina usimamizi na ufuatiliaji wa kina, unakuta fedha za Watanzania masikini zinapotea tu. Zaidi walishindwa kufikia malengo kwa kuwa bajeti tunazotengahaziendi kiuhalisia. Hata ukiangalia bajeti ya 2020/2021, tulitenga shilingi bilioni 705 hapa, lakini Waziri anakiri kwenye ibara ya 22 kwamba mpaka Aprili, 2021 zimeenda shilingi bilioni 376 tu, ambayo ni asilimia 53; ndani ya miezi kumi, bado miezi miwili tu utaona kabisa dhahiri kwamba hawataenda kutekeleza kama ambavyo wamepanga. Kwa hiyo, hata hapa tunaweza tukawa tunakaa, Wabunge tunafurahia tumepewaa miradi kadhaa kwenye maeneo yetu, lakini kiuhalisia haitaenda kutekelezeka. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo hapo kwenye ubadhilifu wa miradi yetu hii ya maji; na tumekuwa tukiongea hapa kwa kweli, kuanzia Bunge la Kumi, Bunge la Kumi na Moja na Bunge hili la Kumi na Mbili Wabunge wanasi mama wanalamika fedha zinazopotea. Mheshimiwa Waziri

ameainisha hapa kwamba kuna miradi 85 ilibidi irudiwe tena. Nitachukua michache tu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kwenye Kiambatanisho Na. 2, mfano ameainisha Mradi wa Ntomoko, Kondoa huko Dodoma zilitumika shilingi bilioni 2.2, lakini tena kuuhuisha, wametumia shilingi bilioni 2.2 na kitu, asilimia 100. Ukienda kule Mombo, Mbuyuni kuna mradi ulikuwa umeshatumia shilingi milioni 400 ukawa haufanyi kazi. Ili kuuhuisha, imebidi tena watumie shilingi milioni 300, asilimia 85.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda Arusha huko Karatu Remote, kulikuwa na bwawa linajengwa huko, lilitumia shilingi milioni 124 likawa halijafikia kufanya kazi. Ili kulihuisha lifanye kazi, ikabidi watumie tena shilingi milioni 204, asilimia 165. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujua, hawa watu waliofanya huu ubadhirifu wamechukuliwa hatua gani? Tumeshaomba hapa, Wizara ifanye ukaguzi wa kina kwenye miradi yote ili tuweze kujua ni miradi mingapi imetumia kiasi gani cha fedha ya Watanzania masikini na haifanyi kazi na hao watu wamechukuliwa hatua gani? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine, naenda kwenye miji 28 ambayo na Tarime ilikuwemo. Ni dhahiri hii miji 28 ingekuja ingeweza kutusaidia sana. Kuna fununu kwamba kuna baadhi ya miji itaenda kuondolewa ikiwepo Tarime, Mafinga, Songea na kwingine. Zile dola 460, mwaka 2020 aliongea Mheshimiwa Kitwanga hapa kwa machungu sana, akaeleza kwamba hizi dola 460 zingeweza kutosha miji hata 54; na akaeleza kwamba kuna harufu harufu ya upotevu wa fedha kwenye hii kitu. Sasa badala ya 28, wanataka wapunguze irudi 24.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa *DPR* ya sasa hivi; kwa maana ya mapitio ya kina ya mradi huu kwa sasa, wanaonyesha kwamba hata mtandao wa maji wanaenda kuupunguza kutoka kilometra 5,751 kwenda 711. *Capacity*

wanaipunguza kutoka 98,450 wanapeleka 48,150. Sasa unajiliza, kama wanapunguza haya yote, tulitarajia basi gharama ingeenda kuwa kinyume na hapo, badala ya dola 460, ziwe dola 225. Tujiulize nyininge zinaenda wapi? (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Tarime mathalani, ukisema ugawanye tu, huwezi ukatumia dola milioni 16.2 ambayo ni shilingi bilioni 38. Tarime pale; kutoka Rorya kuja Tarime ambao watanufaika na wananchi wa Rorya karibia zaidi ya Kata 11, siyo zaidi ya shilingi bilioni 16 tu. Kwa hiyo, tunaomba sana. Kila nikiongea namkumbuka Mheshimiwa Kitwanga mwaka 2020 alivyokuwa akilalamika. Tuna wataalam wetu, tuna *ma-engineer* wetu, tuna *technician* wetu hapa hapa Tanzania. Kama *WAPCOST* tunaona ni shida, basi ufanyike uchunguzi wa kina tena. Hata Bunge lako kupitia hii Kamati ya Maji, muunde Tume ipitie huu mradi. Hizi hela ni nyangi sana. Ni mkopo ambao Watanzania masikini wataenda kuulipa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuhakikishe kwamba, tunaenda na ile *review* ya mwanzo na siyo ya sasa hivi ambayo wanasema wanaenda kupunguza baadhi ya miji ili iweze kutumika *effectively* kuhakikisha kwamba siyo tu miji 28, ikiwezekana na miji mpaka 54. Hata hii 28 yenye, 24 ambayo itabahatika kupata, mtandao wa maji nao wameupunguza sana. Kama ilikuwa wakamilishe kwa Tarime nzima Kata nane, sasa hivi watajikuta labda wanakamilisha Kata mbili au tatu. Haiwezekani kabisa, kuna harufu ile ile ya uendelevu wa ubadhilifu wa fedha. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri anajitahidi sana, anapita huko kuhakikisha kwamba miradi inahuishwa, lakini sasa bila kung'oa mizizi ya ubadhirifu wa fedha kwenye Wizara hii, tutaendelea kulia na fedha za Watanzania masikini zitaendelea kupotea. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa Tarime, vile visima 23 mmechimba visima vinane lakini maji yanatoka kwenye visima sita. Mradi wa Gibaso hautoi maji kule Tarime Vijijini na mradi wa Mwema hautoi maji ambao ulitumia fedha

nyingi sana. Tunaomba sana, sana uweze kupitiwa na hawa ambao wanawajibika kupoteza hizi fedha waweze kuchukuliwa hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Boniventura Kiswaga, atafuatiwa na Mheshimiwa Francis Mtega na Mheshimiwa Ing'ondo Ramadhan Abeid ajiandae.

MHE. BONVENTURA D. KISWAGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia kwenye Wizara hii muhimu ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naomba kwa namna ya pekee nimpongeze na kumshukuru Waziri wa Maji, ndugu yangu Mheshimiwa Awesso ambavyo anajitahidi sana kuhangaikia kuhakikisha kwamba wananchi wanapata maji katika nchi hii pamoja na Naibu wake na Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, ndugu yangu Sanga. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo wenzangu wamesema hapa, kwa kweli maji ni uhai na hakuna kitu kingine ambacho kila mwanadamu anakitumia kama siyo maji. Kuna vitu vingi vizuri, vitamu duniani lakini wanadamu hawavitumii, lakini kila mmoja anatumia maji. Kwa hiyo, tutakapokwenda kuhakikisha kwamba tunatoa huduma za maji kwenye vijiji vyetu, tutahakikisha kwamba wananchi sasa tunawajengea uchumi ambao wanastahili kuwa nao. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, moyo usiokuwa na shukrani hukausha mema mengi. Kwa hiyo, napenda kuishukuru Serikali ya Awamu ya Tano kwa kutuletea mradi wa maji mkubwa katika mji wetu mkubwa wa Magu. Kwa hiyo, Mji wa Magu umepata maji, lakini maji yale ni mengi mno ambayo yanastahili kuhudumia vijiji 32 vyenye takribani wakazi 180,000. Maombi haya tumeshayaleta ili angalau haya maji yaweze kuwafikia wananchi wa Jimbo la Magu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika vijiji hivyo 32, kuna Kijji cha Mahaha ambacho kina wakazi wengi sana; Shishan, Isolo, Kabale pamoja na vijiji vingine; Kungulu, Ndagalu, Salama, Mobulenga, Nyashoshi, Kuhumbi, Misungwi, Sagani, Mwalina, Mwamabanza, Watelesha, Mwamibanga, Iseni, Bugabu, Chandulu, Vijninjibili pamoja na Nyahanga. Ni vijiji 32 vyenye wakazi 182,000. Vijiji hivi vikipata maji tutakuwa tumewakomboa sana wananchi wa vijiji hivyo na hasa akina mama ambao wanaamka usiku wa manane kwenda kuchota maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, unajua wazalishaji wengi wa uchumi kule vijijini ni akina mama, lakini muda wote wanaumaliza kutafuta maji. Anaamka saa nane anakwenda kwenye maji, anarudi saa tano, hana muda hata wa kwenda kwenye mashamba kwa ajili ya kuzalisha kwenye kilimo. Kwa hiyo, nalomba sana Wizara ya Maji, kwa sababu Mheshimiwa Awesso ameshafika Magu pamoja na Sanga, waone namna ambavyo wanaweza kutusaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mradi huu kulikuwa na upungufu wa kilometra 24 katika Mji wa Magu pale na ninaamini Rais wetu mpPENDWA, hivi karibuni atakuja kuufungua huu mradi wa maji. Sasa hizo kilometra 24 zilikuwa zinahitaji shilingi milioni 260. Wakati huo Awesso akiwa Naibu Waziri na Sanga akiwa Naibu Katibu Mkuu, wote wamepandishwa kuwa Waziri na Katibu Mkuu, hebu mwelekeze shilingi milioni 260 ili kilometra 24 katika Mji wa Magu wananchi waweze kupatiwa maji. Kwa sababu, akija kufungua Rais, halafu wananchi wakanyoosha mabango, sasa sjui atafukuzwa Mkurugenzi au DC au atafukuzwa Waziri au Katibu Mkuu? Nami nataka Waziri na Katibu Mkuu mwendelee kuwepo kwenye Wizara hii. Hebu angalieni namna ambavyo mnaweza kusaidia ili wananchi wasiinue mabango. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna Mji wa Kisesa pale ambao chanzo chake ni Butimba. Chanzo hiki ni cha muda mrefu na tayari mkandarasi ameshapitishwa. Tatizo kubwa ni *exemption* ili aweze kutoa vifaa vyake bandarini. Hebu

tuliangalie suala hili la *exemption* kwa sababu ni suala ambalo linakwamisha sana kuendeleza miradi ambayo iko tayari na fedha ziko tayari. Mradi huu utahudumia katika Mji wote wa Rwanyima, Nyamagana kwa ujumla, Buswelu pamoja na Kisesa, Usagara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba sana kwa sababu mradi huu ndiyo utakaokwenda kutatua changamoto nydingi katika Mji wa Kisesa ukiwa na Kata ya Bujola, ukiwa na Kata ya Bukandwe, ukiwa na Kata ya Bujashi. Kwa hiyo, haya ni maeneo muhimu sana ya kiuchumi na tunaamini kwamba maji yakifika na kwa sababu Mheshimiwa Hayati Rais Dkt. John Pombe Magufuli alitaja Kisesa kwamba iwe Makao Makuu ya Wilaya mpya ya Kisesa, kwa hiyo, maji haya ni muhimu sana, yanashubiriwa na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, haya ni maeneo muhimu sana ya kiuchumi. Tunaamini kwamba maji yakifika, kwa sababu hayati Rais Dkt. John Pombe Magufuli alitaja Kisesa kwamba iwe Makao Makuu ya Wilaya Mpya ya Kisesa. Kwa hiyo, maji haya ni muhimu sana, yanashubiriwa na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa na miradi inayozunguka Ziwa Viktoria vijiji 16. Wataalam wa Wizara ya Maji walifika na tayari upembuzi yakinifu umekwishafanyika. Tulikuwa na matarajio kwamba mradi huu ungekuwa umeanza bajeti hii ya fedha tunayoendelea nayo, lakini mradi huu haujaanza. Vijiji hivi viko kabisa kwenye maeneo ambayo Ziwa Victoria linapita pale. Vijiji hivi ni Shinembo, Bundilya, Nyamhanga, Inolelo, Mwamanga, Kigangama, Lutale, Kayenze, Kageye, Itandula, Rangi, Matale, Ihushi, Sese na Busekwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Mheshimiwa Waziri anakuja ku-*wind up* hapa atueleze kwa sababu ni ahadi ya wananchi kwamba tutakwenda kutatua kero za maji na kumaliza kabisa ili wananchi waweze kupata huduma ya maji safi ili angalau wananchi wawe na matumaini ya kutosha kwa Serikali yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, niunge mkono hoja kwa sababu namwamini Waziri pamoja na Naibu na Katibu Mkuu Wizara ya Maji. Ahsante sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, kwa orodha ya majina niliyonayo hapa, ya Wabunge wanaotaka kuchangia, Wabunge wanaofuata kuanzia sasa watachangia kwa dakika tano kila Mbunge.

Mheshimiwa Francis Mtega, atafuatiwa na Mheshimiwa Ramadhan Igihondo Abeid na Mheshimiwa Twaha Mpembenwe ajiandae.

MHE. FRANCIS L. MTEGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia katika Wizara hii muhimu ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Aweso; na Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa *Engineer Maryprisca Mapunda*.

Pia niwapongeze sana Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na wataalam wote wa Wizara ya Maji kwani wamefanya kazi kubwa sana na tunajua nchi yetu hii ni kubwa sana lakini kwa jitihada zao kwa kweli wamejitalidi mpaka hapo walipofikia. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo naomba nijikite kuchangia mambo mawili tu. Moja ni kuwajibika na la pili ni kuwajibishana, kwani naamini hizi ndizo nguzo kuu kabisa kujenga nidhamu kwa wafanyakazi ili waweze kutimiza lengo la kuwapa maji wananchi wote kule vijijini. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, naomba nitoe changamoto kadhaa zinazowapata wananchi wetu kule vijijini. Yawezekana kwa kuwa hii ni Wizara kubwa na inajumuisha Wizara nyingine, zile changamoto ambazo zitahusu moja kwa moja Wizara hii Mheshimiwa Waziri atazijibu anapojumuisha, lakini zile ambazo zitahusu labda Wizara zingine na wenyewe

watapata nafasi kujibu watakapokuwa wanatoa hotuba zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa mambo ya washirika na mamlaka zilizo chini ya Wizara. Nimeona katika hotuba ukurasa wa 80, Waziri ameellezea namna anavyoshirikiana nao na ametoa miongozo. Hata hivyo, kanuni hizo zinafanya baadhi ya mamlaka hizo pengine kwa kutofahamu au kwa makusudi kabisa kufanya changamoto kubwa sana kwa watumiaji wa maji kule vijijiini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na maji safi na mazingira. Wananchi wanapata mfadhili awasaidie kujenga tenki kubwa la maji, naenda *RUWASA*, *RUWASA* wana masharti yao. Wanasema kwanza maji yale yapimwe na Mkemia Mkuu, lakini pia bonde waje waidhinishe, wapime kina cha maji. Sasa ukienda bonde wao watasema tunasubiri kwanza mvua zinyeshe tuone maji huwa yanajaa kiasi gani. Ukienda wakati wa mvua wanasema tusubiri kiangazi tuone maji huwa yanapungua kiasi gani. Hivyo wananchi wanakosa huduma ya maji. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, maji yale wananchi huwa wanayatumia muda wote. Sasa mfadhili anataka kuongeza wingi wa maji hivyo kumbe wangeweza kutoa kibali, tenki likajengwa huku wanasema vipimo hivyo viendelee kwa vile maji yale yanatumika moja kwa moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nije katika umwagiliaji. Wakulima wale huwa wanahangaika sana. Wanaenda Mamlaka ya Bonde, Bonde wanasema sisi tumesitisha vibali, hatutoi vibali kabisa, lakini unakuja kwa Sekta ya Umwagiliaji, wao wanasema sisi tunaruhusu mfereji upite hapa lakini kule kibali hawatoi. Sasa wananchi hawa wanaendelea kupata changamoto kubwa sana. Wananchi hawa muda wote wanapita mamlaka zingine za mifereji wanawatoza ada ya maji. Ukienda Mamlaka ya Bonde wanasema sisi hatujapata ada yoyote na hawa hawana *control number*, leo watapita na *counter book* jipya, kesho watapita na *ki-note book*, anakusanya fedha na hazieleweki zinaenda wapi. Huku

analipa elfu 50,000 kwa heka moja, fedha haziingji Serikalini, lakini, mkulima huyu anauza gunia moja shilingi 45,000, kwa hiyo ni changamoto kubwa sana kwa watumiaji wa maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye kuwajibishana. Kuwajibishana kwa upande wa Wizara. Utendaji kazi kwa upande wa Wizara mambo ni mazuri sana, mambo yanaenda vizuri kama nilivyopongeza lakini kule kwa watendaji wa chini kwenye vijiji namwomba Mheshimiwa Waziri akae na wadau mbalimbali aongee nao. Hii itampa picha namna gani mambo yanaenda kule kwa sababu nimeona katika ukurasa wa 80 wa kitabu ametaja anavyoweza kushirikiana...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. FRANCIS L. MTEGA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kusema kwamba ushirikiano wa Waziri na Wizara ya TAMISEMI, ningeomba hizi Mamlaka zote ziwajibike kwa Waheshimiwa Madiwani. Waheshimiwa Madiwani kwenye Baraza lao ndiyo pekee wanaoweza kuhoji na wanaweza angalau wakafuatilia miradi ile kwa ukaribu Zaidi. Tumeona akienda Waziri mwenyewe na Mheshimiwa Naibu Waziri wanakuwa wakali lakini hawa Madiwani wanaweza kusimamia kwa ukaribu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Ighondo Ramadhan Abeid, atafuatiwa na Mheshimiwa Twaha Mpembwenwe na Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile ajiandae.

MHE. ABEID R. IGHONDO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia fursa hii angalau niseme mawili matatu kwenye mjadala huu wa Wizara hii ya Maji. Awali ya yote, kutokana na muda naomba nitambue kazi nzuri

inayofanywa na watendaji pamoja na Mawaziri wa Wizara hii. Kwa mantiki hiyo, niishukuru Serikali kwa miradi mikubwa ya maji ambayo imekwishakamilika na inatoa maji hivi sasa kwa upanuzi mkubwa wa njia za maji pamoja na miundombinu katika Kijiji cha Halunyangu, Kijota, Mgori, Mangida, Mughamu pamoja na Msisi. Miradi hii kwa kiwango kikubwa imeondoa adha kwa wananchi ambao walikuwa wanapata tabu kweli kweli wanapohitaji huduma ya maji. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti hii nashukuru na naipongeza Serikali kwa kutupatia fedha kwa ajili ya miradi mikubwa minne ya maji. Kijiji cha Mwighanji, Mitula, Migugu na Ughandibe. Hatua hii ni nzuri sana na naomba sana Serikali ihakikishe miradi hii inakamilika kwa wakati kama ambavyo imepangwa. Kwa mazingira hayo, naomba sasa *DDCA*, ambaao ni Wakala wa Uchimbaji Visima vya Serikali wafike mara moja kwa ajili ya kuanza kazi ili wananchi wetu waondokane na adha ya kupata taabu ya maji. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nitambue pia mchango wa wadau, taasisi binafsi kwenye upatikanaji wa maji katika Jimbo la Singida Kaskazini. Naomba nitambue Shirika la *Rehema Foundation, Silver Crescent* ya kutoka Nchini Uturuki ambaao kwa kushirikiana na Mbunge tangu aanze kazi miezi sita sasa amefanikiwa kukarabati visima 23 ambavyo vilikuwa vimekufa kabisa lakini na kuchimba visima virefu vinne katika Kijiji cha Kinyamwenda, Makuro, Maghandi na Itamka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi kubwa katika hili, visima vile vinatoa maji ya kutosha kuanzia lita 10,000 kwa saa moja. Ni ombi kwamba maji haya yasambazwe. Naiomba Wizara kwa kushirikiana na *RUWASA*, maji hayo yasambazwe ili yawafikie wananchi wengi kwenye vijiji vingi badala ya kubaki pia yanatolewa kwenye centre tu ile pale kilipo kisima.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto kubwa sasa ambayo naiona kwenye miradi mingi ya maji, Singida Kaskazini pamoja na maeneo mengine ni suala la ufuatiliaji.

Ufuartiliaji ni tatizo kubwa sana. Unakuta kisima kimetengenezwa leo kinakaa miaka 20 hakijawahi hata kutembelewa siku moja kuangaliwa changamoto zake.

Kwa hiyo, visima vingi vimekufa. Mathalani, visima hivi 23 ambavyo mimi Mbunge kwa kushirikiana na wadau tumevikarabati, vilichimbwa mwaka 1980 na Shirika la TCRS. Kwa hiyo, niombe sasa Wizara ya Maji wawe na tabia ya kufuartilia miradi, ku-cross check...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. ABEID R. IGHONDO: Lah! Naunga mkono hoja ingawa bado nilikuwa na mengi ya kusema hapa. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Twaha Mpembenwe atafuatiwa na Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile na Mheshimiwa Vincent Mbogo ajiandae.

MHE. TWAHA A. MPENGBENWE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili kuweza kuchangia katika Wizara hii muhimu sana. Awali ya yote nichukue fursa hii kwanza kabisa kumpongeza ndugu yangu Juma Aweso, Waziri, kwa kazi kubwa na nzuri ambayo anaifanya katika Wizara hii. Sambamba na hilo, niseme tu unyenyekevu aliokuwa nao, mabega yake kuwa chini, basi aendelee kuwa hivyo hivyo. Nasema haya kwa sababu japokuwa mimi ni mgeni hapa Bungeni, sijwahi kusikia hata siku moja Mbunge ye yote akisema kwamba Aweso hapatikani kwenye simu, Aweso hana ushirikiano. Hivyo, nampongezahukuru sana Mheshimiwa Aweso kwa kazi yake hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila vile vile, Mheshimiwa Naibu Waziri anafanya kazi nzuri sana. Tangu nifike hapa, kila Mbunge ambaye anamwomba kwenda nae katika Jimbo lake kuzungumza kero za wananchi analifanya hilo. Ni mategemeo yangu vile vile nitamwomba Kiti kikiridhia ili niweze kwenda nae kule Kibiti twende tukazungumze na wananchi wale kwa pamoja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangia katika Wizara hii jambo moja tu la Kitaifa la msingi. Nalo ni kuweza kuwa na timu maalum katika Kanda hizi ili ziweze kufuatilia miradi mikubwa mikubwa. Tukifanya hivyo, tafsiri yake ni kwamba tutakuwa tunakwenda kurahisha mzigo mkubwa ambao Mheshimiwa Waziri anakuwa nao kila wakati. Yeye atakuwa anapokea zile taarifa, akiwa anakwenda kule tayari ana taarifa *in advance*. Kwa hiyo, tukifanya hivyo itamsaidia sana Mheshimiwa Waziri katika kuweza kui-control hii miradi mikubwa mikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nzungumze pale Jimboni kwangu. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri, katika bajeti ambayo ilikuwa imetengwa mwaka 2020/2021 tuna miradi takriban kama minne. Kuna mradi mmoja uko kule Mtunda takriban shilingi milioni 736, mradi ule mpaka hivi sasa bado haujaanza na fedha bado hajapelekwa. Kuna mradi mwingine uko kule katika Kata ya Mahege, takriban shilingi milioni 402, fedha bado hazijapelekwa nayo ilikuwa ni bajeti ya mwaka 2020/2021. Lakini kama haitoshi, kuna mradi ambao uko katika Kata ya Mjao shilingi milioni 486, bado vile vile fedha hazijapelekwa, nayo ni bajeti ya mwaka uliokuwa umepita.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale anapotoka Mbunge kabisa katika Kata ya Mtawanya, kuna mradi wa shilingi milioni 61. Chonde, chonde Mheshimiwa Waziri, sitaki kuamini akili yangu kwamba fedha hizi hazitokwenda kwa sababu anakujuua. Uchapakazi aliokuwanaao Waziri, mambo makubwa ambayo anaendelea kuyafanya katika sekta hii, naamini tu kwamba ni kiasi cha kusema muda utafika, fedha hizi zitakwenda. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri tuweze kwenda kufanya taratibu za msingi kupeleka fedha hizi ili sasa miradi ile iweze kwenda kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimwambie Mheshimiwa Waziri tu kama mambo yatakuwa mazuri ukipata ruhusa kule Tanga. Miradi hii itakapokuwa imekamilika, nataka nimhakikishie Waziri, sisi watu wa Kibiti tuna zawadi tumemwandalia pale. Atakapokuja kama atakuwa

amepata ruhusa kuna zawadi ya *mathna* tunaweza tukampatia ili sasa kwa namna moja au nyingine mambo mazuri yaendelee kufanyika na wananchi wale waweze kunufaika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumze jambo moja la msingi kubwa sana ambalo limewagusa sana watu wa Kibiti pamoja na Wajomba zangu wa Rufiji pale. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri amesema kwamba upembuzi yakinifu unaweza ukaenda kufanyika katika Bonde la Mto Rufiji. Nataka nimwambie, hii kauli ni kauli ya matumaini makubwa sana kwa wajomba zangu wa Rufiji na sisi vile vile watu wa Kibiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka Mheshimiwa Waziri, aamini hili, katika Jimbo la Kibiti kuna kata tangu jimbo lile lianzishwe hazijawahi kuwa na bomba. Kuna Kata ya Kiongoroni, kuna Kata ya Mbuchi, kuna Kata ya Maporoni, kuna Kata ya Msala, hizi kata hazijawahi kuona bomba la maji likiwa linafunguliwa. Kwa hiyo, uanzishaji wa mradi ule utakapokuwa umefanikiwa, nimhakikishie Waziri kwamba, tutamwongeza zawadi nyingine. Tutakwenda sasa katika mambo ya *wathulatha* sio tu *mathna*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima na taadhima na unyenyekevu wa hali ya juu sana, naomba niunge mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile, atafuatiwa na Mheshimiwa Vincent Mbogo na Mheshimiwa Boniface Mwita Getere ajiandae.

MHE. SIMON S. LUSENGEKILE: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia Wizara ya Maji. Kipekee sana nimpongeze sana rafiki yangu Mheshimiwa Aweso kwa kazi kubwa anayofanya pamoja na Naibu Waziri na Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji. Wanafanya kazi kubwa, tunaona kazi zao wanazofanya, kweli zimekuwa ni kazi za msingi. Niwaambie tu kwamba wananchi hasa wananchi wa Busega wana imani kubwa nao kwa sababu

wameona mageuzi makubwa ambayo wameyafanya kwenye Wizara ya Maji kwa huo muda mfupi ambao wamekuwa kwenye madaraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, mageuze hayo ni Pamoja na namna ambayo wamefanya kuhakikisha kwamba wanapunguza gharama za ujenzi wa miundombinu ya maji, kwa sababu tumeona kuna sehemu zingine ambazo wameenda, gharama zimeshuka, unakuta *BOQ* ilikuwa bilioni mbili lakini kwa sababu wamenda pale mmefanya *revision* ya *budget* zimeshuka mpaka kufikia hata bilioni 1.6. Haya ni mageuzi makubwa sana ya kimkakati ambayo wameamua kuyafanya kwenye Wizara yenu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee pia nimshukuru sana Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa alipokuja pale kwangu Mkura aliahidi kutupatia mradi wa maji na sasa mradi tayari umeshaanza kazi, tayari wakandarasi wako pale wanafanya kazi. Kwa kweli, tunawapongeza sana na muda ujao naamini kwamba mradi huu utaanza kutoa maji. Nimwombe tu rafiki yangu Waziri, bado kuna shida ya fedha pale. Naomba apeleke fedha ili mradi ule ukamilike kwa wakati na naamini kabisa kwamba Mheshimiwa Waziri ni msikivu na kwa sababu ni kijana na kwa sababu Wasukuma ni wakarimu aende pale akaangalie namna mradi unavyotekelzwa ili umalizike kwa haraka sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nizungumze suala moja ambalo limekuwa likinipa shida kidogo. Kuna baadhi ya miradi ambayo inaenda kutelekezwa kwenye kata, lakini unakuta kata moja ina vijiji vine, lakini mradi unakuwa wa vijiji vitatu, kijiji kimoja kinabaki. Hili limekuwa ni tatizo na niishauri Wizara, kama wameamua kupeleka mradi kwenye kata, basi ni nzuri kata nzima kumaliza vijiji vyake vyote ili kisibaki kijiji na ikaonekana kama wametengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mfano, kwenye Kata ya Kiloleli yenye vijiji vinne, Kijiji kimoja kimeachwa, Kijiji cha Ilumya, lakini kwenye Kata ya Mwamanyilli, Kijiji kimoja cha Milambe ambako Mbunge anatoka kimeachwa. Kwenye

Kata ya Mkura, Vijiji viwili kwa maana ya Mwang'ale na Chabutwa vimeachwa. Kwa hiyo, nafikiri kwamba tunapokuwa tunafanya *designing* ya mradi kwenye kata husika basi ni vizuri kata nzima iweze kuchukuliwa na vijiji vyote viweze kupata maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimefurahishwa sana na namna ambavyo wameanza kuleta mkakati wa mradi mkubwa wa maji wa Ziwa Viktoria kwenda Itilima ambao kwa awamu ya kwanza utaanza na Busega, utaenda Bariadi lakini pia utaenda Itilima. Mradi huu ni mradi mkubwa na ndio mradi pekee ambao *uta-so/ve* tatizo la maji kwa Wilaya ya Busega, Wilaya ya Bariadi na Wilaya ya Itilima.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe Mheshimiwa Waziri, kwamba, moja ya mradi ambao unatakiwa macho ya Waziri yaende hapo ni huu mradi mkubwa sana, kwa sababu hii miradi mikubwa unapokuwa umemalizika ni mradi ambao utahudumia wananchi wengi. Pale kwangu Jimbo la Busega zaidi ya vijiji 42 vinaenda kupitiwa. Mradi huu kwa Mkoa wa Simiyu utapita kwenye vijiji 256.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba na nimeona Waziri tayari ameweka kwenye Mpango bilioni 19 kwa ajili ya kuanza kati ya bilioni 400. Nimwombe kwamba awekeze sehemu hii ili wananchi wengi, zaidi ya 200,000 wa Wilaya ya Busega waweze kupata maji kupitia mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninavyokwambia sasa Wilaya ya Busega wananchi wanaopata maji safi na salama ni asilimia 52 wengine bado hawapati maji safi na salama na kijiji cha mwisho ni kijiji chenye kilometra 42, leo tunazungumza kuleta maji Dodoma zaidi ya kilometra 800 tunaomba na sisi utukumbuke kwenye kilometra 42 nao waweze kupata maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja. Mheshimiwa Aweso karibu Usukmani, karibu Busega. Ahsante. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Vincent Mbogo, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwita Getere. Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga ajiandae.

MHE. VINCENT P. MBOGO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwanza nitampongeza kidogo sana Mheshimiwa Aweso kwa sababu, katika hotuba yake jimbo langu halijaguswa, limeguswa kidogo kuna ukakasi. Ma-engineer ndani ya Wilaya ya Nkansi wako wawili, tena ni *technicians*, engineer hakuna. Kwa hiyo, Wilaya ya Nkansi nzima suala la maji ni sifuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna ahadi alizotoa Mheshimiwa Hayati pamoja na Mheshimiwa Samia Suluhu. Katika mji mdogo ambao katika jimbo langu ndio mji ambao najisifia ultakiwa kuwe na mradi wa mabwawa ambayo yanaweza kuhudumia vijiji vitatu hadi vinne, lakini kwenye hotuba yake hayapo. Na hii nadhani kutokana na kwasababu, kule wilayani engineerwa maji hamna kwa hiyo, hapati taarifa sahihi. Kwa hiyo, nakuomba Mheshimiwa Aweso njoo uokoe Jimbo la Nkansi Kusini maji ni hoi, hakuna maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Nkansi Kusini nina kata tatu hawajawahi kuona maji ya bomba kila siku ni vifo vyaa mamba na magonjwa ya tumbo basi. Kwa hiyo, Mbunge nimebaki gari langu ndio *ambulance* kubebea watu kupeleka hospitali magonjwa ya tumbo na vifo vyaa mamba, wanaliwa na mamba. Mheshimiwa Aweso baada ya kumaliza Bunge nakuomba hairisha ziara nyingine zote za majimbo, Nkansi Kusini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu, nimeona Wabunge wengi wamechangia humu, kwanza nawashangaa, wengine matenki mabovu, wengine miundombinu chakavu, mimi hakuna miundombinu, hakuna matenki. Kwa hiyo, nakuomba baada ya Bunge mara ya kwanza Nkansi Kusini, ingia Ninde, ingia Kate, ingia Wampembe, utakuja na taarifa kamili. *Kule wananchi*

wanajihesabu kama wako Kongo. [Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma ya wananchi ya maji hawaajaifurahia nchi yao wanani pigia simu wanalamika wamesahafulika. Mheshimiwa Aweso, Wizara ya Maji, Nkansi Kusini anza nako kule ndio iwe kama *sample* nakuomba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vipo vijiji ambavyo viko mwambao kule mwa Ziwa Tanganyika hakuna miundombinu. Watu wanasema hapa wanakunywa maji na mifugo kule wanakunywa maji na nguruwe pori. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wanasema wana maji mekundu kule wana tope, wanatumia maji machafu, yaani ni shida Wilaya ya Nkansi Kusini. Mheshimiwa Aweso njoo ukomboe Nkansi Kusini upande wa maji, anza na mabwawa ambayo ni ahadi ya Mheshimiwa Rais, njoo uanze na visima. Nakushukuru umeweka visima kidogo, lakini bado asilimia ni ndogo mno. Ipo miradi iliyotelekezwa wameweka tu mabomba ya maji pale mipira hamna miaka, ukiuliza ina miaka nane, mengine mabomba yana miaka saba, yana miaka tisa, ni shida. Maliza bajeti yako Nkansi Kusini moja kwa moja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, yapo majimbo au vijiji ambavyo kama Mbunge wa Wilaya, naongea Wilaya ya Nkansi kwa ujumla kwasababu, ndio Mbunge wa Chama Cha Mapinduzi na ndio chama tawala ambacho naamini ndio kinacholeta maji, ndio kinacholeta huduma ya mabomba kila maeneo kwa Wilaya ya Nkansi jumla. Kwa hiyo, Mheshimiwa Aweso...

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Vincent Mbogo kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Aida Khenani.

MHE. VINCENT P. MBOGO: Mheshimiwa Naibu Spika, ndio naipokea Mbunge wangu pacha. (*Kicheko*)

NAIBU SPIKA: Ukae kwanza yeze azungumze. Ahsante. Mheshimiwa Aida Khenani.

TAARIFA

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpa Taarifa kaka yangu, pacha wangu anayetoka Nkansi Kusini kwamba, Wilaya ya Nkansi ina Majimbo mawili Nkansi Kusini anakochangia yeze ambako ndio anatoka, lakini Nkansi Kaskazini Mbunge wake aliyechaguliwa na wananchi anatoka Chama Cha Demokrasia na Maendeleo, CHADEMA. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Vincent Mbogo unaipokea Taarifa hiyo.

MHE. VINCENT P. MBOGO: Mheshimiwa Naibu Spika, siipokei kwasababu, hawana Serikali. Na hata huduma ninazoongea hizi kinacholeta ni Chama Cha Mapinduzi kwa hiyo... (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eeh, kengele imegonga?

MBUNGE FULANI: Bado.

MHE. VINCENT P. MBOGO: Mheshimiwa Naibu Spika, aah, naunga mkono hoja. Ahsante sana na Mbunge wangu pacha, asante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Asante sana. Taarifa iliwekwa kwa namna ya kuweka mambo sawasawa, lakini wakati ukizungumza Mheshimiwa Vincent Mbogo ulieleza zile kata tatu ambazo hazina miradi ya maji yoyote na ukasema kama wako Kongo. Sasa kwa sababu, ulikuwa unaeleza jambo ambalo wananchi wana hali mbaya nalo na haturuhusiwi kutumia michango ya nchi nytingine, unaweza kuitumia humu ndani ile ambayo inafanya vizuri unataka nchi yetu iige huko.

Lakini ile ya kuonesha kwamba, pengine kuna hali fulani hivi ambayo haiku sawasawa hairuhuswi. Kwa hiyo, ifute hiyo kama wako Kongo halafu tuendelee na mchangiaji mwininge.

MHE. VINCENT P. MBOGO: Mheshimiwa Naibu Spika, naifuta hiyo kauli, wako Tanzania. (*Makofi/Kicheko*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa, nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Mnyeti Alexander Pastory. Mheshimiwa Stanslaus Mabula ajiandae.

MHE. DEO K. SANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niungane na wenzangu kuweza kuchangia. Kwanza nianze kwa kumpongeza sana Waziri pamoja na Naibu Waziri na Katibu Mkuu na Manaibu pamoja na Wizara nzima kwa kazi nzuri wanayowatendea haki Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nimpongeze Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuwaamini hawa ambao wanawatendea Watanzania wanakwenda kwa kasi. Nawashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na miradi kadhaa ya maji katika Jimbo la Makambako. Nimeona kwenye bajeti wametutengea fedha, ombi langu Mheshimiwa Waziri na kundi lako, pale Ikelu pana mradi unaoendelea, mkandarasi yuko pale. Ombi langu tunaomba mkandarasi huyu kwasababu amesimama na yuko hatua za mwisho, mumlipe fedha ili aweze kumalizia mradi wananchi wa Ikelu waweze kupata maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile tuna mkandarasi yuko pale Ibatu. Mkandarasi huyu amesimama kwasababu hamjamlipa fedha. Tunaomba alipwe fedha ili kusudi aendelee kukamilisha ule mradi ili wananchi wa Ibatu waendelee kupata maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna mkandarasi yuko pale Usetule Mahongole, vilevile amesimama. Niombe sana Mheshimiwa Waziri na timu yako tuhakikishe tunawalipa ili wamalizie kwasababu, wamebaki hatua za mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mkandarasi wa mwisho yuko pale Nyamande, Mbugani na Mtulingala, Mkandarasi huyu anafanya kazi nzuri, lakini amesimama hawezি kuendelea kwasababu, hajalipwa fedha. Niombe sana aweze kulipwa fedha ili aweze kumalizia kazi iliyokusudiwa wananchi wale waweze kupata maji. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niungane na Wabunge wenzangu, tuna miradi ile ya miji 28. Katika miji 28 ikiwepo na Makambako. Na katika Makambako kuna kata tisa zinazotegemea mradi huu au miradi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba utakapokuwa unahitimisha hapa uwaambie wananchi wa Makambako ni namna gani wana imani kubwa ingawa katika maelezo yako umeeleza vizuri tumepata imani kwamba, mradi huu sasa unakwenda kutekelezwa. Sasa kwenye hitimisho hapa useme ili wananchi wa Makambako waweze kupona; wajue katika kata zao tisa wanazosubiri katika mradi huu mkubwa ni lini mkandarasi atakuwa katika Mji wa Makambako ili wananchi wa Makambako waweze kupata maji? Na wakati huo unapohitimisha na hii niliyoisema ya makandarasi waliosimama nayo useme hapa, ili wananchi wa Makambako wapate imani kama ambavyo ulituambia kwenye kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa leo nilitaka nizungumzie hili ambalo wakandarasi hawajalipwa na hii miradi ambayo ya miji 28. Watu wana imani kubwa sana ya miji hii 28 hasa ukiwepo na Mji wa Makambako ambao wananchi wanausubiri kwa hamu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, ahsante sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula, atafuatiwa na Mheshimiwa Selemani Kakoso. Mheshimiwa Dkt. Pallangyo ajiandae.

MHE. STANSLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Naibu Spika, na nitumie nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi walao niseme kidogo juu ya Wizara ya Maji kwasababu, ninaamini ili wananchi wetu waweze kufanikiwa kwenye mahitaji yao mengi wanahitaji maji safi salama na maji kwa wingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli kwamba, Wizara ya Maji imefanya kazi kubwa sana, sana kabisa, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri na timu yake nzima pamoja na Wizara kwa Ujumla, chini ya Katibu Mkuu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu muda wetu ni mchache sana na kwa hizi dakika tano niseme walao mambo matatu; la kwanza Mheshimiwa Kiswaga amezungumza ni vyema sana Wizara ikaendelea kutusaidia katika wakandarasi ambao tumeshawapata kwenye miradi yetu. Kwa mfano mradi wa chanzo kipyta cha maji pale Mwanza, mradi ambao ni mradi bora na utakaosaidia sana Jiji la Mwanza kupata maji. Mkandarasi inawezekana akakwama kwa sababu hajapata msamaha wa vifaa vinavyotoka nje ambako alikuwa anafanya kazi nyingine. Ninaamini mkandarasi akipata vifaa hivi kwa wakati tutakuwa tumepiga hatua kubwa sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili, ninaendelea sana kuishukuru Wizara kwasababu ya kazi kubwa iliyofanya. Tunao mradi unaoendelea huu wa chanzo kipyta cha maji na usambazaji wa bomba kutoka kule Lwanima kwenda Butimba kupitia Sawa kwenda Kanindo kwenda Igoma kwenda Kishiri utakaosaidia mpaka watu wa Buhongwa? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, liko tatizo na inawezekana sio la Wizara likawa linaunganisha na Wizara ya Fedha. Tunapompa mkandarasi kazi kuna kitu kinaitwa *GN – Government Note; Government Note* inatoka ya mwaka

mmoja-mmoja. Tunapotoa *Government Note* ya mwaka mmoja wakati mkandarasi ana mkataba wa miaka miwili au miaka miwili na nusu tafsiri yake ni kwamba, atakapokuwa ameanza ujenzi wa mradi ile *GN* unakuta imeshaisha muda wake analazimika kusubiri tena miezi mitatu mpaka miezi sita. Hii inafanya tunachelewesa sana wakandarasi tulio wapa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, na ili twende vizuri ninadhani Wizara ya Fedha ikubaliane na Serikali na Wizara ya Maji inapotoa *GN* itoe *GN* ya uhai wa mkataba, lakini ikiwa imeongeza miezi 12 itakayo isadia Wizara kumsimamia mkandarasi vizuri na kwa wakati. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na la tatu na la mwisho, ninafahamu Mji wetu wa Mwanza unakuwa kwa kasi. Mpaka sasa tunacho chanzo cha maji kinacho zalisha zaldi ya lita milioni 90. Mahitaji ya Jiji la Mwanza, Nyamagana, Illemela, Magu mpaka Misungwi ni zaidi ya lita milioni 160 na hizi milioni 90 tunazitumia sote kwenye hizi wilaya takribani tatu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe. Tunao mradi wa Mwanza *South* tunautegemea sana na sasa tuko kwenye hatua za mwisho. Wataalamu wanasema wanasubiri *no objection*, Serikali iongeze nguvu ili tupate huu mradi ambao sina shaka utasaidia sana kwenye maeneo mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatarajia tukipata fedha hizi tutajenga tenki la lita milioni sita kule Nyamazobe litakalowasaidia sana watu wa Malimbe, watu wa Luchelele, pamoja na Chuo Kikuu cha SAUT ambacho kiko Nayamagana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sio hiyo tu maeneo yote ya kwenda Igoma, maeneo yote ya Buhongwa. Maji haya yatakwendwa mpaka Kisese kule kwa Mheshimiwa Kiswaga, yatakwendwa mpaka kule kwa Mheshimiwa Pastory Mnyeti kule Usagara na kwa kufanya hivi yatakwendwa mpaka Illemela. Hapo tutakuwa tumekidhi walao mahitaji kwa asilimia 98 ya watu wa Mwanza. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini zaidi ya yote nikupongeze sana Mheshimiwa Aweso na msaidizi wako, ndugu katibu na timu nzima mnafanya kazi nzuri, mnakwenda kila mahali na kwa kweli mnaitembelea miradi yenu. Mungu awabariki sana na sina shaka kazi tuliyobakisha ni kusema ndio na shilingi yako mzee upambane kuhakikisha maji yanatufikia. Bwana awabariki sana, ahsanteni. (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Selemani Moshi Kakoso, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Pallangyo. Mheshimiwa Hamis Mwinjuma ajiandae.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Naibu Spika, nishukuru sana kunipa nafasi. Awali ya yote niishukuru sana Serikali kuititia kwa Waziri kwa kuleta miradi mikubwa na mingi kwenye jimbo langu, ninakushukuru sana Mheshimiwa Waziri. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kuzungumzia tunahitaji Mradi wa Ziwa Tanganyika. Katil ya maeneo ambako hatujatendewa haki na karibu Mikoa ya Kigoma, Katavi na Mkoa wa Rukwa hatujapata huduma ya maji safi na salama, lakini tukiwa tumeyaangalia. Ziwa Tanganyika ndio ziwa ambalo lina maji mengi, tena maji safi, kwa bahati mbaya sana wananchi wa mikoa hiyo hawajapata huduma ya maji kutokana na hilo ziwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nikuombe sana Mheshimiwa Waziri, nimeona kwenye kitabu tuna bilioni karibu 600 ndani ya mikoa hiyo mitatu. Niombe sasa Serikali ije na mpango mkakati kuhakikisha mikoa ambayo inazungukwa na hilo ziwa iweze kunufaika kupata mradi wa maji ya kutokana na ziwa Tanganyika. Mradi huu ukiyatoa maji Ziwa Tanganyika jimboni kwangu utanufaisha karibu vijiji kumi, Vijiji vya Ikola, Kapalambsenga, Karema, Kasangantongwe, Sibwesa, Kasekese, Ikaka, watanufaika na huu mradi, lakini utakuja kuwanufaisha sana wananchi wa Mkoa wa Katavi, Makao Makuu ya Mkoa pale Mpanda Mjini. Niombe Mheshimiwa Waziri hili ukalifanyie kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo jingine ambalo nina ombi ni mradi wa ukarabati wa visima kwenye eneo la Mishamo. Eneo hili lilikuwa ni eneo lilikuwa linahudumiwa na shirika la wakimbizi. Karibu miradi mingi iliyochimbwa visima vilivyokuwa vimechimbwa kwenye maeno hayo vilihudumiwa kwa muda mrefu na shirika hilo la wakimbizi na baadaye visima hivyo vikawa vimeharibika. Nimeona kwenye bajeti upo mpango mkakati wa kuvikarabati. Niiombe sana Serikali kuititia kwako Mheshimiwa Waziri tunahitaji sana ufufuaji wa hivyo visima viwasaidie wananchi. Karibu wananchi 60,000 wanaoishi kule huduma yao ya maji si nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini upo mradi wa maji ambaao tulishaiomba Serikali Kijiji cha Ifumbula, Kijiji cha Kapemba, Kijiji cha Mwazwe na Kijiji cha Rugufu. Tunaomba huu mradi muupelekee fedha ili uweze kuwanufaisha wananchi kwenye maeneo haya. Ni imani yangu Mheshimiwa Waziri kama mtapeleka huu mradi utasidia sana kutatua kero ya maji kwenye eneo la Mishamo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho tunaomba Mheshimiwa Waziri, tunajua jitihada ambazo unazifanya ni kubwa sana wewe na wataalamu wako na wasaidizi wako kwa ujumla. Miradi ya maji ina gharama kubwa sana ni vyema sasa Mheshimiwa Waziri uende ukaangalia, tuna miradi ambayo inaidhinishwa na Serikali ukiungalia fedha zinazotolewa na mradi unaokuwa umetekelizwa haviendani sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe sana Mheshimiwa Waziri hili uweze kulisimamia tunakuamini kwamba, umefanya kazi nzuri na ulishafika jimboni kwangu umefanya mikutano na umezindua miradi ya maji ambayo ilishatekelezwa. Lakini ni vizuri sasa mkaangalia mfumo wa utekelezaji kwa ajili ya miradi hii ambayo inachukua fedha nyingi. Mkiibana mnaweza mkapata nafasi ya kuweza kupunguza gharama na tukatekeleza miradi mikubwa mingi itakayowanufaisha wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kukushukuru Mheshimiwa Waziri. Yupo *Engineer* ambaye anafanya kazi kwenye halmashauri yangu amefanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, Naunga mkono hoja, ahsante. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Pallangyo, atafuatiwa na Mheshimiwa Hamis Mwinjuma. Mheshimiwa Kasalali Mageni ajiandae.

MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kuniona niweze kuchangia kidogo kwenye bajeti hii ya Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila kumung'unya maneno nitangulie kusema kwamba Serikali imefanya kazi nzuri sana kwenye sekta hii ya maji. Kwa hiyo, nichukue nafasi hii kumpongeza sana kwa kazi nzuri Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Watendaji wote pamoja na Wakuu wa Taasisi ambazo zipo chini wa Wizara hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wiki iliyopita nilipiga kelele kidogo kusema kwamba miundombinu ya maji kwenye Kata za Akeri imeharibika lakini nilipokuja kufungua hotuba ya Waziri nikakuta ametoa majibu, kuna mradi wa maji Patandi ambapo ndipo shinda ilikuwepo wa Sh.461,300,000 unajumlisha na Vijiji vya Patandi, Akeri, Kimundo, Ndoombo Nkoarisambu na Ndoombo Mfulony, tunasema ahsante sana kwa mradi huo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa maji Nshupu wenyе thamani ya shilingi 269,427,924 utatekelezwa, tunasema ahsante sana kwa Serikali. Mradi wa Maji Olmulo ambao unapitia Losinyai, Enoti, Milongoine, Orjoro, Mbuguni, Laroi, Terati, Kisima ya Mungu and Enjoro umetengewa kiasi cha shilingi 350,000,000, tunashukuru sana kwa mradi huo. Nikumbushe tu Mheshimiwa Waziri kwamba mradi huo utapita Mbuguni na Shambarai Burka msisahau kupeleka matawi kwa ajili ya wananchi wale.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mradi wa maji Mbaseni, Maji ya Chai, Kitefu wa thamani ya Sh.300,000,000, tunashukuru sana kwa kutukumbuka. Kuna mradi wa maji Kikwe, Nambala, Maweni na Karangai wa Sh.287,049,450, tunasema ahsante mno kwa kutukumbuka. Kuna mradi wa maji Kikatiti, Maroroni, Kitefu na Samaria umepewa Sh.287,049,430, tunashukuru Serikali kwa kutukumbuka. Mradi wa maji Sura, Ushiri, Poli, Kwaugoro, Valeska, Patanumbe, Makiba, Kisimili Juu, Msitu wa Mbogo umepewa Sh.50,000,000, tunashukuru sana kwa kutukumbuka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Iakini nitoe angalizo kwamba hivyo vijiji viliviyotajwa hapa viko mbali sana; Sura na Ushiri viko mlimani wakati Valeska na Patanumbe ni chini karibia na Mbuguni, sidhani kama hizi fedha zilizotengwa zitatosha, naomba waangalie namna ya kubadilisha. Pia kule Akeri kuna chanjo cha Kwa Saibala ambacho kimeharibika kinahitaji ukarabati na ndicho ambacho kinapeleka maji kwa watu wengi. Naomba chanzo hicho Wizara ikiangalie, watume *RUWASA* wakakikague, kikarabatiwe kwani sasa hivi kinatoa maji machafu na wakati mwingine hakuna maji kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia chanzo cha Makilenga, Mheshimiwa Waziri nadhani atakuwa anakumbuka alikuja akamfuta mtu kazi pale, kile chanzo ni cha kukarabatiwa. Sasa hivi kinatoa maji machafu yanahitaji kutibiwa ili kuondoa *fluoride* na wadudu hatarishi kwa maisha ya watu. Naomba mtukumbuke kwa hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kwenye hotuba ya Rais aliahidi kwamba kwenye Mpango wa Miaka Mitano ijayo tutaelekeza nguvu katika kuvuna maji ya mvua. Kule Shambrai Burka kuna korongo la Mto Nduruma, hii ni sehemu ya Mradi wa Maji wa Bonde la Mto Pangani. Korongo lile lilifukiwa katika harakati za kuendeleza mashamba kwenye miradi ambayo inaendelezw pale, baada ya kufukiwa kila msimu wa mvua maji yanaondoka kwenye korongo yanakwenda kwa wananchi yanaharibu mali zao na hata kuvunja nyumba zao na barabara zinakuwa zimejaa maji

zinakuwa kama mito. Tunaomba Wizara ifanye utaratibu ama wa kwenda kulichimbua lile Korongo au kujenga bwawa sehemu inaitwa Marurani ili yale maji yakija yasiende tena kusumbua wananchi yakawa laana yahifadhiwe na baadaye yatumike kwa ajili ya umwagiliaji na kwa matumizi ya binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasikia kengele imelia, nakushukuru sana kwa kuniona, nampongeza Waziri na timu yake, ahsanteni sana na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Hamis Mwinjuma, atafuatiwa na Mheshimiwa Kasalali Mageni, Mheshimiwa Anatropia ajiandae.

MHE. HAMIS M. WINJUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii na mimi nisema mawilli, matatu kwenye hoja iliyopo mezani. Nisije nikafika mwisho muda ukaribana ama nikajisahau niseme kwanza naunga mkono hoja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nichukue fursa hii kuwapongeza watendaji wetu kwenye Wizara ya Maji; Ndugu yangu Waziri Jumaa Hamidu Aweso na M-engineer wake, dada Naibu Waziri Maryprisca Mahundi, Katibu Mkuu Eng. Sanga (Mzee wa Mnadara), dada yangu Nadhifa Kemikimba, Mkurugenzi wa Tanga (UWASA), Eng. Upendo Rugongo, Meneja wa Tanga (UWASA – MUHEZA) Eng. Nyambuka na Meneja wa RUWASA - Muheza Eng. Cleophate Maharangata, kusema kweli mnatutende haki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua matatizo ya maji nchi hii ni makubwa na pengine ndio tatizo kubwa kuliko yote hasa kwa Wabunge wanaotoka Majimbo ya vijijini kama mimi. Mimi natoka Wilaya ya Muheza ambapo kuna changamoto kwenye kila kitu; elimu, afya, barabara na kadhalika. Akitokea mwananchi mwenzangu yejote wa Muheza hapa ukamuuliza tatizo la kwanza la Muheza ni nini, naamini atakutajia maji. Akina mama wa Muheza kuna mahali nilifika wakaniambia Mheshimiwa ukiweza kuhakikisha

tunaweza kuchota maji kwenye mabomba ikifika mwaka 2025 lete shati lako lisimame hapa wewe ukapumzike na tutalipigia kura. Kwa hiyo, ndugu yangu Mheshimiwa Jumaa na wasaidizi wako nafikiri mnajua kama mpaka Ubunge wangu mmeushika kwenye mikono yenu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kauli ya Kiswahili wanasema kwamba asiyeshukuru kwa kidogo hawezu kushukuru kwa kikubwa. Pamoja na tatizo kubwa la maji Wilaya ya Muheza kusema kweli watendaji hawa wanatusikiliza na wanapanga kuyatatuwa matatizo haya kwa moyo wao wote. Unaona hata maana ambapo hawawezi kulifanya kwa asilimia 100 lakini ndimi zao zinakuwa laini na unaona unawahangaisha katika kutafuta suluhisho ya matatizo yale. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Muheza tuna Mradi wa Kilongo ambao umetengewa kiasi cha shilingi milioni 778, tuna mradi wa Kwemdimu una shilingi milioni 649; mradi wa Kwemnyefu, Mdogo, Pongwe una shilingi bilioni 6.1 na ule mradi mkubwa kabisa ambao tunaamini unakwenda sasa kutatua tatizo zima la maji Wilaya ya Muheza wa miji 28 ambao sisi tumetengewa bilioni 40. Tunafahamu mioyo yenu ni mizuri na tunafahamu tatizo liko wapi, ni fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliombe Bunge lako Tukufu kama kuna kitu ambacho tunatakiwa kufanya kama Wabunge ni kuhakikisha Wizara ya Maji inapewa fedha zote ambazo tumekulaliana hapa. Kwa miaka 10 mfululizo ikiwemo bajeti yao ya mwaka huu wa fedha unaokwisha wamekuwa hawapewa hata asilimia 60 ya fedha ambazo wanaziomba, KKwa mfano, bajeti ya mwaka huu wa fedha wamepata asilimia 54 tu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ufahamu wangu, tunapoamua kwamba tunatenga fedha kwa ajli ya kwenda kutekeleza miradi ya maji tunakuwa tumeamua kwamba kuna asilimia fulani ya matatizo ya maji ya nchi hii tunakwenda kuyatatuwa siyo yote. Kwa hiyo, kama tumeamua kwamba tunatenga fedha na zinakwenda kutatua asilimia

20 ya matatizo ya maji katika nchi hii tunapowapa asilimia 50 maana yake tunakwenda kutatua asilimia 50 ya asilimia 20 ambayo tulipanga, tunazidi kujirudisha nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge tumeingia kwenye Bunge hili hasa Wabunge wa Vijijini kama mimi tukijua kwamba tatizo kubwa ni maji na kama hatutaikomalia Serikali iwe inatoa fedha zote ambazo zimeombwa na Wizara ya Maji ambazo zimepangwa kutekeleza miradi hii tutatoka hapa matatizo yale hayajakwisha. Sidhani kama hiyo ndiyo namna tunataka kukumbukwa, tumeingia tumekuta tatizo la maji, tutoke tuliache tatizo la maji. Naomba tulikomalie au kwa lugha ya mtaani tunasema kidedea Wabunge wote na ukiwemo Naibu Spika kuhakikisha kwamba Wizara ya Maji inapata sehemu kubwa ya fedha ilizoomba ili miradi hii ya maji iweze kutekelezwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nondo zilikuwa nydingi lakini nashukuru, naomba kuunga mkono hoja. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Kasalali Mageni, atafuatiwa na Mheshimiwa Anatropia Theonest tutamalizia na Mheshimiwa Anton Mwantona.

MHE. KASALALI E. MAGENI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikushukuru sana kwa nafasi hii. Kabla sijaongea sana niseme tu naunga mkono hoja. Pia nimpongeze ndugu yangu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Aweso na Naibu wake kwa kazi nzuri wanayoifanya kwenye sekta ya maji. Wanafanya kazi nzuri ya heshima na sisi hatuwezi kuwalipa kwa maneno yetu haya lakini Mwenyezi Mungu atawalipa vile wanavyostahili. Naomba waendelee kuchapa kazi na Mungu na Watanzania wanawaona. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wa Sumve wanalo jambo lao ambalo wameniomba nije nimwambie Mheshimiwa Waziri kuhusu mambo ya maji. Katika Jimbo la Sumve lililoko kwenye Wilaya ya Kwimba nadhani katika Mkoa wa Mwanza ambao ukilitaja Ziwa Victoria unaongelea Mkoa

wa Mwanza kwa kiasi kikubwa ni jimbo pekee ambalo halijui utamu wa maji ya bomba kutoka Ziwa Victoria. Mheshimiwa Naibu Waziri nkiangalia katika bajeti zilizopita kila mara mradi nafikiri namba 3403 ambaao unahusisha kupeleka maji ya bomba kutoka Ziwa Victoria katika Miji ya Sumve, Malya pamoja na Malampaka iliyoko kwenye Jimbo la Maswa Magharibi kwa Mheshimiwa Mashimba umekuwa unatajwa kila bajeti, unatengewa hii shilingi milioni 600 lakini haufanyiki. Mpaka umekutwa na miradi mingine, naanza kuona Busega ambaye ni mjukuu wa Kwindi tumemzaa sisi anapangiwa mabilioni ya fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Simiyu na Wilaya ya Kwindi hasa Jimbo la Sumve kijigrafia, hali ya hewa inafanana. Mradi huu wa Kuokoa Mazingira wa Simiyu, unapokwenda Simiyu unaiacha Sumve inakuwa sio sawa, watu wa Sumve tuna matatizo makubwa ya maji. Tunaomba mradi huu katika bajeti hii muweke fedha ambayo watu wa Sumve na sisi tutajiona ni sehemu ya Watanzania kwa sababu tupo kwenye Wilaya ya Kwindi lakini Jimbo la Kwindi lina maji ya bomba kutoka ziwa Victoria lakini Jimbo la Sumve hakuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri aliwahi kuja kwenye ziara Wiayani Kwindi nikamwombwa walau utengenezwe usanifu yale maji ya bomba katika tenki la lita milioni mbili waliloliweka kwenye Mji wa Ngudu yaende walau kwenye Kata za Lyoma, Malya, Wala ili kata zilizo karibu na mji wa Ngudu zipate maji kutoka Ziwa Victoria. Hata hivyo, naona bado usanifu ni wa kupeleka kata zilizo kwenye Jimbo la Kwindi lakini Jimbo la Sumve tumeachwa. Kwa niaba wa watu wa Sumve naomba kusema kwamba maji ya bomba kutoka Ziwa Victoria ndiyo yatatuokoa na matatizo ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Sumve hata uchimbaji wa visima wamekuwa wakichimba wanakosa maji chini. Tuna shida visima havijawahi kutusaidia kutatua tatizo hili. Tunapata visima vichache lakini na vyenyewe havijengewi mfumo wa maji ambaao utawafikia watu wote. Naomba katika jambo hili la maji kwenye Jimbo la Sumve

mtuangalie kwa jicho la pekee. Naunga mkono hoja kama nilivyosema lakini nahitaji sana tupate majibu yanayoeleweka hasa kwenye mradi wa maji ya bomba kutoka Ziwa Victoria kwenda kwenye Mji wa Malya, Sumve na Malampaka ambao uthalisha vijiji vingi vya Jimbo la Sumve na kuwa limepunguza tatizo la maji kwa kiasi kikubwa kwa watu wa Sumve. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jimbo la Sumve pia ipo miradi nimeona nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri miradi ya visima katika vijiji vya ...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Kengele imeshagonga Mheshimiwa.

MHE. KASALALI E. MAGENI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii. Nasisitiza maji ya bomba kutoka Ziwa Victoria kwenda Jimbo la Sumve hayaepukiki, naomba mtusaidie. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Anatropia Theonest tutamalizia na Mheshimiwa Anton Mwantona.

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nitaongelea maeneo matatu kama muda wangu ukiniruhusu. Kwanza, nitaongelea tathmini ya upatikanaji wa fedha lakini na uendelezaji wa habari ya maji. Pili, nitaongelea bajeti iliyoletwa kwenye Halmashauri ya Kyerwa lakini pia na tathimini ya CAG kuhusiana na utendaji lakini na mikataba mbalimbali ambayo imekuwa ikitekelezwa kwenye miradi ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, niseme bajeti imekuwa haiendi na haitoshi. Wabunge kadhaa wamesema utekelezaji wa bajeti ya maendeleo umekuwa ni asilimia 53 ambayo ni ndogo. Nisisahau kusema Mheshimiwa Waziri na Naibu wako mnafanya kazi nzuri sana lakini kazi mnayoifanya isipokuwa na fedha inakuwa ina matunda au tija ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mdogo tu ukiangalia kwa takwimu mlizoweka kwenye kitabu chenu mmesema katika mwaka wa wa fedha 2019/2020 mmeweza kuongeza tija katika upatikanaji wa maji vijijiini kwa asilimia 2.3 ina maana kutoka kwa asilimia 70.1 hadi asilimia *72 point something* ambayo naona kwamba ni tofauti ya asilimia 2 tu. Pia upatikanaji wa maji mjini kutoka asilimia 84 mpaka asilimia 86 unaona kwamba ni asilimia 2 tu. Kwa hiyo, kazi kubwa mnayofanya ni asilimia 2 tu bado ni ndogo sana. Hata hivyo, mngefanya nini kama hamna fedha au bajeti? Nadhani sasa ni kazi ya Serikali kuhakikisha kwamba inapeleka fedha ya kutosha, hata kama bajeti tunayotenga Bungeni ni ndogo basi iende lakini inavyokwenda kwa asilimia 52, 53 hata kutokee maajabu hakuna kitakachofanyika. Hiyo hoja yangu ya kwanza. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ya pili ambayo nataka niongelee, kuna msemo amesema Mhindi mmoja anaitwa Rajendra Singh amesema vita ya tatu ya dunia itatokana na kukosekana kwa maji na wanavyochangia Wabunge hapa inaonyesha Dhahiri. Vita siyo lazima ushike bunduki lakini ukiona kila sehemu kuna changamoto ya maji ujue tayari hiyo ni vita. Kwa hiyo, naomba sana Serikali itoe kipaumbele kuhakikisha kwamba fedha zinakwenda. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sio tu fedha kwenda na hiyo ninaingia kwenye sehemu yangu ya tatu, CAG ameinisha changamoto nyangi sana katika miradi ya maji, muda hautoshi ningeweza kuwaeleza. Kwa uchache mikataba haitekelezwi inavyostahili na fedha zinakwenda lakini hakuna usimamizi unaofaa. Naomba Mheshimiwa Waziri utupe majibu ya ripoti ya CAG alivyoeleza changamoto hasa kwenye masuala mazima ya *tendering* kwamba michakato inakuwa haiendi sawasawa ndiyo maana fedha inapotea na ndiyo maana hatuoni tija katika uwekezaji wa maji. Nitakuomba Mheshimiwa Waziri uweze kuongelea suala hili. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sio hiyo tu katika bajeti iliyopita mlipanga kutekeleza miradi 1,116 imetekelizwa

miradi takribani 355 ambayo ni sawasawa na asilimia 30 yaani kama tunaogelea pale pale. Hapa nirudi kwenye miradi sasa inayokuja kutekelezwa katika Halmashauri yangu ya Kyerwa. Nimekuwa nikieleza mara nyingi na Mheshimiwa Waziri nimekuwa nikikutumia picha za changamoto za maji za Kyerwa, tuna maji kwa asilimia 50 tu, zaidi ya watu asilimia 50 hawana maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Kyerwa tuna vyanzo vya maji vya kutosha na chanzo kikubwa cha maji ambapo nimewasikia wenzangu wanaongelea huko kwao Rukwa sisi kwetu tuna chanzo kikubwa cha maji ambacho ni Mto Kagera na kata zote zinazozunguka mto huu hazina maji. Nimeona mmeweka kwenye bajeti Kata za Mrongo, Bugomora, Kibale, Businde, Bugara zina changamoto ya maji lakini ni kata zinazopakana na Mto Kagera. Fedha iliyotengwa hapa, muda hautoshi ningeweza kusoma ni ndogo mtakuwa tu mnazibaziba tu viraka. Tunaomba utekelezaji wa mradi mkubwa wa maji tuweze kutibu changamoto ya maji Wilaya ya Kyerwa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sio hiyo tu watu wa Kyerwa hawatanielewa nisipoongelea changamoto ya Kata ya Kikukuru, kule tangu Uhuru hawajawahi kuona bomba la maji. Kata hiyo ina wakazi zaidi ya 17,000, kwa hiyo, ni kata kubwa sana ambapo lazima Serikali iweze kusikiliza na kupeleka miradi ya maji. Hata kama haina fedha za kutosha basi chimba visima *at least* kwa wakati huo ambapo tunasubiria miradi mikubwa watu waweze kupata maji. Bajeti ya shilingi bilioni 3 iliyotengwa kwa ajili ya Kyerwa nisema ukweli hiyo ni ndogo sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, muda wangu ni mchache lakini Kata ya Songambele pia ndiyo picha zile nilizokutumia, watu wanakunywa maji na ng'ombe. Kuna Kata ya Rwabwere sehemu inaitwa Mkijugwangoma hawajawahi kuona maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Anton Mwantona.

MHE. ANTON A. MWANTONA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata nafasi kuweza kuongea neno kidogo kwenye Wizara hii ya Maji. Pia namshukuru Mungu kwa kunipa uhai hadi siku ya leo napochangia katika Wizara hii. Nampongeza sana Waziri wa Maji mdogo wangu Mheshimiwa Aweso, Naibu Waziri wa Maji Mheshimiwa Maryprisca Mahundi, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote wa Wizara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, nimepitia bajeti ya Wizara ya Maji kwa kweli nimeona bajeti hii ni ndogo kwa Wizara hii. Mwaka huu wa fedha Wizara imepata shilingi bilioni 705 kwenye bajeti lakini kwa bahati mbaya sana fedha ambazo zimekuja kwenye Wizara ni bilioni 346 ambazo ni asilimia 53, ni fedha ndogo sana kwa Wizara. Tuombe Serikali ihakikishe kwamba fedha zinazopangwa kwenye bajeti zinapelekwa kama inavyotakiwa ili kumaliza kiu ya Watanzania kuhusu maji safi na salama kwa wananchi wake. Vinginevyo kila mwaka tutakuwa tunakuja kupiga kelele hapa kwamba bajeti ni ndogo, fedha haziendi na kwa sababu ya ufinyu wa bajeti ndio maana Wizara inashindwa kutekeleza malengo yake kama inavyotakiwa. Chonde chonde Serikali tunaomba tupeleke fedha kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia ninamshukuru Rais wetu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan alisema ataboresha Mfuko wa Maji nchini. Nimuombe Rais ahakikishe kwamba Mfuko wa Maji unapatiwa fedha ya kutosha ili changamoto za maji ziweze kuondoka hapa kwetu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nije Jimboni kwangu, namshukuru Waziri wa Maji pamoja na Naibu Waziri walipanga ziara kuja katika Jimbo la Rungwe wakatembelea miradi mbalimbali ikiwepo Mji wa Tukuyu, tukawaeleza matatizo yetu pale, mpaka leo *local radio* za pale Rungwe zimemnukuu Naibu Waziri akiahidi kwamba tatizo la maji

Tukuyu litakwisha, kila siku ndio salamu za asubuhi pale Rungwe. Nashukuru Waziri Mheshimiwa Jumaa Aweso pamoja na Naibu Waziri baada ya kusikia kilio cha wana Rungwe, Mji wa Tukuyu juzi juzi wamewapelekea shilingi milioni 500.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia alitembelea Mradi wa Rukata, Kata ya Kinyala, juzi juzi pia kawapelekea shilingi milioni 100 angalau mradi uanze wananchi wapate moyo. Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri ninawashukuru sana Mungu awaties nguvu katika utendaji kazi wenu ili miradi hii ya wananchi iweze kwenda vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi mwininge ambao napenda kuishukuru Wizara ni wa Masoko. Kuna mradi upo pale na kuna vijiji vingi vimenufaika. Kwenye bajeti hii kuna fedha kwenda kurekebisha madhaifu yalikuwepo kwenye mradi huu. Vijiji vitakavyofaidika nii zaidi ya 16 ambayo ni Ikama, Itagata, Lufumbi, Lupando, Bujesi, Lwifwa, Isabula, Mmbaka, Busisya, Burongwe, Ngaseke, Igembe, Mtandabara, Nsyasya, Mperwangwasi pamoja na Nsaga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli hivi vijiji vilikuwa na matatizo makubwa, chanzo cha maji kimetokea katika eneo lao lakini maji ya kutosheleza yalikuwa hayapatikani katika vijiji hivyo. Wizara imetenga zaidi ya shilingi milioni 500 kwenda kurekebisha miundombinu ili wananchi katika maeneo hayo waweze kupata maji ya uhakika, hiyo peke yake nashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Wizara imetenga fedha kwa ajili ya kupeleka maji kwa awamu ya pili katika mradi huu, vijiji 15 vinanufaika. Kuna Kijiji cha Mpumburi ambacho ni chanzo cha maji pia pale kinakwenda kupata maji. Vijiji vingine vyta Segera, Mpombo, Masukuru, Ijiga, Mpakanani, Byebe, Njugiro, Kiroba, Kikore, Matwebe, Kiambambembe, Lubanda, Katunduru na Ilima vinakwenda kupata maji. Hiyo ni shukrani ya pekee sana kwa Waziri lakini pia wa Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna vijiji vilikuwa kwenye bajeti ya mwaka huu ambayo inaisha mwezi wa sita, sijaviona kwenye bajeti inayofuata. Naomba chonde chonde tuna siku kadhaa kumaliza mwaka huu, mwaka unakwisha mwezi wa sita; kuna vijiji kama Champandapanda, Kata ya Kiwila mwaka huu unakwisha na ilitengewa shilingi milioni 205, kuna Kijiji cha Ikuti, Lyenje vilitengewa shilingi milioni 126, ni fedha ndogo, naomba Wizara kama kutakuwa na uwezekano kabla ya mwaka huu wa fedha haujaisha tuwapelekee hawa watu fedha ili miradi yao iweze kutekelezwa kwa sababu changamoto ni kubwa.

NAIBU SPIKA: Kengele imeshagongwa Mheshimiwa.

MHE. ANTON A. MWANTONA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano pale Lyenje pale Ikuti kuna kituo cha afya kimejengwa lakini kwa bahati mbaya sana hawana maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, naomba kuwasilisha. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha sehemu ya kwanza tutaendelea baadaye leo ambapo tutaanza na Meshimiwa Naibu Waziri halafu Waziri mwenye hoja atahitimisha hoja yake.

Baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 10.00 alasiri leo.

*(Saa 07.06 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 10.00 Jioni)
(Saa 10.00 jioni Bunge lilirejea)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tukae.

HOJA ZA SERIKALI

MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA MAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

(Majadiliano Yanaendelea)

NAIBU SPIKA: Tunaendelea. Nimwite Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa *Engineer Maryprisca Mahundi* achangie. (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe pamoja na Bunge lako Tukufu kwa kunipa fursa hii ili nami niweze kuchangia na kutoa ufanuzi wa baadhi ya hoja zilizotolewa wakati wa uwasilishaji wa bajeti ya Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee napenda kumshukuru Waziri wangu wa Maji Mheshimiwa Jumaa Hamidu Aweso, Mbunge kwa kuwasilisha kwa umahiri hoja ya Wizara yetu ya Maji kuhusu Mpango wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja iliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Maji imechangiwa na Wabunge wengi, tunashukuru sana Ni wazi kuwa muda niliopewa kikanuni hautanitosha kujibu hoja zote kwa ufasaha. Hivyo, katika muda huo mfupi, kwa kuzingatia wingi wa hoja, naomba njikite kwenye baadhi ya hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Mkoa wa Mtwara, napenda kusema kwamba Waheshimiwa Wabunge wote maelezo yote waliyoyatoa kutokana na matatizo ya maji katika Mkoa wa Mtwara, kwa uchache nichukue matamshi ya Mheshimiwa Tunza Malapo na Mheshimiwa Hokororo; waliongea kwa hisia kali sana kuhusiana na akina mama wa Mtwara kuchota maji ambayo wanasema ni maji ya kuokota. Wamekuwa wakitamka hivyo kwa sababu ni maji ambayo walikuwa wakiyatega nyakati za mvua na kuingia kwenye mashimo ambayo wanakuwa wameyaandaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiwa kama mama, suala hili limeniingia na kujisikia vibaya. Nitawajibika kwa nafasi yangu kuhakikisha tunaenda kutekeleza mikakati ya Wizara ambayo tumejiwekea hasa kwa kutumia Mto Ruvuma.

Chanzo hiki cha Mto Ruvuma naamini kitakuwa ni suluhi ya matatizo ya maji Mtwara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia mradi wa maji Ziwa Victoria kwa Mkao wa Simiyu. Mkao huu upo katika hatua za mwisho kupata huu mradi wa maji na tayari tuko kwenye hatua za kuweza kumpata Mhandisi Mshauri atakayefanya kazi ya usimamizi. Mara baada ya kupata Mhandisi Mshauri, kazi ya kumpata mkandarasi wa ujenzi pia itafanyika. Lengo ni kuona kwamba ujenzi wa mradi huu unakwenda kuanza mara moja. Tutafanya hivi kwa kuhakikisha tunasambaza maji maeneo yote ambayo bomba kuu litapita; kilomita 12 kulia na kilomita 12 kushoto kama sera inavyotutaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Mkao wa Songwe, napenda kuwapongeza Wabunge wote; Mheshimiwa George Mwenisongole, Mheshimiwa Shonza, Mheshimiwa Hasunga, Mheshimiwa Condester na Mheshimiwa Neema. Wote wamechangia kwa uchungu, namna ambavyo maji yamekuwa ni tatizo. Kwa Mkao wa Songwe tuna mradi mkubwa wa chanzo cha maji cha lleje; na yenyewe tunakwenda kushughulikia mwaka ujao wa fedha. Baada ya kushughulika na chanzo hiki cha lleje, tunaamini tunakwenda kutatua tatizo la maji Mkao wa Songwe katika Majimbo karibia yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kuhusiana na kufikisha maji katika taasisi zetu za Serikali kama vile mashule ama mahospitali na vituo vya afya, tayari Wizara ipo kwenye mchakato wa kuona tunafanya ushirikiano mzuri pamoja na Wizara ya Elimu na Wizara ya Afya ili kuhakikisha shule zetu zinapata maji na watoto wanapata maji katika mazingira rafiki. Lengo ni kuona tunakwenda kuondoa changamoto ya mimba za utotonii na vile vile kuhakikisha watoto nao wanafikia ndoto zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili tayari katika utekelezaji nimeshalifanya katika ziara zangu. Nilishakwenda Biharamulo na nikahakikisha nimeacha maagizo pale ya shule ya

sekondari kupata maji; Singida vilevile na pia katika Mkoa wa Mbeya nimetoa maagizo katika Sekondari ya Lyoto na yenyewe iweze kupatiwa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nimekuwa nikiongea mara nyingi, kwa sasa hivi Wizara ya Maji tuko katika mageuzi makubwa. Malalamiko haya ya Waheshimiwa Wabunge tunayasikia na sisi tukiwa kama sehemu ya jamii, tunayafahamu. Tukwenda kutekeleza miradi yote ambayo imekuwa ikisuasua kwa muda mrefu na tutahakikisha inakwenda kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi yote ambayo imekuwa ikiwasumbua wananchi katika maeneo mbalimbali kwa kutokukamilika, sasa hivi *RUWASA* imechukua nafasi. *RUWASA* imekuwa ni changa, bado tu ina mwaka mmoja lakin wameshafanya ufumbuzi wa miradi mbalimbali. Kwa hiyo, tutaendelea kutumia pia wanafunzi wetu ambao tunawapata kwenye Chuo chetu cha Maji na vile vile watumishi ambao wapo ndani, tayari na wao wameendelea kuchukua kasi ya Waziri wetu Mheshimiwa Jumaa Aweso, kwa sababu yeye wakati wote anahitaji kuona matokeo ya haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi watendaji wameshabadilika, wameshaachana na kufanya kazi kwa mazoea na sasa hivi wanafanya kazi vizuri. Wakurugenzi, Mameneja wa Mikoa na Wilaya tunawashukuru sana kwa sababu maagizo tunayowaachia tukiwa katika ziara zetu, yamekuwa yakifanyiwa kazi kwa karibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mikakati ambayo tumejiwekea kama Wizara ya kuhakikisha maeneo ya vijijini ambako maji hayajawahi kutoka bombani, sasa ndiyo wakati wa maji kutoka bombani. Tunataka tuhakikishe akina mama wanaachana na kazi ngumu ya kubeba maji vichwani, tunakwenda kumtua ndoo mwanamama kichwani. Hapa nina kila sababu ya kumpongeza na kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu, mama yetu mpandwa mama Samia Suluhu Hassan, katika hotuba yake ya matumaini makubwa

kwa Wizara ya Maji alipokuwa akihutubia Bunge lako Tukufu aliweza kutuhakikisha kwamba atakwenda kutuongezea fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukishapata fedha, ni usimamizi; sisi tuko tayari tutakesha, tutafanya kazi usiku na mchana. Lengo ni kuona kwamba tunahakikisha akina mama wanapata maji kwa umbali ambao ni rahisi kufikika na wanaachana na shughuli za kubeba ndoo vichwani na kupoteza muda mwangi. Tunafahamu kwamba ndoa nydingi zimekuwa zikivunjika kwa akina mama hawa kukesha huko kwenye visima, vilevile tunafahamu kuna akina mama waliopata hata ulemavu kwa sababu ya kupata vipigo vikali kutoka kwa waume zao. Sisi kama Wizara tumesema kwamba suluhu sasa ya akina mama kuondokana na dhoruba hizi zote inakwenda kupatikana mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Mkao wa Mbeya kuna mradi mkubwa wa kimkakati wa Kiwira. Huu utasambaza maji katika maeneo yote ya Jiji la Mbeya, maeneo ya Chunya kwa badaye, maeneo ya Rungwe Mbeya Vijijini na maeneo ya lleje pia yatajikuta yananufaika na mradi huu mkubwa. Huu mradi tutausimamia kwa karibu na tutaona kwamba kuanzia mwaka ujao wa fedha tumeshautengea fedha ya kutosha na tutakuwa tunautengea mara kwa mara. Lengo ni kuona kwamba unakwenda kukamilika ndani ya muda ambao unahitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kwa Mkao wa Mbeya kwa mji wa Tukuyu pale mjini, tayari tumeendelea kupeleka fedha. Hivi karibuni tumepeleka shilingi milioni 500. Lengo ni kuona kwamba tunaboresha maji katika Mji wa Tukuyu, lakini vilevile kusimamia fedha ambazo tunazipeleka kule wilayani na mikoani ili ziweze kufanya kazi na tutasimamia kuhakikisha thamani ya pesa inakwenda kuonekana katika utekelezaji wa miradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Mbeya pale mjini tumepeleka Ilunga *Project* ambayo itasaidia maeneo ya Iwambi mpaka Mbalizi. Kwa Chunya tutaangalia mradi wa

Matwiga ambao sasa umekuwa ni wa muda mrefu sana toka mwaka 2012, lakini toka baada ya RUWASA kuundwa mradi ule sasa unaelekea mwishoni, unakwenda kukamilika na vijiji 16 vinakwenda kunufaika. Yote haya ni katika kuona kwamba mageuzi ndani ya Wizara ya Maji yanakwenda kutekelezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuongea haya yote, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Sasa Waheshimiwa Wabunge nimwite mtoa hoja aje ahitimishe hoja yake. Waziri wa Maji, Mheshimiwa Jumaa Hamidu Aweso.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nikupongeze wewe binafsi kwa ushirikiano mkubwa ambao umetupa katika kipindi chetu chote cha hotuba hii ya bajeti, ahsante sana, Mungu akubariki sana. Kwa namna ya kipekee utufikishie salaam kwa Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mzee wetu Mheshimiwa Job Ndugai, tunamshukuru sana, amekuwa akitupa ushirikiano mkubwa sana sisi viongozi kuhakikisha kwamba tunatimiza wajibu wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee namshukuru sana Rais wetu mpendwa, Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan; Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mzee wangu Mheshimwia Isidori Mpango; pamoja na Waziri wetu, Mheshimiwa Mkuu Kassim Majaliwa Majaliwa kwa ushirikiano mkubwa na maelekezo yao katika kuhakikisha Watanzania wanapata huduma ya maji safi salama na yenye kutosheleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe ahadi kwenye Bunge hili Tukufu, mimi Jumaa Aweso pamoja na timu yangu ya Wizara ya Maji akiwemo Naibu Waziri wa Maji, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na timu nzima ya Wizara yetu ya Maji hatutakuwa kikwazo kwa Watanzania kupata maji safi salama na yenye kutosheleza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee, nitumie nafasi hii sana, sana, kulishukuru sana Bunge lako Tukufu; kiukweli michango ambayo imetolewa na Waheshimiwa Wabunge. Jana nilikuwa na Wahandisi wetu wa maji; kiukweli mawazo, hoja, maoni na ushauri ambao mmetupa sisi Wizara ya Maji Waheshimiwa Wabunge ni zaidi ya Wahandisi wetu wa Maji. Hongereni sana, Mungu awabariki sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nikiwa kama mwenye dhamana ya Wizara hii ya Maji, nimepata funzo kubwa na nitoe ahadi mbele yenu, tutafanya kazi kwa ushirikiano mkubwa kuhakikisha Watanzania wanaenda kupata maji safi salama na yenye kutosheleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee nimpongeze *Chief-Whip* wetu, mama yangu Mheshimiwa Mhagama ahsante sana, Mungu akubariki sana. Sisi wengine kwenye hizi nafasi bado ni wageni. Tumetoka shule, tumekuwa Wabunge, tumekuwa Manaibu na leo ni Mawaziri, lakini umetupa ujasiri. Ahsante sana, Mungu akubariki sana dada yetu, nasi tutaendelea kujituma kuhakikisha Watanzania wanapata huduma ya maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii tena kwa namna nyingine kulishukuru Bunge lako. Waheshimiwa Wabunge Zaidi ya 84 wameweza kuchangia katika bajeti yetu kwa kuzungumza. Pia tumepokea kwa maandishi mchangwa wa Mheshimiwa Mbunge Charles Mwijage. Itoshe kwamba hoja zote na maoni na ushauri, sisi kama Wizara ya Maji tumepokea na tutaenda kuyafanyia kazi yale ambayo Waheshimiwa Wabunge wametuelekeza katika Wizara yetu ya Maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba Waheshimiwa Wabunge kutokana na uchache wa muda, nizijibu hoja za baadhi ya Kamati pamoja na Waheshimiwa Wabunge na kuwakikishia kwamba hoja nyingine zote tutazijibu kwa maandishi. Itoshe kusema, namshukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti wetu, Mheshimiwa Christine Ishengoma pamoja

na Kamati yetu ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa namna ambavyo wamekuwa wakitupa ushirikiano sisi Wizara ya Maji katika kuhakikisha kwamba tunatimiza majukumu yetu. Ushauri wao mwingi ambao wametuelekeza juu ya kuanzishwa na kusimamia mpango mkakati wa kuhakikisha uvunaji wa maji ya mvua unakuwa endelevu kwa matumizi ya akiba, hasa na wakati wa kiangazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado wametuelekeza kutekeleza mpango wa ujenzi wa miundombinu wa maji taka katika miji na Makao Makuu ya Mikoa. Pia kuongeza kasi ya kutekeleza mipango na mikakati ya kuimarisha upatikanaji wa maji katika Jiji la Dodoma, itoshe tu kusema maoni ambayo mmetupa sisi tumeyapokea na tunayafanyia kazi katika kuhakikisha Watanzania wanapata huduma ya maji safi salama na yenye kutosheleza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu hoja za Waheshimiwa Wabunge. Moja ya hoja ambayo imezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wengi ni kuhusu suala zima la Ankara za maji. Naomba nizungumze hapa, ni haki ya mwananchi kupatiwa huduma ya maji, lakini mwananchi asisahau ana wajibu wa kulipia bili za maji. Sisi kama viongozi wa Wizara, jukumu letu ni kuhakikisha mwananchi hapewi bili bambikizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa kulizungumza, hata nami nilipopita maeneo mbalimbali nilizisikia hizo kelele. Nawapongeza katika hili kwa sababu anayelala na mgonjwa ndiye anayejua mihemo ya mgonjwa. Hongereni sana Waheshimiwa Wabunge kwa kujua changamoto za wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa ambaye anaidhinisha bili ni Taasisi yetu ya *EWURA*. Baada ya kusikia hizi changamoto, tumetoa maelekezo mahususi kwa *EWURA* juu ya kufuatilia bili hizi bambikizi. Wameshaifanya hiyo kazi na ripoti hivi karibuni watanikabidhi. Nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, mamlaka yoyote ambayo

imekwenda kinyume aidha kwa kuwabambikizia watu bili za maji, au kutoa bili ambazo hazijaidhinishwa na *EWURA*, tutazichukulia hatua hata wawe na mapembe marefu kiwango gani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nitoe maoni na ushauri kwa wananchi, pamoja na changamoto hizo, lakini zipo changamoto ambazo tumeziona sisi kama Wizara. Unakuta wakati mwingine mwananchi anatumia maji, bili anayopata ni ya gharama kubwa. Leo mwananchi anapiga mswaki, bomba amelifungua zaidi ya dakika tano; leo unakuta mvua mvua inanyesha, lakini anatumia maji yaliyokuwa *treated* anamwagilia maua; leo anatumia maji ambayo yamekuwa *treated* kufyatulia matofali. Tunaomba sana *EWURA* pamoja na mamlaka zetu za maji kutoa elimu kwa wananchi ili kuhakikisha kwamba mwananchi anaweza kuyafahamu hayo ili kuhakikisha kwamba anapata matumizi sahihi ya maji na aweze kupata bili zilizokuwa sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hili la bili za maji, maelekezo ambayo tumeyatoa sasa hivi Wizara, mamlaka zetu zote za maji tumeanzisha mfumo mpya ambao unaitwa *Unified bill system*, kwamba wajunge kuhakikisha tunakwenda kudhibiti ubambikizaji wa bili za maji. Hili ni sambamba na maelekezo ambayo tumeshayatoa; wasoma mita kuhakikisha kwamba hawawakadirii wananchi mita za maji. Katika kusoma huko mita za maji lazima wawashirikishe wananchi wetu ili kuhakikisha kwamba wanalipa bili halisia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa naomba niongeze, pamoja na suala zima la bili za maji, kumekuwa na tabia za mamlaka zetu za maji wakati mwingine kumkatia mwananchi maji kipindi cha sikuu au kipindi cha *week-end*. Sisi kama Wizara ya Maji tumepeiga marufuku; mamlaka zote za maji ni marufuku kumkatia maji mwananchi kipindi cha sikuu ama kipindi cha *week-end*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine katika kuhakikisha tunadhibiti bili hizo za maji, Waheshimiwa Wabunge sisi kama Wizara ya Maji tumetoa maelekezo mahususi kwa mamlaka

zetu za maji zote nchini; ni marufuku kwa mwananchi ye yote wa Tanzania kuhakikisha kwamba wanamlipisha *service charge*. Tumeshaifuta. Ikitokea Mkurugenzi au mtu ye yote ambaye anataka kumbambikizia mwananchi kwa maana katika bili yake amemwekea *service charge*, tutashughulika naye ipasavyo ili kuhakikisha kwamba tunamwokoa mwananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Naibu Spika, linguine limezungumziwa suala la dira za malipo ya kabla, kwa maana ya *prepaid meter*. Itoshe tu kusema kizuri huigwa. Tumeona wenzetu wa Wizara ya Nishati kuititia *TANESCO* wamekua wakitumia *meterza LUKU* na sisi kama Wizara ya Maji tumetoa maelekezo mahususi kwa Mamlaka zetu za Maji kuhakikisha wanafunga *prepaid meter* na tumeshaanza na tumeona faida hiyo. Leo tulikuwa tukipata makusanyo milioni 23 pale bandari, baada ya kufunga *Prepaid Meter DAWASA* wanakusanya zaidi ya milioni 103, hayo ndiyo manufaa makubwa kwetu sisi. Kwa hiyo, maelekezo ambayo tumetoa ni kwamba Mamlaka zote za Maji ambazo ziko katika daraja A kuhakikisha kwamba wanafunga *prepaid meter* ili kuhakikisha kwamba tunaondokana na hizi changamoto. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa awamu hii tunayokwenda nayo, naomba nitoe maelekezo mahususi kwa Waheshimiwa Wabunge wote waweze kufungiwa *prepaid meter* ili kama kutakuwa na changamoto yoyote muweze kutupa maoni na ushauri tuweze kuyafanyia kazi wakati tunaelekeea kwa wananchi wetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, imezungumzwa hapa changamoto ya gharama ya uunganishaji wa maji. Waheshimiwa Wabunge, sisi Wizara ya Maji jukumu letu ni kuhakikisha Mtanzania anapata maji, si maji tu ila ni kwa maana ya maji safi, salama na yenye kutosheleza lakini kwa gharama nafuu. Maelekezo ambayo ametupa Mheshimiwa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan ni kuhakikisha mwananchi anapatiwa maji bila ya gharama kubwa. Kwa hiyo sisi tumelipokea, tutakwenda kuliwekeea utaratibu mzuri, lakini

maelekezo ambayo tumewapa Mamlaka zetu za Maji kwa mwananchi ambaye anataka kuunganishwa maji kwa maana gharama inakuwa ni kubwa na yeye uwezo wake ni mdogo, maelekezo tuliyoyatoa wananchi hao walipe kwa awamu na zile gharama watalipia katika bili kama walivyokubaliana na Mamlaka zetu za Maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine Waheshimiwa Wabunge wametoa maoni mengi, Kamati yetu wametoa maoni mengi, juu ya kutumia vyanzo toshelevu tulivyokuwa navyo. Waheshimiwa Wabunge nao wameelekeza mambo mengi kwa maana ya maziwa na mito tuliyokuwa nayo. Itoshe kusema tu, nchi yetu ya Tanzania Mwenyezi Mungu ameibariki sana. Ina rasilimali za maji toshelevu juu ya ardhi na chini ya ardhi takribani mita za ujazo bilioni 126. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mita za ujazo bilioni 105 ni maji yaliyokuwa juu ardhi na mita za ujazo bilioni 21 ni maji yaliyokuwa chini ya ardhi na mahitaji yote ya Tanzania ni bilioni 60 tu. Kwa hiyo hatuna sababu hata moja kuona wananchi wetu wanateseka juu ya suala nzima la maji. Kwa hiyo, wataalam wa Wizara yetu ya Maji, lazima tubadili *mind set* zetu katika kuhakikisha tunatumia rasilimali toshelevu na Watanzania wanaweza kupata huduma ya maji safi, salama na ya kutosheleza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru sana maelekezo ya viongozi wetu, Mheshimiwa Makamu wa Rais pamoja na Waziri Mkuu sisi wasaidizi wao wametuelekeza namna ya kufanya uthubutu na tunaona namna viongozi wetu walivyofanya uthubutu mkubwa katika Taifa letu. Leo tunaona mambo ambayo yalikuwa hayawezekani, leo yanatekelezeka. Tunaona nchi yetu namna inavyojengwa *Standard Gauge*, kwa hiyo sisi kama Wizara ya Maji tumethubutu kwa kuanza ujenzi wa *Standard Gauge* kutoka Tabora, Igunga mpaka Nzega kwa kuyatoa maji kutoka Ziwa Victoria. Mradi ule umekamilika na Mheshimiwa Rais ametupa maelekezo mahususi maji yale yaliyofika Tabora tuyapeleke Kaliua, tuyapeleke Sikonge na mpaka Urambo kwa Mama Sitta ili kuhakikisha kwamba Watanzania

wanaenda kunifaika na huduma hii ya maji safi, salama na ya kutosheleza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kana kwamba haitoshi tunakwenda kuwatumia chanzo toshelevu cha Mto Ruvuma ili kuhakikisha wananchi wa Mtwara tunakwenda kutatua tatizo la maji pale Mtwara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukimwona mtu mzima analia ujuwe kuna jambo. Pamoja na Unaibu Spika wako lakini hukuacha kuja Wizara yetu ya maji kuomba tutumie Mto Kiwira ili wananchi wa Jimbo la Mbeya waweze kupata huduma ya maji. Nataka niwaambie wananchi wa Mbeya, sisi kama Wizara ya Maji si Wizara ya Ukame, tunakwenda kutumia Mto Kiwira ili kuhakikisha kwa wananchi wa Jiji la Mbeya tunakwenda kutatua tatizo la maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nzungumzie suala zima la miji 28. Kwanza nimshukuru Rais wetu, Mama Samia Suluhu Hassan, maelekezo mahususi ambayo ametoa katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni dhahiri, dhamira yake, nia yake ni kuona Watanzania wanapata huduma maji na safi na salama. Ameona wanawake wenzake namna gani walivyokuwa wakinyanyasika, wakiteseka juu ya maji.

Niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge mimi Juma Aweso pamoja leo ni Waziri wa Maji sikuwahi kuishi Masaki, nimetokea katika mazingira hayo ya maji ambayo akinamama walikuwa wanapata tabu. Nimewona mama yangu mzazi wakati akimuacha baba yangu amelala badala ya kumpetipeti yeye anaenda kutafuta maji. (*Makofi/ Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge mimi Juma Aweso uchungu wa mama ambao mnaupata naufahamu, tutafanya kazi usiku na mchana kuhakikisha Watanzania wanapata huduma ya maji safi, salama na ya kutosheleza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mahusiano mazuri ya nchi yetu na Rais wetu, tumepeata fedha dola milioni 500 kwa ajili ya kuhakikisha Watanzania katika miji 28 wanakwenda kupata huduma ya maji safi, salama na ya kutosheleza. Hapa niwe muwazi zaidi, Wizara yetu ya Maji ilikuwa ikilalamikiwa sana, moja kutumia miradi kwa gharama kubwa. Utekelezaji wa miradi hii ya miji 28 *financial agreement* ilikuwa kwa ajili ya kutekeleza maji katika miji 16. Sisi kama viongozi wa Wizara ya Maji tukasema hapana, lazima tutazame *design* ya mradi huu juu ya utekelezaji wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuja kugundua kwamba, eneo ambalo leo linahitaji pampu tatu wanaweka pampu 11, tumezikata, tukasema ili hapana. Eneo ambalo wangeweza kuweka bomba la milimita 300 wanaweka millimita 900, tukasema hapana, fedha hizi ambazo zingeweza kutatua maeneo mengine tumezibana badala ya miji 16 tunakwenda kutekeleza miji 28. Waheshimiwa Wabunge tunaomba mtuamini katika kuhakikisha kwamba tunatekeleza miradi hiyo na Watanzania waweze kupata huduma ya maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi tuko katika hatua ya mwisho na nataka niwaambie ukiona giza linatanda ujue kumekucha. Huu ni mradi wa muda mrefu sana, lakini sasa hivi tumeshakamilisha hatua za manunuzi, tuko katika utaratibu wa kupata kibali *Exim*, wakandarasi waende *site*, maelekezo mahususi ambayo nimeyatoa kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji na watendaji wote, *signing* ya wakandarasi zote zitafanyika katika majimbo yenu katika kuhakikisha wananchi wanaenda kufaidika na huu mradi wa maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wimbo mbaya haimbiwi mwana; sisi nikubali kama Waziri wa Maji, Wizara ya Maji ilichezewa sana na niwashukuru sana watangulizi wangu Mheshimiwa Kamwelwe, Profesa Kitila Mkumbo pamoja na Profesa Makame Mbarawa, tumefanya mageuzi makubwa sana katika Wizara yetu ya Maji. Tulikuwa tukifanya ziara,

niliwahi kufika pale Njombe kuna Kijiji kinaitwa Ukarao, nipo na Mhandisi wa Maji unamuuliza kwa nini wananchi hapa hawapati maji? Anakwambia tatizo ni *design*, kama tatizo ni *design* mbona eneo la Njombe lina baridi, mbona wewe umeweka *solar*? Anasema Mheshimiwa nimeghafirika, naomba uniokoe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, achana na hilo, nilikwenda Mwakitolio, Shinyanga Vijiji, mradi wa bilioni 1.4, fedha imetolewa lakini wananchi hawapati maji, unamuuliza Mhandisi wa Maji, wewe hapa pesa imetolewa kwanini wananchi hawapati maji? Ananiambia Mheshimiwa Waziri naomba nikunong'oneze. Namwambia hapana kuninong'oneza, waambie wananchi kwa nini hawapati huduma ya maji, sijawahi kuona wananchi wachawi kama kijiji hiki, usiku mabomba yanapaa. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mageuzi ya Wizara yetu hatuwezi kuwa na Wahandisi wababaishaji wa namna hii, mageuzi tuliyofanya, Wahandisi 118 tumekwishaachana nao katika Wizara yetu ya Maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, achana na hilo, moja ya vitu ambavyo vilikuwa vinaathiri Wizara ya Maji ni uitiri wa wakandarasi ambao hawana uwezo. Watu walikua wakipewa kazi kishemeji shemeji, kiujomba ujomba, zaidi ya makandarasi 59 tumeshaachana nao na majina yao tumeyapeleka katika Bodi ya Wakandarasi waweze kuchukuliwa hatua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo ambalo nataka kusema katika Wizara yetu ya Maji, ukicheka na nyenyere ambaye anakutambalia kwenye mapaja atakung'ata pabaya, mimi siko tayari kung'atwa. Tutawashughulikia makandarasi wote ambao watataka kuikwamisha Wizara yetu ya Maji ili kuhakikisha kwamba Watanzania wanapata huduma ya maji safi salama na yenye kutosheleza. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Wizara ya Maji pamoja na timu nzima hatutacheka na mkandarasi, sisi Wizara ya Maji hatutacheka na Mhandisi yeyote wa Maji, sisi tutacheka kwa kuona maji yanapatikana katika mabomba, huo ndiyo msimamo wetu. Kwa hiyo, nishawahi kusema kwamba vipo vya kuchezea, ukishiba chezea kidevu chako au kitambi si miradi ya maji, tutashughulikiana ipasavyo. (*Makofi/ Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mageuzi hayo, tumefanya *plot* kwa nini miradi ya maji itumie gharama kubwa. Tumeweza kutengeneza miradi 192 ambayo *engineering estimation* yake ilikuwa bilioni 207, lakini kutumia wataalam wetu wa ndani tumetekeleza kwa bilioni 163 na bilioni 44 tumeweza kuziokoa. (*Makofi/ Vigelegele*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo ukienda Matamba Kinyika pale Njombe, mradi wa *engineering estimation* iliyoletwa ilikuwa bilioni 6.6, lakini sisi tukasema hapana, mradi huu tutatumia wataalam wetu wa ndani tuone, mradi hule vijiji tisa tumeukamilisha kwa bilioni 1.5, wananchi wanapata huduma ya maji safi na salama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa tuna mradi pale Sumbawanga Vijiji, Muze *Group*, mradi huu ni wa vijiji 10, lakini ulitakiwa kutekelezwa kwa bilioni 6.7, tukasema hapana, wataalam unapokuwa Mhandisi wa Maji kwa maana una taaluma ya kutengeza miradi ya maji, hii kazi mnaiweza na hamjashindwa ifanyeni. Sasa hivi vijiji 10 vimekamilika, wananchi wanapata huduma ya maji, bilioni 2 hazijaisha lakini wananchi wale wameanza kupata huduma ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo msimamo sisi Wizara tuliuweka, wakandarasi wababaishaji hawana nafasi, kwa hiyo hatuwezi kufanya kazi zote kwa *force account*, lakini tulichokifanya sisi kama Wizara ya Maji, tume-*shortlist* wakandarasi ambao wamefanya kazi nzuri katika Wizara ya Maji wale ndiyo tutakwenda nao kuwapa kazi kuhakikisha kwamba tunakwenda kutatua changamoto ya maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tumekwenda mbali, tulikuwa tukifanya ziara katika wilaya na mikoa, unakuta wilaya moja *tank design* moja, lakini gharama tofauti. Tukasema hapana sisi tumeanzisha *design manual*, kesho Waziri Mkuu anakutana na Wahandisi wote wa Maji Nchini, atakwenda kuwakabidhi hizi ili kuhakikisha kwamba Wahandisi wa Maji wanakwenda kutekeleza miradi kwa kufuata *designs* hizi ili kuhakikisha kwamba Watanzania tunakwenda kuwatekeleza miradi bora, yenye uwezo mzuri na ambayo itadumu kwa muda mrefu kuhakikisha Watanzania wanapata huduma maji safi na salama na yenye kutosheleza. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ndugu zangu ni kuhusu suala nzima la ufuatilajji wa miradi ya maji. Tulikuwa tukipita wakati mwingine Mhandisi au *Technician* anaweza akakwambia vituo vinatoa maji lakini havitoi, kumbe anashindwa kufuatilia kwa sababu ya changamoto ya usafiri. Kwa kipindi kifupi kwa mageuzi ambayo tumeyafanya, kesho Waziri Mkuu anakwenda kukabidhi pikipiki 145 ili kuhakikisha *Technicians* wetu hawakai ofisini na kuchezza *computer*, waende wakafie kwenye matanki ya maji kuhakikisha Watanzania wanapata huduma ya maji. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na pikipiki hizo magari yanakuja hivi karibuni zaidi ya 22 ili kuhakikisha maeneo ambayo hayana vifaa hivi waweze kupatiwa ili waweze kupata huduma ya maji safi na salama. (*Makof*/*Vigelegele*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine lililokuwa linatuathiri sisi kama Wizara ni muundo wa Wizara, leo Mhandisi tuna Wizara ya Maji lakini Mhandisi yuko *TAMISEMI*. Tumeona changamoto juu ya utumishi na hata kuitendaji katika kumchukulia hatua. Waheshimiwa Wabunge hili lilionekana Mheshimiwa Rais alitoa maelekezo kwa maana Wahandisi wa Maji wote waje chini ya Wizara yetu ya Maji. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, achana na hilo, kwa dhamira ya dhati ya kuhakikisha kwamba tunakwenda kutatua tatizo la maji, tulileta hapa Muswada wa Sheria na Wabunge wakaupitisha juu ya uazishwaji wa Wakala Maji Vijijini. Sasa hivi ni mwaka mmoja *RUWASA* amezaliwa kama ndama, amezaliwa anakwenda, leo tumekutana na miradi kichefukichefu zaidi ya 177 ambayo tumei-/ist mpaka sasa hivi mwaka mmoja, zaidi miradi 85 tumeshaikwamua kupitia *RUWASA*. Mkakati wetu wa Wizara ya Maji kuhakikisha miradi yote ambayo haijakamilika kuhakikisha tunaikamilisha kwa wakati na Watanzania waweze kupata huduma maji safi, salama na yenye kutosheleza. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kuapatia maji ni vita, hatuwezi kukubali kuona kwamba hapa imeliwa milioni 100, hapa imeliwa 150, sisi ni viongozi na hii ni nchi yetu, maji ni uhai, maji hayana mbadala, maji si kama wali ukikosa wali utakula ugali ukikosa ugali utakula makande, ukikosa maji tu utapata maradhi. Kwa hiyo nii ni vita yetu sote na wala msiongope Waheshimiwa Wabunge, baba wa Taifa mwaka 1978 na 1979 wakati anakwenda kumtoa Nduli Iddi Amini alisema maneno yafuatayo: “*Nia tunayo, uwezo tunao na sababu tunao*”.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwezo wa kukabiliana na makandarasi wababaishaji tunao, kwa kushirikiana wote Waheshimiwa Wabunge. Niwaombe muwe mabalozi na maelekezo ambayo nimeyaelekeza Wahandisi wetu wa Maji hakuna siri, kama unatekeleza mradi Ludewa kwa nini usiwaeleze Baraza la Madiwani, kama unatekeleza mradi Ludewa kwa nini usimwambie Mheshimiwa Mbunge. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kanuni na Sheria, zipo janjajanja zilizokuwa zinafanywa na Wahandisi wetu, baadhi unamwambia kwa nini ulete taarifa kwenye baraza? Anakwambia sasa hivi hatujajibiki huko. Tumeianzisha *RUWASA*, hatujaanzisha *RUWASA* kwa maana taasisi iishi mbinguni, tumeianzisha kwa ajili ya kutatua matatizo ya watu, lazima washirikiane na viongozi katika maeneo husika. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nimekwishazungumza na Mheshimiwa Ummy dada yangu kuhakikisha kwamba tunashirikiana na Wizara ya TAMISEMI na Ofisi ya Mazingira kuhakikisha tunasimamia tunafuatilia kwa pamoja ili kuhakikisha kwamba Watanzania waishio vijiji wanapata huduma majisafi salama na yenye kutosheleza. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha kwamba tunaongeza nguvu mikoani na kukwamua miradi mingi kwa wakati na Watanzania waweze kupata huduma ya maji, tumeweza kuanzisha timu mikoani *Water Rescue Team*. Hapa tumeangalia kada tofauti tofauti ipo changamoto ya *design*, tumeweza wataalam wa *design*; kama kuna changamoto ya suala la manunuzi, kuna wataalam wa manunuzi; na kama suala la tafiti la maji, kuna mtu wa tafiti za maji. Kwa hiyo haya tumeyazingatia na tumeanza kutekeleza na tumeona miradi mbalimbali tunavyoikwamua kwa wakati na hii imetusaidia pia kubadili *mind set* za watu wetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *mind set* za Wahandisi wetu wa Maji wakati fulani zilikua zinatuchelewesha. Kwa mfano, Serikali unaweza ukakuta imewekeza fedha nyingi Bukoba, Dar es Salaam, Mwanza na Tabora, lakini leo hata mtu akitaka kutengeneza mtandao wa mita kumi anakuja kuomba fedha katika Wizara, tumesema hapana. Leo tumeona DAWASA makusanyo yao walikuwa wakikusanya bilioni saba sasa hivi wanakusanya bilioni 13 na fedha zile wameweza kutekeleza miradi. Wameweza kutekeleza mradi wa bilioni 10 Kisarawe kwa kutumia pesa zao za ndani, wameweza kutekeleza mradi wa maji Kigamboni kwa bilioni 25 kupitia fedha zao za ndani. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka niwaambie Wakurugenzi wote wa Mamlaka za Maji ukibebwa na wewe basi hebu usijiachie, kuhakikisha kwamba tunatatua changamoto maji. Kwa yejote ambaye atashindwa, atatupisha ili kuhakikisha kwamba tunaenda kuwapatia Watanzania huduma ya maji safi, salama na yenye kutosheleza. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, limezungumzwa hapa suala la uvujaji wa maji. Si busara hata kidogo kuona Serikali imewekeza fedha nyingi katika miradi ya maji lakini unapita mtaani maji yanamwangika ili hali wananchi wengine hawana maji. Niliwahi kufanya ziara katika baadhi ya Mamlaka, unapewa taarifa, Mkurugenzi wa Maji anakwambia hapa upotevu wa maji ni asilimia 46. Mtu anapokwambia upotevu wa maji asilimia 46 lazima uhoji, mimi nategemea unaponiambia upotevu wa maji asilimia 46 nikipita mtaani niyaone mabwawa ya samaki au nione mafuriko. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu ambacho nilichokigundua, kuna wizi mkubwa sana wa maji. Nilifanya ziara Morogoro pale, wamenipa taarifa lakini nikajiridhisha kulala, tumeenda kukikamata kiwanda kinaiba maji bila utaratibu wowote, tumebanana nao zaidi ya milioni 250 wamezilipa.

Kwa hiyo, nimeshawaita Wakurugenzi wa Mamlaka zetu za Maji na nimewapa maelezo mahususi; moja kudhibiti huu wizi na huu wizi wakati mwingine hata baadhi ya watumishi wetu wanashiriki. Kwa hiyo kikubwa hawa watu tutawachukulia hatua na hii ni vita yetu sote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni juu ya upashanaji wa habari, leo mwananchi anaweza akaona maji yanavuja, anatoa taarifa kwenye mamlaka husika *hawa-respond*, lakini mwananchi huyo huyo anajiunga bando anamatumia Waziri, Waziri ukitumia katika mamlaka hiyo hiyo, utaona wanapiga picha Mheshimiwa tumeenda hata kama usiku tumeshakwamua.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelekezo ambayo tumewapa Wakurugenzi wa Mamlaka zetu za Maji utaratibu wa haraka ambao wanaufanya kama tunavyowatuma sisi viongozi, waende wakafanye pale mwananchi anapowapa taarifa, kwa sababu wananchi ndiyo mabosi wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kulishukuru Bunge, lakini tumepata maoni mazuri sana. Ninachotaka kukisema, mvua katika nchi yetu ya Tanzania isiwe laana, iwe fursa, kwa maana ya kuhakikisha kwamba tunatengeneza miundombinu ambayo tunaweza tukavuna maji lakini tunaweza kujenga mabwawa yatakayoweza kutumika katika maeneo yenye ukame ambayo hayana maji, yaende kupatiwa huduma ya maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo niendelee kumpongeza sana Naibu wangu Waziri wa Maji ili ni jembe wembe amefanya kazi kubwa sana na namna anavyojituma, Waziri wako nitakupa ushirikiano mkubwa sana. Lakini kwa namna ya kipekee nimshukuru sana katibu wangu Mkuu *Engineer Athony Sanga* pamoja na Naibu Katibu Mkuu mama *Engineer Sediki kamikimba* katika kuhakikisha kwamba watanzania wanapata huduma ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tumejipanga leo Katibu Mkuu akiwa Ruvuma mimii nipo Songea yeye akiwa Ruvuma mimi zangu Mbeya Naibu Waziri akiwa Kilimanjaro Naibu Katibu Mkuu yupo zake Mtwara yote ni katika kuhakikisha tunasimamia na tunafuatailia miradi yetu ya maji na watanzani wanaweza kupata huduma maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maendeleo ya sekta ya maji Waheshimiwa Wabunge yanaanza na mimi maendeleo ya sekta ya maji Waheshimiwa Wabunge yanaanza na wewe, maendeleo ya sekta ya maji yanaanza na sisi sote kwa kushikamana ahsante sana mungu awabariki sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.
(*Makofi/Vigelegele*)

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono japo kuwa nawaona Wabunge ambao wanalamika sana maeneo yao wametiwa matumaini hapa na bado wamekaa kwenye kuunga mkono hoja. Lakini hoja imeungwa mkono tutaendelea na utaratibu wetu katibu.

NDG. MOSSY LUKUVI- KATIBU MEZANI:

KAMATI YA MATUMIZI

KITABU CHA PILI

MATUMIZI YA KAWAIDA

MWENYEKITI: Waheshimiwa tukae. Katibu!

NDG. ASIA MINJA - KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaanza na kitabu cha pili matumizi ya kawaida ukurasa 324.

FUNGU 49 - WIZARA YA MAJI

Kifungu 1001- *Administration and Human Resource Management*.... Sh. 3,773,171,693

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge kifungu hiki ndicho chenye mshahara wa Waziri na kwa mujibu wa kanuni zetu hapa ninayo majina ya Wabunge mbalimbali ambao wanataka ufanuzi ya mambo ya kisera tutaanza na Mheshimiwa Cosato David Chumi.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti nashukuru kwa kunipa nafasi na pia napenda kutumia nafasi hii kuishukuru Serikali na kuipongeza katika mradi wa miji 28 kama aliyosema Mheshimiwa Waziri awali ilikuwa iwe miji 16 17 lakini baadaye *review ikafanyika ikawa miji 28*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo mazuri ya Mheshimiwa waziri, ninapenda nimsikie na wananchi wa Mafinga na miji 28 wasikie mradi huu unaanza lini kwasababu tunazungumza hapa nadhani ni mwaka kama wa nne kila

bajeti kila maswali na majibu ni miji 28 miji 28 na katika miji 28 Mafinga ikiwepo.

Waziri atuambie na Taifa lisikie yani lini kabisa wakandarasi wapo *sige* imekuwa ni habari ambayo kwa kweli hata wananchi tunashindwa la kuwaambia naomba kuwasilisha. Na ikiwa maelezo hayajitoshelezi nitaombwa kuungwa mkono tupate kujadili kwa kushika shilingi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Maji ufanuzi.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, hata sisi ili jambo limetutesa sana lakini kama nilivyo sema kwamba dhamira ya Rais wetu mama Samia Suluhu Hassan kuhakikisha watanzania wanapata huduma ya maji na huu mradi ulikuwa miji 16 tungeweza kuutekeleza lakini tukasema hapana hizi ni pesa nyingi ambazo zingeweza kuhudumia maeneo ambayo watu wana changamoto ya maji waweze kupatiwa huduma ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kaka yangu Casato Chumi na nataka wananchi wa Mafinga wanisikie mradi huu tunakwenda kutekeleza kabla ya mwezi huu wa juni kuisha kuhakikisha wananchi wakandarasi wanakuwa saiti ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge naona Mheshimiwa David Casato Chumi amekaa kwa hiyo amelizika. Nimuite sasa Mheshimiwa Ritta Kabati lakini niwakumbusha Waheshimiwa Wabunge tunapozungumzia kwenye kifungu hiki cha mshahara wa Waziri ni mambo ya sera mambo ya jumla si mambo ya jimbo moja. Mheshimiwa Ritta Kabati.

MHE. DKT. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Naibu Spika ahsante sana kwa kunipatia nafasi niweze kuomba ufanuzi kuhusiana na masuala ya maji, kwanza na nianze sana kumpongeza Mheshimiwa Waziri Naibu Waziri MaryPrisca na viongozi wote walioko katika Wizara hii ya maji kwa

kuhakikisha kwamba tunaanza sasa kuondoa changamoto ya maji katika miji yetu yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona kwamba ziwa Victoria limekuwa mtatuzi wa maji wa miji 28 hiyo ambayo itapatiwa maji kulingana na mkakati wa Serikali. Nilikuwa nataka kuuliza je, nini mkakati wa Serikali kuhusiana na nyanda za juu kusini kwamba tunayo na sisi maziwa tunayo ziwa Tanganyika, Ziwa Rukwa, Ziwa Nyasa ambayo tunategemea kama kutakuwa na mkakati pengine sasa Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini inaweza ikaondoa kabisa tatizo la maji nikiomba Mheshimiwa Waziri sasa atupatie ufanuzi ahsante Mheshimiwa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Maji ufanuzi.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpogeze Mheshimiwa Mbunge lakini kubwa ambalo ninalotaka kusema maelekezo mahususi kwa viongozi wetu wakuu akiwemo Mheshimiwa Rais, mama Samia Suluhu Hassan, ni kuhakikisha tunatumia rasilimali zetu toshelezi tulizokuwa nazo. Na nchi yetu ya Tanzania tuna rasilimali za maji juu ya ardhi na chini ya ardhi mita za ujazo bilioni 126, bilioni 105 juu ya ardhi na bilioni 21 chini ya ardhi hatuna sababu tena ya kulalamika juu ya suala zima la maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mkakati ni wa wizara yetu ya maji na hata katika bajeti yetu ni kuhakikisha tunatumia rasilimali hizi toshelevu kwa maana ya kuwa na *standard gauge* ya miradi yetu ya maji na tumeanza kuyatoa maji ziwa Victoria kuyapeleka Tabora, Igunga mpaka Nzega.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tumehainisha maziwa ya ziwa Tanganyika sasa hivi tumepeleka maji Kigoma, lakini mkakati wetu maeneo ya Katavi kutumia ziwa Tanganyika kuhakikisha wananchi wa Katavi wanapata huduma ya maji, lakini pia Ziwa Nyasa ili kuhakikisha kwamba wananchi wa Ruvuma nao wanaenda kunufaika na maji pamoa na Mkoa wa Njombe. Kwa hiyo, sasa hivi tupo katika

hatua ya kumpata mwandisi mshauri na tunafanya tathimini takribani vijiji 413 vitaenda kunufaika kutokana na rasilimali hizi za maji zilizokuwepo ahsanteni sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Ester Amos Bulaya,

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na mimi nihitaji ufanuzi na nisiporidhika nitatoa shilingi. Nimemsikia Waziri kwenye majibu yake katika suala zima la upotevu wa maji, ameungumizia katika upande wa kujunganishia maji na hakataja milioni 200 lakini suala la upotevu wa maji kwenye ripoti ya *CAG* ya miaka yote tangu ukiwa Naibu Waziri mpaka leo Waziri imekuwa ikisemwa kila siku na hakuna mkakati wowote wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ukiangalia tangu mwaka 2012 tiliioni 2.7 zimetengwa kwa ajili ya kuhakikisha tatizo la maji linakwisha lakini bado kuna tatizo kubwa la upotevu wa maji mbali tu nakujunganishia watu kiholela kuna suala la miundombinu nimesema wakati nachangia kwenye ripoti ya *CAG* ambao na wewe upo waziri na ulikuwepo mwaka uliopita, Serikali imepata hasara bilioni 177 2019/2020 2018/2019 ulikuwepo ukiwa Naibu Waziri serikali imepata hasara bilioni 155 kwa miaka miwili kwa ajili ya upotevu wa maji. Serikali imepata hasara ya bilioni 332 sasa tuijilize kwa miaka kumi Serikali imepoteza kiasi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, na tunakuja hapa mnajibu hivi, tunapiga makofi ile hadhima ya kumtua ndoo mwanamke haijatimia kwasababu hakuna mikakati Madhubuti ya kupambana na tatizo la upotevu wa maji. Tunataka tujue mna mkakati gani mahususi ambao utakuwa *serious* kabisa kuondokana na tatizo la maji kwasababu hii wizara inatengewa pesa nydingi na bado tatizo la maji halijaisha kwa nini msiunde, hata timu ya wataalam ya kuhakikisha wanachunguza nini tatizo sio tena na wewe unakuja kulalamika sijui milioni 200 ni asilimia moja tu kati ya hela ambazo zimepotea.

MWENYEKITI: Haya ahsante sana

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya bilioni 300 nisipo rikizi natoa shilingi.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri ufanuzi.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiwa Waziri wa Maji faraja yako nikuona wananchi wanapata maji na ukiona Serikali imewekeza mradi wa maji halafu maji yanapotea wananchi hawapati maji, nimeweka wazi hapa lazima ujisikie vibaya, sasa sisi kama mkakati tulivyoingia katika wizara kipindi ambacho tupo Naibu Waziri tumekuta asilimia 44 ya upotevu wa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikakati ambayo tumeiweka juu ya kujenga na kuboresha miundombinu yetu ya maji sasa hivi tupo kwenye asilimia 36 kwa hiyo mikakati ambayo sisi tumewalekeza wakurugenzi wa mamlaka zetu za maji moja ni kupitia mapato yao kutenga asilimia 35 ya makusanyo wanayoyapata kujenga, kukarabati na kuboresha miundo mbinu ya maji ili kuvunda hiyo mivujo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kingine tumeenda mbali zaidi tumeingia hadi *performance contract* kwa muhandisi ama mkurugenzi wa mamlaka ya maji tukiona bado anashindwa kudhibiti masuala ya mazima ya mivujo na kushindwa kufika katika asilimia 20 huyo tutaachana naye katika kuhakikisha mamlaka zetu tunapata watu wafanisi ambaao wanaweza kuifanya kazi ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ester Bulaya.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, waziri bado ajajibu hoja hapa ya msingi, mnasema mmetoka kwenye asilimia 40.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Bulaya kwa kanuni zetu zilivyo ukisimama mara ya pili hautoi tena maelezo marefu

kwasababu umeshajibiwa ulichokitaka mwanzo kama haujardhika endelea sasa kutumia haki yako iliyopo kikanuni.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Spika natoa hoja ya kutoa shilingi na Waheshimiwa Wabunge waniunge mkono kwa maslahi ya Taifa tujadili ili suala kwa kina naomba kutoa hoja. (*Makof*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge waliosimama wamefika kumi kwa hiyo hoja imeungwa mkono. Sasa Waheshimiwa mkae ili wasimame Wabunge wanaotaka kuchangia kwenye hoja hii, Mheshimiwa Waziri wa Mazingira, Mheshimiwa Mchungahela na Mheshimiwa Kakunda.

MHE. ESTER A BULAYA: Halima Mdee huku kasimama.

MWENYEKITI: Nani huyo anayetaja huko bado sijafika mbona watu mnakuwa na haraka? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mbunge wa Kibiti Twaha, Mheshimiwa Simbachawene, Mheshimiwa Dkt. Christine, Mheshimiwa Halima Mdee haya tuenze na Mheshimiwa Mchungahela.

MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru ni mara ya kwanza kushiriki katika mijadala ya namna hii.

MWENYEKITI: Basi nitakupa nafasi baadaye kidogo Mheshimiwa Kakunda.

MHE. JOSEPH G. KAKUNDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa nafasi hii kwanza nieleze tu wazi mwanzo kabisa kwamba siungi mkono hoja ya Mheshimiwa Bulaya kwasababu mikakati ambayo imelezwa kwenye sera ya maji na mikakati ambayo imelezwa kwenye mkakati wa Taifa wa kuendelelza sekta ya maji unazitaka mamlaka za maji zote mijini, pamoja na *RUWASA* kuhakikisha kwamba wanafuatilia kwa ukaribu kama kuna upotevu wowote wa maji. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na wale ambao wanaiba maji kwa kuiunganishia wanatakiwa wakamatwe na

kuchukuliwa hatua za kisheria. Kwa hiyo, sasa kwasababu hatua hizo zimekuwa zikiendelea lakini mapambano ni sawasawa na polisi wanapambana na uhalifu. Uhalifu upo jambo hili kwa sababu mamlaka zimekuwa zinafanya kazi suala hili ni suala ambalo ni msisitizo tu kuweka Mheshimiwa Waziri kama ambao anauweka alivyosimimama mbele yetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti naunga mkono hoja za Mheshimiwa Waziri za kuwataka wataalam wa maji wahandishi wa maji waweke mkakati kuhakikisha kwamba upotevu wa maji unapungua ahsante sana. (*Makof!*)

MWENYEKITI: Ahsante sana, Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma.

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, siungi hoja ya Mheshimiwa Estar Bulaya naunga hoja ya Serikali kwasababu Mheshimiwa Waziri amesema upotevu wa maji umepungua mpaka sasa hivi na jitihada bado zinaendelea na wamesema kuwa wakurugenzi wote waangalie upotevu wa maji kama hawataendelea ataweza kuwajibisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naunga mkono wa Serikali siungi mkono wa Ester Bulaya ahsante. (*Makof!*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Halima Mdee.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Bulaya kwasababu kadhaa, mosi ni muhimu waziri akijibu hoja ajibu akitambua kwamba Chama cha Mapinduzi kimekuwa kimepewa dhamana nchi hii tokea tume pata uhuru kwa mantiki ya TANU na CCM tusizungumze kama vitu viwili tofauti. Lakini la pili mwaka 2010 mpaka 2015 asilimia 27 ya manunuzi yote ya nchi hii yalipelekwa kwenye sekta ya maji. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ikagundulika kwamba zaidi ya shilingi tirioni 2.7 zimeenda chini bila kuwa na tija,

hoja inayozungumzwa hapa mmezungumza mamlaka za maji lakini taarifa za CAG zinasema hata mamlaka za maji zenyewe hamzipatii yale mapato ambayo yanayotakiwa kupata kama hamjatoa mapato hamjawapa fedha bilioni zaidi ya mia nane hivi mnategemea mamlaka za maji zita-*perform* vipi? Na miaka yote mamlaka za maji zimeferi ndio maana tatizo limekuwa ni endelevu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na fedha zinazidi kuongezeka sasa kitu ambacho kinashauriwa kwamba kuwe na *task force* mahususi kwenda kufanya ukaguzi mahususi na maalumu ili tuje na jibu lenye tija la kusaidia Taifa *it doesn't make sense* Mheshimiwa Mwenyekiti namalizia kwamba tume-eject *tirions of money* kwenye maji lakini leo tukisema Wabunge ambaao majimbo yenu hayana maji nyosheni vidole watanyosha *60 percent*

MWENYEKITI: Haya Mheshimiwa Halima.

MHE. HALIMA J. MDEE: Kwa hiyo, hoja ya Mheshimiwa Bulaya ambayo naiunga mkono na naomba nimalizie...

MWENYEKITI: Ahh! ngoja kwasababu tangia umeanza kuzungumza mpaka sasa hujazungumza hiyo hoja wewe ambayo wewe unataka kuiunga mkono. Wewe unazungumza upotevu wa mapato kwa ujumla yeye ameenda mahususi.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa!

MWENYEKITI: Upotevu wa maji sasa unaongea kitu tofauti kabisa.

MHE. HALIMA JAMES MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Mheshimiwa Bulaya ni upotevu wa maji si ndiyo?

NAIBU SPIKA: Ndiyo!

MHE. HALIMA J. MDEE: Na gharama ambayo inatokana na upotevu wa maji na gharama ambayo inatokana na upotevu wa maji.

MWENYEKITI: Hapana, tuelewane vizuri. Hoja ya upotevu wa maji ukilileta na hoja ya upotevu wa mapato, ndio maana umeanza kwa kusema zimepotea trillioni kadhaa, yeye mwenye hoja hajazungumza habari ya trillioni kadhaa, kataja bilioni mia mbili na kitu kwa sababu amekwenda mahsus i kwenye hoja ya upotevu wa maji. Wewe umeipanua hoja sasa imekuwa ni kama haishikiki tena, yaani unataka kuingiza kila kitu kwamba fedha tulizopeleka zinapotea, hapana, tuelewane.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyezekiti, hoja inashikika.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Halima Mdee, muda wako ulikuwa umeshakwisha, kengele imegonga.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyezekiti, taarifa.

WABUNGE FULANI: Hakuna taarifa.

MWENYEKITI: Hata hivyo kengele ilikuwa imeshagonga. Mheshimiwa Simbachawene.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyezekiti, kwanza nimpungeze Waziri kwa majibu mazuri sana. Waziri anakwenda vizuri na Watanzania wanaomsikiliza na Waheshimiwa Wabunge humu ndani, makofi waliyopiga, ukiangalia nyuso zao unaona matarajio makubwa kwa kazi nzuri anayofanywa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyezekiti, hoja hapa ni upotevu wa maji, kiwango cha kawaida cha upotevu wa maji; katika masuala ya kihandisi huwa kuna *allowable allowance* kwenye jambo lolote lile. Sasa kwenye upotevu wa maji *the allowable* upotevu ni asilimia 20 ya maji yote utakayokuwa nayo. Hali ya upotevu wa maji ilikuwa asilimia 44 lakini kutokana na juhudzi za Wizara imeshuka mpaka sasa hivi upotevu ni asilimia 36. Kwa hiyo, kuna jitihada kubwa inafanywa na Wizara. Kama jitihada hizi zilizofanyika Mbunge

ha-appreciate kwamba kuna kazi imefanyika basi maana yake anataka wafanye vizuri zaidi na mtu akitaka watu wafanye vizuri zaidi si wazo baya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nadhani anachozungumza mto hoja, anachokizungumza Waziri ni kilekile ila ni lugha tu hapa imeshindwa kuwekwa vizuri ikaonekana kama ana nia mbaya. Mimi nadhani mto hoja ana nia nzuri, anatakiwa tu aungwe mkono lakini tumuunge mkono zaidi Waziri ili wafanye vizuri zaidi katika kupunguza upotevu wa maji. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Twaha Mpembewwe.

MHE. TWAHA A. MPEMBENWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi lakini niseme tu kwanza naunga mkono hoja ya Serikali siungi mkono hoja iliyokuwa imetolewa na Mheshimiwa Ester Bulaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapokuwa katika Serikali kuna taratibu ambazo huwa zinapaswa zifuatwe na pale ambapo kunakuwa kuna tatizo kuna mikakati maalum ambayo inapaswa iwekwe. Tumeona Mheshimiwa Waziri ameweza kutuelezea mikakati ambayo ameiweka kama Serikali au Wizara katika kuhakikisha kwamba upotevu ule wa maji ambao umezungumziwa unakwenda kupungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama hiyo haitoshi, kikubwa zaidi ambacho napenda nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla wake; upotevu wa maji ulikuwa kwa asilimia kadhaa na sasa umepungua mpaka kufikia asilimia 36. Kwa hiyo, tafsiri kubwa hapa ni kwamba sisi wote kwa pamoja ni lazima tuiunge mkono Serikali ili tuweze kuhakikisha kwamba tunakwenda kufanya vizuri katika kuweza kumtua mama ndoo kichwani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha msingi cha kukizingatia hapa ni kwamba uadilifu ni kitu cha msingi sana. Katika huu upotevu wa maji tuna mifano mizuri sana, tayari ameshatuambia Mheshimiwa Waziri wakati amefanya ziara

Morogoro kulikuwa na upotevu mkubwa sana wa maji, lakini siku wanakwenda kufanya ziara wakagundua kwamba kuna kiwanda kinatumia maji yale. Uadilifu huu ni sawasawa na uadilifu katika maeneo mengine; vyama vyaa siasa huwa vinapewa ruzuku, hajulikani ruzuku hizo zinafanya vitu gani. Kwa hiyo, mambo haya ya uadilifu lazima tuyazingatie sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba naunga mkono hoja ya Serikali, tusonge mbele tuweze kumtua mama ndoo kichwani. Ahsante. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Mchungahela.

MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono hoja ya Serikali na kulkataa hoja ya Mheshimiwa Bulaya kwa sababu mbili, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, Serikali imejielekeza kikamilifu kabisa katika kutekeleza majukumu mawili. Jukumu la kwanza ni hilo la kupunguza upotevu wa hayo maji lakini pia Serikali imejielekeza kwa nguvu zote katika kutatua hizo kero za maji. Kwa hiyo, ukiangalia kazi hizi zote mbili zinafanyika kwa wakati mmoja na Wizara moja. Hapo unaweza ukaona kwa jinsi gani Wizara hii illiyokuwa makini. Kwa hiyo, kuwaambia kwamba eti hawajafanya chochote itakuwa ni jambo la kutotendea haki Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naunga mkono hoja kwamba Serikali imefanya kazi kubwa sana na naikataa hoja ya Mheshimiwa Bulaya. Ahsante. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Selemani Jafo.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namuomba dada yangu, Mheshimiwa Ester Bulaya amrudishie ndugu yangu, Mheshimiwa Aweso shilingi yake kwa sababu kwanza tunafahamu nia ya Waziri, wakati

mwagine unasoma kutokana na nia ya mtu; *commitment* ya Waziri na timu yake unaona ni wazi kabisa wako *committed* kwa ajili ya kuwasaidia Watanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, suala zima la upotevu wa maji linahusiana na *management* katika maeneo mbalimbali. Wakati mwagine viongozi au watendaji walikuwa wakishindwa kutimiza wajibu wao na leo hii tunaona jinsi ambavyo Waziri amechukua hatua kadhaa hata kubadilisha baadhi ya watendaji lengo ni kuhakikisha kwamba Mamlaka za Maji zinatimiza vizuri wajibu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ni kudhibiti suala zima la wizi na uchakavu wa miundombinu. Kwa mfano, katika kipindi tulichotoka, zaidi ya miradi 800 ilitekelezwa lakini bajeti ya mwaka huu zaidi ya miradi 1,500 ikiwemo na ukarabati wa miradi hiyo itatekelezwa. Katika maeneo ya mijini zaidi ya miradi 114 inakwenda kukarabatiwa na mingine kujengwa upya. Kwa hiyo, unaona lengo la Wizara na Waziri jinsi wanavyojipanga kuhakikisha maji yanapatikana pamoja na suala zima la upotevu wa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Mheshimiwa Ester Bulaya ni nzuri lakini ukiangalia nia njema ya Mheshimiwa Waziri, mrudishie shilingi yake tuunge mkono juhudhi hii kubwa inayofanyika kwa ajili ya mustakabali wa nchi yetu. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Maji.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimuombe dada yangu, Mheshimiwa Ester, ukisoma maandiko ya dini yanasema yafaa nini imani bila ya vitendo. Kwa sababu hata kwenye jumbo lake kipindi yupo Bunda jitihada tulioifanya pale ni kubwa; ukienda Mugumu chujio tu peke yake ilikuwa ni changamoto, leo tumekwamua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la upotevu wa maji lazima itambulike hii ni changamoto ya kidunia. Leo kwa Afrika wapo ambao upotevu wa maji ni asilimia 40, sisi tupo

asilimia 36. Nilieleza hapa jitihada hizi zisiishie tu kwa Waziri, maendeleo ya sekta ya maji yanaanza na mimi, wewe na sisi sote. Suala la upotevu wa maji kuna changamoto ya uchakavu wa miundombinu, kwa mfano pale Dar es Salaam tumewapatia fedha sasa hivi wanakwenda kujenga mtandao takribani 1,600; hizi ni jitihada kubwa zinafanywa na Serikali. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa hiyo, nikuombe sana dada yangu, Mheshimiwa Ester Bulaya, tuendelee kuungana pamoja kujenga nchi yetu na kuhakikisha upotevu huu wa maji tunauondo kwa kiwango kinachokubalika. Ahsante sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Haya. Mtoa hoja ahitimishe hoja yake kama anarudisha shilingi ama anaendelea kushikilia Bunge liamue.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Sina haja ya kuwajibu wengine, lakini nijikite pale ambapo Mheshimiwa Simbachawene anasema upotevu wa maji unapungua; namba hazidanganyi na nimetoa takwimu hapa. Mwaka 2015 Serikali imepata hasara ya bilioni 155; mwaka 2019/2020 Serikali imepata hasara ya shilingi bilioni 177, hakuna kilichopungua, upotevu wa maji unaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nia njema ya kusaidia Taifa tunaona shida gani kuunda Kamati Maalum ya wataalam tukatafuta hiki chanzo? Mheshimiwa Waziri anasema hal mashauri zitenge asilimia 30 wakati mnajua makusanyo yote yanakwenda Serikali Kuu na hamrudishi. Pia unasema mamlaka za maji zitenge pesa wakati unajua kuna shilingi bilioni 850 hazijaenda. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye kitabu cha CAG amesema kati ya mamlaka 23, 21 zina upotevu mkubwa wa maji. Kama Taifa tunapata kigugumizi gani kuunda timu ya wataalam tukahakikisha tatizo hili linakwisha? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maslahi ya Taifa, kwa maslahi ya wananchi na wanawake wanaoteseka kutokana na kukosa maji safi na salama na pesa zinatengwa hakuna usimamizi, sitoi shilingi Bunge lako liamue wajue nani wanawatetea wananchi na akina nani wanaitetea Serikali. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Bulaya, umesema hutoi shilingi, kwa hiyo iko palepale maana yake Bunge halina cha kuamua kwenye hoja hiyo.

MHE. ESTER A. BULAYA: Hapana.

MWENYEKITI: Ndivyo ulivyo hitimisha hoja yako Mheshimiwa; umesema hutoi shilingi kwa hiyo iko palepale maana hoja ingekuwa ni unatoa shilingi Bunge liamue. (*Makofi/Kicheko*)

Waheshimiwa Wajumbe, nadhani hilo tunalimaliza kwa namna hiyo. Tunaendelea na Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula.

MHE. STANSLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, bado nilikuwa nacheka kidogo hapa, naona Mheshimiwa Ester amekumbana na upemo wa Tanga kule mpaka amepotea. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni ndogo sana na kwa sababu nimemuona na Waziri wa Fedha na Mipango hapa, nataka tu ufanuzi ambao kiukweli tukifanya mabadiliko utatusaidia sana. Nimeeleza kwenye maelezo yangu wakati nachangia kumekuwa na utaratibu wa utoaji wa *GN* kwa wakandarasi wanaopata mikataba mikubwa ya utekelezaji wa miradi ya maji hapa nchini. Mara nyingi sana *GN* imekuwa inatolewa pale tu mradi unaposainiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajikuta mkandarasi ana muda wa maandalizi na muda anaokwenda kuanza kazi,

mpaka anapokuja kuanza kazi kumekuwa na utaratibu wa kutoa *GN* kwa muda wa mwaka mmoja peke yake. Unakuta mkandarasi amepewa kazi ya miaka miwili, kwa hiyo miaka miwili katikati ya mwaka akiwa anaendelea na kazi ile *GN* inakuwa imekwisha. Matokeo yake analazimika kusimama kuanza tena kusubiri mpaka *GN* nyingine itakapotoka, tumekuwa tunachelewa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine tunaitupia lawama Wizara au Waziri wa Maji kwamba miradi inacheleweshwa kumbe kuna mfumo ambao unatufanya tuchelewe sana. Kwa nini tusiwe na utaratibu wa kutoa *GN* ya muda wa uhai wa mkataba na miezi 12 ya ziada ambayo mkandarasi anakuwa bado kwenye muda wa maandalizi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na nakusudia kushika shillingi kama Mheshimiwa Waziri hatakuwa na majibu mazuri zaidi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, ufanuzi. Naona Mheshimiwa Waziri wa Fedha anataka kutoa ufanuzi.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja anayoisema Mheshimiwa Mbunge ina maana kubwa na uhalisia. Jambo hili lillishafika kwa Mheshimiwa Rais kwa maana ya miradi mingi kukwama na alielekeza hatua zichukuliwe kwenye jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi pamoja na Mheshimiwa Waziri wa Maji tukiwa na wataalam wetu tulishakaa kulifanyia kazi jambo hili na kwa sababu uamuzi huu ulipitia ngazi ya Baraza la Mawaziri kufuata utaratibu huu, tunalifanyia kazi na Mheshimiwa Rais ameelekeza kazi ikamilike kabla ya bajeti kuu ya Serikali ili uamuzi unaofaa ambao utasababisha miradi iweze kufanyika kwa wakati na kuepusha gharama ambazo zinatokana na kusubiriwa kwa mchakato huu uweze kupatiwa ufumbuzi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Mbunge aridhie tu kwamba suala hili liko katika hatua za mwisho na tunaamini tunapoanza mwaka mpya wa fedha tutakuwa tumepata majibu ambayo yatasaidia Waziri wa Maji aweze kutekeleza miradi kwa wakati kama yeche aliyeleta mapendekezo kwetu Wizara ya Fedha. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mabula naona ameridhika. Mheshimiwa Waziri mtakapokuwa mnaangalia hao wakandarasi wa maji muangalie na wa ujenzi pia, changamoto zinafanana. (*Makofii*)

Tuendelee na Mheshimiwa Charles Kajege.

MHE. CHARLES M. KAJEGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina hoja yangu ndogo; Serikali imeanzisha miradi mikubwa ya maji kutoka katika Maziwa makubwa ya Victoria, Tanganyika na Nyasa kwenda katika maeneo ya mbali ambayo hayana maji. Hata hivyo, kuna maeneo kandokando na haya maziwa bado yana matatizo makubwa ya maji. Je, Serikali itaaniszisha lini miradi kuhakikisha kwamba hata maeneo yaliyo karibu na haya maziwa yanapata maji ili kumaliza tatizo hili?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Maji, ufanuzi.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimponeze Mheshimiwa Mbunge, lakini kubwa niseme jukumu la kuwapatia maji ni la Wizara yetu ya Maji. Maelekezo mahsus ambayo tumeyapata ni kwamba wananchi ambaa wanaishi pembezoni mwa maziwa lazima wanufaiki na rasilimali iliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sisi kama Wizara na hata ukitazama katika kitabu chetu cha bajeti tumeweka dhamira ya dhati ya kuhakikisha kwamba tunawapata Wahandisi Washauri kwa ajili ya kuanza ujenzi wa miradi katika

Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa pamoja na Ziwa Victoria na zaidi ya vijiji 413 vinakwenda kunufaika na rasilimali za maji zilizopo. (*Makof*)

MWENYEKITI: Naona Mheshimiwa Charles ameridhika. Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Natarajia kushika shilingi ya Waziri kama hatanijibu vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa mchango wangu nilichangia nikamuomba Mheshimiwa Waziri kwamba atupe majibu mazuri wakati ana-*wind up* kuhusiana na suala la uchimbaji wa visima. Nimejaribu kufanya *research* ndogo leo mchana; visima vinavyochimbwa na Serikali ukichukua kwa mfano Mbeya, kisima cha *standard* ya maji ya kawaida kinachimbwa kwa shilingi milioni 85 wakati mtu akichimba Mwakareli kwa utaalam uleule anachimba kwa shilingi milioni 14. Ukichimba Geita ni shilingi milioni 40, utaalam uleule ni shilingi milioni tisa. Hapa Dodoma shilingi milioni 40; ukichimba kwa kawaida utaalam uleule inakuja shilingi milioni nane mpaka tisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sisi tunaotoka maeneo ambayo hayana maji tunadhani pesa hizi zingechimbwa kulingana na gharama zinazochimbwa na watu wengine, tungekuwa na visima vingi na tatizo hili la maji lingepungua. Ndiyo maana namtaka Mheshimiwa Waziri aniambie ana mkakati gani mzuri wa kuweza kunusuru hizi bei na kurudi kwenye bei za kawaida? Ukiwaliza watu wanasesma kuna makorokoro ya tafiti, utalaam, wakati mwengine yanakuwa ya uongo na maji wanakosa. Mheshimiwa Waziri anieleze ili niweze kukubaliana na yeje kuachia shilingi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Maji, ufanuzi.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mjumbe kwa dhamira yake ya dhati na sisi kama Wizara tunafanya mageuzi makubwa sana katika Wizara yetu ya Maji. Sisi tuna kitengo chetu ambacho ni mahsus kwa ajili ya uchimbaji visima vijijiini kinaitwa *DDCA*. Hata hivyo, baada ya kufanya ziara na kufika na kuhoji baadhi ya mambo tunakwenda kuifumuafumua *DDCA*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, tumeona kweli gharama zinazotumika kwa ajili ya uchimbaji visima zinakuwa kubwa. Kwa mfano, kisima ambacho kingeweza kuchimbwa kwa wiki moja wanatumia mwezi mmoja, lakini unakuta ni janjajanja tu ya wataalam katika kuongeza *per diem*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge, hilo jambo tumeliona na kesho tutakuwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu tunakutana na Wahandisi wote tunakwenda kukabidhi *design manual* kwa wataalam wetu katika kuhakikisha kwamba tunafanya mageuzi na mapinduzi makubwa katika Wizara yetu. Kwa hiyo, nikuombe Mheshimiwa Mbunge utuunge mkono twende tukafanye kazi ili bajeti yetu iweze kupita. Ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Musukuma amekubaliana na ufanuzi wako.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kifungu 1002 – <i>Finance and Accounts Unit</i> ...	Sh.1,413,479,000
Kifungu 1003 – <i>Policy and Planning Unit</i>	Sh. 1,028,354,000
Kifungu 1004 – <i>Government Communication Unit</i> ...	Sh.485,692,000
Kifungu 1005 – <i>Legal Services Unit</i>	Sh.524,128,000
Kifungu 1006 – <i>Procurement Management Unit</i> ...	Sh.978,439,000
Kifungu 1007 – <i>Management Information System</i>	

Unit Sh.
527,326,000

(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kifungu 1007 – Management Information System
Unit Shs. 527,326,000

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge hasa wa Chama cha Mapinduzi ambao ni kazi yao kuitisha bajeti kwa neno "ndiyo," tunaweka Kumbukumbu Rasmi za Bunge. Msipoitikia hatutaona kwenye kumbukumbu kwamba mliitikia. (*Kicheko*)

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kifungu 1008 - <i>Internal Audit Unit</i>	Sh. 581,790,000
Kifungu 1009 - <i>Project Preparation Coordination and Delivery Unit</i>	Sh. 726,189,000
Kifungu 2001 - <i>Water Resources</i>	Sh. 6,477,600,500
Kifungu 2003 - <i>Water Laboratory</i>	Sh. 2,440,645,000
Kifungu 3001 - <i>Water Supply and Sanitation Division</i>	Sh. 9,893,350,000
Kifungu 5001 - <i>Water Development and Management Institute</i>	Sh. 3,864,421,000
Kifungu 6001 - <i>Drilling & Dam Construction Agency</i>	Sh. 1,044,390,807

(Vifungu viliviyotajwa hapo juu Vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

KITABU CHANNEL

MIPANGO YA MAENDELEO

FUNGU 49 – WIZARA YA MAJI

Kifunyu 1001 - Administration and Human

Resource Management Sh.
4,300,000,000
Kifungu 1003 - *Policy and Planning Unit*.....Sh. 10,700,000,000
Kifungu 2001 - *Water Resources*.....Sh. 37,500,000,000
Kifungu 2003 - *Water Laboratory*.....Sh. 4,700,000,000
Kifungu 3001 - *Water Supply and Sanitation Division*Sh. 589,430,000,000

(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

NDG. ASIA P. MINJA – KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

MWENYEKITI: Bunge linarejea.

(Bunge liliujea)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Mtoa hoja, taarifa.

TAARIFA

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nitoe shukrani zangu kwako pamoja na Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji kwa mujibu wa Kanuni 123.3 (a) na (b) ya Kanuni ya Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020 naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi, limekamilisha kazi zake. Naomba kwa sasa taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.
(Makofi)

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Sasa kwa taratibu zetu nitawahoji Waheshimiwa Wabunge wanaoafiki hoja ya Mheshimiwa Jumaa Hamidu Aweso, Waziri wa Maji kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

(Hoja Ilitolewa lafikiwe)

(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa
Mwaka wa Fedha 2021/2022 - Wizara ya Maji
yalipitishwa na Bunge)*

MBUNGE FULANI: Mwongozo wa Spika.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nichukue fursa hii kwa niaba yenu wote kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Timu yake yote kwa kazi nzuri waliyoifanya, maana Wabunge Wengi michango yenu mlikuwa mnapongeza na pia michango yenu mingi ilikuwa na nia ya kuboresha hapa na pale. Kwa hiyo, pamoja na pongezi hizo, tuwatakie kila la heri kwenye utekelezaji wa yale mliyoyaahidi, kwa sababu Bunge limewapa idhini ya kutumia fedha kadri mlivyoomba. Kwa hiyo, tunaamini yale yote mliyoyaahidi mtayatekeleza na tunawatakia kila heri katika utekelezaji huo.

Waheshimiwa Wabunge, nanyi mmefanya kazi kubwa sana. Nichukue fursa hii kuwashukuru sana Kamati yetu ya kudumu ambayo Wizara hii ipo chini yake, mmefanya kazi nzuri, mmefanya kazi kubwa ya kuwashauri na kuwasimamia Wizara hii mpaka tumeweza kufika sehemu ambayo kila mtu anapata matumaini kwamba wananchi katika eneo lake la uwakilishi wana uwezekano wa kupata maji. Kwa hiyo, mmefanya kazi nzuri kwa niaba yetu sote. *(Makof)*

Pia Waheshimiwa Wabunge mbalimbali ambao mmeshiriki mjadala huu, mmechangia kwa hisia na Mheshimiwa Waziri kama alivyosema hapa, sitaki kurudia ile misemo yake ilikuwa inaashiria namna ambavyo yeye na

Naibu Waziri wamejipanga kuhakikisha kwamba hakuna Mbunge anakuwa anasimama sana saa ya maswali humu ndani kwa maana kwamba kila mtu kwake kutakuwa mambo mazuri. Kwa hiyo, tunawashukuru sana. Vile vile mawazo yaliyotolewa kama Waziri alivyosema, mkayafanyie kazi. Mheshimiwa Waziri yapo mambo mengi ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyasema mnayotakiwa kuyafanyia kazi kama Wizara na Watendaji wenu. Tunawatakia kila heri.

Waheshimiwa Wabunge, wakati nikisimama hapa nilimwona Mheshimiwa Hussein Amar akiomba mwongozo kuashiria kwamba pengine siku ya leo namna Bunge liliyoendesha shughuli zake kuna mahali kanuni imevunjwa na kwa hivyo anataka kujua kama jambo hilo linaruhusiwa ama aliruhusiwi.

Mheshimiwa Hussein Amar.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kanuni ya 76 ninasimama kutaka mwongozo wako kwa sababu kumekuwa na mkanganyiko. Pindi Waziri anapo-*wind-up* hapo, anapofikia mwisho anasema anatoa hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mkanganyiko huu unakuja, tuliambiwa kwamba Waziri anaposema anatoa hoja, Waheshimiwa Wabunge ambaio sio Mawaziri wasisimame, lakini wewe umesema, Waziri! Alipotoa hoja, wakasimama Mawaziri, ukasema kwamba wale ambaio waliyokuwa wakilalamikia kwenye majimbo yao mambo yamekuwa mazuri lakini hawakusimama. Tunakuwa na mkanganyiko, ipi sahihi? Naomba mwongozo wako. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, amesimama Mheshimiwa Amar kama nilivyokuwa nimesema, kanuni yetu ya 76 inataka Mbunge ambaye anafikiri kuna jambo limefanyika ambalo linaruhusiwa ama haliruhusiwi. Kwa hiyo anapoomba mwongozo swali lake kwa kitii, linakuwa

kwamba je, jambo hili linaruhusiwa ama aliruhusiwi? Sasa ye ye ameuliza kwamba jambo lipi ni sahihi kati ya hayo mawili?

Mheshimiwa Spika alivyotoa hayo maelezo, hakusema kwamba ukisimama Mbunge inakuwaje, hapana; alisema Serikali kwa kawaida ndiyo wanapaswa kusimama wote kimsingi kwa sababu wanaunga mkono mawazo hayo; lakini Mbunge ambaye anaunga mkono hoja, pia anaruhusiwa kusimama. Siyo kwamba haruhusiwi kusimama. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, baada ya ufanuzi huo, naahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 11.30 jioni Bunge lilahirishwa hadi Siku ya Jumanne,
Tarehe 11 Mei, 2021 Saa Tatu Asubuhi)*